# Nipashe

Jumanne Desemba 24 , 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580109

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



Albinism Hotline

- Jifunze kuhusu Ualbino
- Toa taarifa za nia ovu dhidi ya wenye Ualbino

0800 75 00 50

Piga simu bure

ARIGATOU INTERNATIONAL | GNRC

CEFA

215544702




## JPM aagiza waliomaliza JKT wenye shahada kupewa ajira

UKURASA 3

# Katibu Mkuu akemea rushwa ngono vyuoni

**ASEMA** ni aibu kwa taifa, awaonya wahadhiri wenye tabia hizo, mkakati kudhibiti waandaliwa... *Endelea ukurasa wa 2*



Mchuuzi wa nguo ambaye jina lake halikupatikana, akimjaribisha shati mtoto yakiwa ni maandalizi ya sikukuu ya Krismasi, huku mzazi wake akiangalia Mtaa wa One Way jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**LHRC YAHADHARISHA POLISI KUHUSU MAGOTI**
WATETEZI wa Haki za Binadamu Tanzania, wametoa mambo 10 yanayopaswa...

**UKURASA WA 4**

**BULAYA AFUNGUKA NDOA YAKE MAHAKAMANI**
MBUNGE wa Bunda, Ester Bulaya, amedai mahakamani katika kesi ya uchochezi...

**UKURASA WA 7**

**KANUNI ZAREKEBISHWA UDHIBITI TAKA HATARISHI**
WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)...


## WAZIRI ACHARUKA UJENZI WA HOSPITALI

UKURASA 3

# Kamwelwe ahesabu siku nane kuzima laini simu

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** YANGA, MBEYA CITY HAPATOSHI UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Katibu Mkuu aonya rushwa ngono vyuoni

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, amekemea matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia katika vyuo vya elimu ya juu hasa vitendo vya rushwa ya ngono.

Dk. Jingu alikemea tabia hiyo jijini Dodoma wakati akifungua kikao kilichowakutanisha wakuu wa vyuo vya elimu ya juu kilichohusu namna ya kupambana na ukatili wa kijinsia katika maeneo ya vyuo vya elimu ya juu.

Alisema tatizo la ukatili wa kijinsia limekuwa likishamiri katika vyuo vya elimu ya juu kwa kuwa imeripotiwa kuwa wahadhiri wengi wanatumia madaraka yao kuwalazimisha wanafunzi kufanya nao ngono kwa lengo la kuwafaulisha mitihani.

Alisema sio wanafunzi pekee wanaokumbana na vitendo hivyo, bali hata wafanyakazi wanaofanya kazi katika vyuo vya elimu ya juu wanakumbwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia hivyo nguvu ya ziada inahitajika katika kupambana na vitendo hivyo vyuoni.

"Tumeshuhudia uwepo wa matukio ya ukatili wa kijinsia katika vyuo vyetu vya elimu ya juu hasa rushwa za ngono, hili sio sawa tunatakiwa kulikemea kwa nguvu zote," alisema Dk. Jingu.

Dk. Jingu alisema katika kuhakikisha wanapambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, serikali na wadau wanatekeleza mpango mkakati wa kitaifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ili kuhakikisha vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia nchini vinatokomezwa kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

Vile vile, amewataka wakuu wa vyuo kuhakikisha wanatoa elimu na maelekezo ili kujenga uelewa wa kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa kwa wanafunzi wa kike kwa ajili ya kuepuka matakwa ya wahadhiri wanaotumia hila kuendekeza ukatili wa kingono vyuoni.

Aliwataka wakuu wa vyuo kutekeleza agizo la Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, la kuanzisha madawati ya jinsia katika vyuo vyao ili kuondokana na vitendo vya kikatili na kujenga mazingira yaliyo salama katika vyuo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Uelimishaji kutoka Taasisi ya Kupambana na Kutokomeza Rushwa (Takukuru), Asseri Mandari, alisema taasisi hiyo imejipanga kupambana na tatizo hilo kwa kuanzisha kampeni inayosema "Vunja Ukimya Ondoa Rushwa ya Ngono" itakayosaidia kuondokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa kuzuia rushwa ya ngono.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Jinsia kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Lulu Mahai, alisema kuwa vyuo vya elimu ya juu vina wajibu mkubwa wa kutoa elimu ya kupambana na vitendo vya kikatili kwa wanafunzi na wafanyakazi na wanaamini baada ya kikao hicho watarudi na kuanzisha madawati ya jinsia na kamati mbalimbali zitakazosaidia kupambana na matukio ya ukatili wa kijinsia katika taasisi na vyuo vyote nchini.




Gari linalofanya safari zake kati ya Tegeta Nyuki na Simu 2000, Dar es Salaam, likiwa ndani ya kituo cha mabasi Ubungo likibeba abiria wa kwenda Moshi na Arusha, huku wakilalamikiwa kupandisha nauli kutoka Sh. 25,000 mpaka Sh. 50,000, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kamwelwe asubiri siku 8 kuzima simu

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesisitiza kuwa ifikapo Desemba 31, mwaka huu, laini zote za simu ambazo hazijasajiliwa kwa alama za vidole zitafungwa.

Kutokana na msimamo huo, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amebakiza siku nane kuanzia sasa kutekeleza uamuzi huo wa serikali.

Sambamba na kubakiza siku hizo, Kamwelwe amesema hakuna tatizo linalowafanya watu washindwe kusajili na kwamba watakashindwa kufanya hivyo, watakuwa wamekaidi, hivyo watakosa mawasiliano.

Kamwelwe alitoa msimamo huo jana wakati wa utiaji saini mkataba wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Umoja wa Posta Afrika (PAPU) linalotarajia kujengwa mkoani Arusha kwa gharama za Sh. bilioni 33.5. Utiaji saini huo ulifanywa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na PAPU.

Alisisitiza kuwa suala hilo si la masihara na badala yake watazifungia laini zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa kwa alama za vidole.

"Yaani hapa nasubiri siku ifike tu ili nizime laini na nitakata laini zote ambazo hazijasajiliwa. Lengo letu ni kupunguza uhalifu kwa njia ya simu. Unakuta mtu mmoja anamiliki zaidi ya laini 20, zote za nini?" Alihoji.

"Hakuna cha sintofahamu hapa, Desemba 31 tunakamilisha usajili na tutafunga laini zote ambazo zitakuwa hazijasajiliwa. Niwaambie umuhimu wa jambo hili, tumefanya hivi kwa sababu Watanzania wengi wanaibiwa fedha zao kutokana na utitiri wa laini," alisisitiza.

Wiki iliyopita, Mkurugenzi Mtendaji wa TCRA, James Kilaba, alisema tayari watu milioni tatu wana namba za usajili wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) lakini hawajajitokeza kusajili.

Alisema kati ya watu hao we-

INAENDELEA UK 8

## Watetezi haki wahadharisha wajibu Polisi

**Na Mwandishi Wetu**

WATETEZI wa Haki za Binadamu Tanzania, wametoa mambo 10 yanayopaswa kufanywa na Watanzania, kuleta uwajibikaji kwa Jeshi la Polisi linalodaiwa kumshikilia kwa siku nne Ofisa wa Kitengo cha Elimu kwa Umma wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Tito Magoti.

Pia wametaka Tito na wenzake kufikishwa mahakamani haraka vinginevyo watachukua hatua za kisheria za kimahakama kuwalazimisha kutii sheria zinazomlinda mtuhumiwa.

Mwishoni mwa wiki, Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum, Lazaro Mambosasa, alitoa taarifa kuwa wanamshikilia na kueleza kuwa atatoa taarifa kamili, lakini hadi sasa mwajiri wake na familia yake hawajui yuko kituo gani cha polisi.

Juzi, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mambosasa aliwataka waandishi wa habari kuwa na subira na kwamba leo (jana) angetoa taarifa kuhusu suala hilo, lakini alipoulizwa alisema lipo makao makuu ya polisi ndiyo wanalizungumzia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na LHRC, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) na Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu (WHRDs), watuhumiwa wote wanaokamatwa na polisi wana haki ya dhamana na haki ya kuhojiwa mbele ya mwanasheria, ndugu, jamaa na watu wa karibu.

Mambo hayo ni kulitaka Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama kuwajibika kwa wananchi kwa kutoa taarifa za alipo Magoti ili aweze kupata haki zake kwa mujibu wa sheria au limwachilie kwa kuwa hadi sasa baada ya siku nne haijulikani anatuhumiwa kwa kosa gani.

Mitandao hiyo imesema Jeshi la Polisi ni chombo kilichowekwa kwa ajili ya ulinzi wa raia na mali zao, halipaswi kutumika kuwakandamiza wananchi.

Watetezi hao wamezitaka asasi za kiraia, watetezi wa haki za binadamu, waandishi, mahakama na wadau wote wapenda haki,

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA



Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, akizungumza na wakazi wa Kijiji cha Mchangani, katika Kisiwa Kome, wilayani Sengerema mkoani Mwanza, alipotembelea kijiji hicho wakati wa kukagua usambazaji wa umeme vijijini. **PICHA: ZUENA MSUYA**

# JPM aagiza waliomaliza JKT wenye shahada za chuo kikuu kuajiriwa

**Na Happiness Shayo**

RAIS John Magufuli ameagiza vijana wote wenye elimu ya shahada ya kwanza waliohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) "Operesheni Magufuli" kupewa ajira katika taasisi mbalimbali za serikali.

Ujumbe huo ulitolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro, katika mkutano na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana.

"Serikali imekuwa ikiwajengea vijana uadilifu, umoja, mshikamano, moyo wa kujitolea, moyo wa uzalendo, nidhamu na ari ya kupenda kufanya kazi kwa kuwaingiza kwenye mafunzo ya Jeshi la Kujenda Taifa, hivyo kwa kutambua mchango wao, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Magufuli ameagiza wapewe ajira," alisema.

Alitaja sifa za vijana waliohitimu JKT kuwa ni lazima wawe wametumikia kwa kipindi kisichopungua miaka miwili na kwamba wanatakiwa kuwasilisha taarifa zao binafsi, vyeti vya elimu, taaluma na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya JKT katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia barua pepe ya ps@utumishi.go.tz.

Vile vile, Dk. Ndumbaro aliwaasa waajiri wanaowarejesha kazini watumishi wa umma waliogushi vyeti vya elimu na taaluma kwa visingizio kwamba waliondolewa kimakosa au waliajiriwa kabla ya Mei 20, 2001 kwa sifa ya elimu ya darasa la saba.

"Serikali haitosita kumchukulia hatua mwajiri yeyote atakayekiuka maelekezo halali yaliyotolewa na serikali kuhusu hatua zilizochukuliwa dhidi ya watumishi walioghushi vyeti," alionya.

Akizungumzia suala la udanganyifu na upendeleo katika upandishwaji vyeo, Dk. Ndumbaro alisema ofisi yake imebaini baadhi ya waajiri kuwasilisha taarifa za uongo Ofisi ya Rais-Utumishi ili kuwapandisha vyeo watumishi kwa lengo la kuwanufaisha baadhi yao bila kuwa na vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zinazosimamia utumishi wa umma.

"Ofisi yangu itaendelea kuwachukulia hatua stahiki waajiri watakaobainika kufanya udanganyifu kwa madhumuni ya kuipotosha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili iweze kutoa vibali vya kuwapandisha vyeo watumishi isivyostahili." Aliwataka maofisa utumishi nchini kufanya kazi kwa weledi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma badala ya kuwa chanzo cha kero na matatizo ya kiutumishi.

# Jafo acharuka kukwama kwa ujenzi wa hospitali

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Vijijini mkoani Ruvuma, Saimon Bulenganija pamoja na wakuu wake wote wa idara kuandika barua za kujieleza sababu za kukwamisha ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Hospitali hiyo inajengwa eneo la Mpitimbi kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5, lakini bado ujenzi haujakamilika.

Alitoa agizo hilo alipofanya ziara ya kutembelea miradi mbalimbali ya maendeleo mkoani mkoani Ruvuma na pia amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, pamoja na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kuhakikisha wanafanya uchunguzi ili kubaini kama kuna ubadhirifu wa fedha ili wahusika wachukuliwe hatua.

Alitoa agizo hilo baada ya kukagua ujenzi wa hospitali hiyo ambayo ilipaswa kukamilika Desemba, mwaka huu.

"Yaani hapa hakuna chochote kilichofanyika, maeneo mengine yote ambayo Rais Dk. Magufuli ametoa fedha kwa ajili ya kujenga hospitali wamemaliza nyie bado, sasa naagiza CMT yote na kuanzia Mkurugenzi wenu wa halmashauri muandike barua za kujieleza ni kwa nini mmefikia hapa, nani kasababisha na kwa nini usichukuliwe hatua kila mtu aandike maelezo yake hakuna copy and paste (kunakiri na kubandika)," alionya.

"Ninawaambieni sitasita kuwafukuza kazi wakuu wa idara wote waliohusika kukwamisha ujenzi wa hospitali hii, haiwezekani Rais anatoa fedha halafu baadhi ya watu wanafanya wanavyotaka," alisisitiza Waziri Jafo.

Kabla ya kutoa agizo hilo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Vijijini, Idd Mwakibuka, akitoa taarifa ya ujenzi wa hospitali hiyo, alisema wanahitaji kiasi kingine cha fedha Sh. milioni 425 ili waweze kukamilisha kwa asilimia 100.

# Kamwelwe aipa kibano TPA

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, ameiagiza Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kuhakikisha gawio mwakani linaongezeka na kufikia Sh. trilioni moja.

Waziri alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akizindua bodi hiyo akiwataka kuhakikisha gawio linapanda na kufikia kiasi hicho.

Pia aliitaka bodi hiyo kuongeza mapato kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa katika ukusanyaji wa mapato kutokana na utofauti uliopo kwenye risiti zinazotolewa.

"Hela inayopatikana ni kubwa kuliko inayoingia serikalini, hivyo bodi naomba mkasimamie hayo mapato," alisema Kamwelwe.

Aliongeza: "Kuboresha mapato na kutoa gawio zaidi sambamba na wingi wa uwezo na shehena."

Pia alisema kuna changamoto ya walinzi kupigwa vita na wafanyakazi wenzao pamoja na wafanyabiashara, na kuitaka bodi kwenda kulisimamia jambo hilo.

Alisema Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ambayo ndiyo mmiliki wa TPA imeanzishwa kwa mujibu wa sheria ya uanzishwaji wake namba 17 ya mwaka 2004 chini ya usimamizi wa bodi ya wakurugenzi kwa niaba ya serikali.

"Mnalo jukumu la kutekeleza sera za serikali katika kuhakikisha kuwa TPA inatoa huduma kwa ufanisi na tija ya hali ya juu," alisema.

Aliwataka wakasimamie utekelezaji wa mpango mkakati wa tatu wa mamlaka (2015/16-2020/21) ambao unaelekea nwishoni na kuwa tayari kuanzisha mpango utakaofuata 2020/21-2025/26.

Waziri alisema utekelezaji wa sera ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda ni kulifikisha taifa kuwa uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

"Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam unaoendelea ili ukamilike mwakani kama ilivyopangwa ikiwa ni pamoja na ununuzi wa mitambo mikubwa," alisema.

Alisema ukarabati wa bandari nyingine za mwambao wa bahari hususani Tanga na Mtwata unaendelea pamoja na mitambo.


## SHIRIKA LA UMEME TANZANIA

TANESCO We light up your life

## TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) lina watangazia wateja wake wote zikiwemo Taasisi za Serikali na binafsi, Mashirika ya umma, Viwanda na watu binafsi wenye madeni ya bili za umeme kuwa;

TANESCO inaendesha zoezi maalum la kusitisha huduma ya umeme kwa wateja wote wanaodaiwa bili za umeme.

Wateja wote wenye madeni wanatakiwa kulipa bili zao haraka ili kuepuka adha ya kusitishiwa huduma ya umeme katika msimu wa sikukuu.

**TANESCO HAITATOA TAARIFA NYINGINE ZAIDI YA TANGAZO HILI.**

**Imetolewa Na:**
**OFISI YA UHUSIANO**
**TANESCO MAKAO MAKUU**
**18 Disemba2019**

# Bulaya adai ndoa yake haijavunjika

**Na Hellen Mwango**

MBUNGE wa Bunda, Ester Bulaya, amedai mahakamani katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo wanane wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kuwa bado ana ndoa na mume wake Afande Gustav Babile, kwa sababu ndoa ya kanisani haivunjiki.

Kadhalika, amekiri kuwa yeye na Babile ni wanandoa na kwamba ndoa yao bado iko hai, lakini anaishi Mbweni, jijini Dar es Salaam.

Bulaya ambaye ni mwandishi wa habari mwandamizi wa zamani wa magazeti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), alitoa madai hayo jana wakati anahojiwa na upande wa Jamhuri mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na jopo na mawakili wa serikali sita, Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, Wakurugenzi wa Mashtaka Wasaidizi, Faraja Nchimbi, Pendo Makondo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, Mawakili wa Serikali, Jacqline Nyantori na Salim Msemo.

Akihojiwa na Wankyo, kuhusu maisha yake ya familia, mshtakiwa huyo alidai kuwa alifunga ndoa mwaka 2003 na kwamba kwa sasa anaishi Mbweni na Mbunge wa Kawe, Halima Mdee ni jirani yake.

Akihojiwa na Nchimbi, kuhusu hati yake ya kusafiria alidai, katika hati hiyo hakuna mahali popote palipogongwa muhuri pakionyesha alisafiri nje ya nchi kati ya Februari 16 hadi 28 mwaka 2018.

Alidai alichoieleza mahakama ni kwamba, Februari 16, mwaka jana, aliwahi kuondoka katika mkutano wa kufunga kampeni kwa kuwa Mdee alikuwa anaumwa, hivyo walienda kujiandaa na safari ya kwenda kwenye matibabu Afrika Kusini.

Mkutano huo ulifanyika katika viwanja vya Buibui, Mwananyamala, Dar es Salaam.

Alidai hajawahi kuieleza mahakama siku waliyosafiri na katika hati yake ya kusafiria imegongwa muhuri katika ukurasa wa 17.

Katika hatua nyingine alidai, hakuna sheria inayoruhusu chama cha siasa kuhamasisha wafuasi wake kudai haki kwa maandamano ama vurugu.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 20 na kusikiliza mfululizo hadi Januari 24, mwakani na shahidi wa 10 wa upande wa utetezi anatarajiwa kutoa ushahidi wake.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika na Katibu Mkuu wa zamani, Dk. Vicent Mashinji.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche na Ester Matiko.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama, wote wanadaiwa kuwa, Februari 1 na 16, mwaka jana, Dar es Salaam walikula njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko la kutawanyika.

Pia wanadaiwa kuwa Februari 16, mwaka huu katika barabara ya Kawawa, Kinondoni Mkwajuni washtakiwa hao wakiwa na wenzao ambao hawapo mahakamani walikiuka tamko la kuwataka kutawanyika la Ofisa wa Polisi SSP, Gerald Ngiichi kwa kugoma kutawanyika na kusababisha uvunjifu wa amani.

Inadaiwa kugoma huko kulisababisha hofu na hatimaye kifo cha Akwilina Akwiline na majeruhi kwa askari wawili ambao ni H.7856 PC Fikiri na E.6976 CPL Rahim Msangi.



Meneja Biashara na Maendeleo wa Kampuni ya Unga wa Ngano Camel Flour, Tawaqal Sumba (katikati), akimkabidhi mwanzilishi wa kituo cha kulea watoto yatima pamoja na wanaoishi katika mazingira magumu, Rahma Kishumba, msaada wa unga wa ngano mifuko 20 ya kilo 24 uliotolewa na kampuni hiyo, ikiwa ni sehemu ya shughuli za kuisaidia jamii zinazoendelea kufanyika sehemu mbalimbali nchini. Makabidhiano hayo yalifanyika kituoni hapo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TRA yawakumbusha msamaha riba

**Na Juster Prudence**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imewataka walipakodi wote waliopewa msamaha wa riba na adhabu kumaliza madeni yao kabla ya Desemba 31, mwaka huu.

Mamlaka hiyo ilitoa kauli hiyo katika tangazo lake kwa vyombo vya habari jana na kwamba msamaha huo ulibuniwa ili utekelezwe ndani ya muda maalumu.

Kwa mujibu wa Kaimu Kamishna Mkuu wa TRA, Msafiri Mbibo, alisema mlipakodi yeyote ambaye alipewa msamaha chini ya agizo namba 282A, 2018 ya usimamizi wa kodi inayohusu msamaha wa riba na kodi na akashindwa kutekeleza masharti ya mkataba baada ya muda uliotolewa, msamaha huo utabatilishwa na atalazimika kulipa kodi kama ilivyokuwa mwanzo.

Alisema ifikapo Januari 1, mwakani, Kamishna Mkuu atachukua hatua za kukusanya kodi dhidi ya walipa kodi wote watakaoshindwa kuheshimu msamaha waliopewa na kukusanya kodi stahiki, riba, na adhabu zote bila kujali kama walipewa msamaha mwanzo.

Walipakodi waliopewa msamaha huo ni wale waliomba msamaha wa riba na adhabu za kodi kwa Kamishna Mkuu, waliopatiwa msamaha wa riba na adhabu, waliingia makubaliano na Kamishna Mkuu ya kusamehewa riba na adhabu za kodi kama ilivyoainishwa katika agizo la namba 282A, 2018 ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi na waliokubali kulipa kodi ya msingi iliyokadiriwa kwa mkupuo au kwa awamu.

Msamaha huo uliotolewa Juni 14, 2018 na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, ulitakiwa utekelezwe ndani ya muda maalum kuanzia Julai 1, 2018 hadi Juni 30, 2019.

# UNDP yatoa mil. 800/- ujenzi mradi wa maji

**Na Jumbe Ismailly, IKUNGI**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP) limetumia Dola za Marekani 361,778 (Sh. 829,558,942) kugharamia ujenzi wa mradi wa maji na umeme katika Kijiji cha Mtavaira, wilayani Ikungi, mkoani Singida.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema hayo kwenye taarifa yake ya utekelezaji wa mradi wa maji na umeme iliyosomwa kwa niaba yake na Mratibu wa Mradi wa Halmashauri hiyo, Peter Manyerere, kwenye sherehe za uzinduzi wa mradi huo uliofanyika Kijiji cha Mtavira kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Prof. Kitila Mkumbo.

Alisema malengo ya mradi huo ni kuwapatia huduma ya majisafi, salama na umeme unaotokana na nishati jua, kupunguza usumbufu kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji huyo, mradi huo pia utasaidia wakazi wa vijiji hivyo kuepuka magonjwa yanayosababishwa na matumizi ya maji yasiyo salama, vilevile kupunguza gharama za kununua maji na kupata umeme kwa gharama nafuu.

Alizitaja changamoto kubwa zilizoukabili mradi huo kuwa ni pamoja na kukosekana kwa mfumo wa chombo cha kufuatilia taarifa za mauzo kwenye boksi, baadhi ya wananchi kutaka malipo ya fidia wakati wa kutekeleza mradi na kuendelea kutumia maji yasiyo safi na salama.

Changamoto zingine ni upungufu wa umeme hasa wakati wa mvua, hivyo umeme unaotokana na nishati ya jua unapungua na kuathiri utendaji kazi wa mitambo na kukosekana kwa chombo cha usafiri kwa msimamizi wa mradi kama vile gari au pikipiki ili kusaidia kufuatilia kwa karibu mradi huo.

Akitoa taarifa fupi, Meneja wa mradi huo kutoka UNDP, Emmanuel Nnko, alisema shirika hilo liliipatia Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi 'powerbank' 950 ambazo kila moja ina uwezo wa kuhudumia kaya 400.

# MATANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### TAREHE YA MWISHO YA MSAMAHA MAALUM WA KODI KWA MUJIBU WA AGIZO NAMBA, 282A, 2018 YA MSAMAHA WA RIBA NA ADHABU

**Dar es Salaam, 19 Desemba 2019:**
Mamlaka ya Mapato Tanzania (Ijulikanayo kama"TRA" au "Mamlaka") inapenda kuwakumbusha walipakodi wote kwamba mnamo tarehe 14 Juni 2018, Waziri wa Fedha na Mipango alitangaza msamaha maalum wa riba na adhabu chini ya **AGIZO Namba 282A, 2018 ya msamaha wa Riba na Adhabu** kwa walipakodi wenye malimbikizo ya madeni ya kodi na wale ambao kwa hiyari yao waliweka wazi au kuthibitisha malimbikizo ya madeni yao ya Kodi na walikuwa tayari kulipa malimbikizo hayo ya kodi ya msingi katika kipindi na masharti yaliyowekwa na AGIZO hilo.

Msamaha huo wa kodi ulibuniwa ili utekelezwe ndani ya muda maalum ukianzia **tarehe 1 Julai 2018 hadi 30 Juni 2019**. Hata hivyo, kulingana na sababu za msingi, Serikali kupitia **Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu),** (Nyongeza ya muda wa Kulipa), 2019, iliongezea muda wa malipo ya Kodi ya msingi kufikia tarehe 31 Desemba 2019, kwa walipakodi ambao: -

a) Waliomba msamaha wa riba na adhabu za kodi kwa Kamishna Mkuu;
b) Walipatiwa msamaha wa riba na adhabu;
c) Walioingia makubaliano na Kamishna Mkuu ya kusamehewa riba na adhabu za kodi kama ilivyo ainishwa katika **AGIZO Namba 282A, 2018 ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi (msamaha wa Riba na Adhabu).**
d) Walikubali kulipa Kodi ya msingi iliyokadiriwa kwa mkupuo au kwa awamu; na
e) Wale ambao mpaka tarehe **30 Juni 2019,** alishindwa kulipa kwa ukamilifu, kiasi cha kodi ya msingi kilichokubaliwa.

Hivyo, walipakodi wote waliopewa msamaha wa riba na adhabu wanakumbushwa kutumia fursa hii kumalizia madeni yao ya kodi ya msingi kabla ya au **tarehe 31 Desemba 2019** kama ilivyoainishwa katika makubaliano. Izingatiwe kwamba, mlipakodi yoyote ambaye atakuwa amepewa msamaha chini ya **AGIZO namba 282A, 2018 ya Usimamizi wa Kodi (Msamaha wa Riba na Adhabu),** na akashindwa kukidhi au kutekeleza masharti ya mkataba wa makubaliano ya malipo, Kamishna Mkuu atabatilisha mkataba wa makubaliano na kudai kiasi cha kodi ya msingi kilicho salia pamoja na riba, na adhabu kama vile hakukuwa na masamaha uliotolewa.

Aidha kwa taarifa hii ya mwisho, walipakodi wote wanajulishwe kwamba, kuanzia **tarehe 1 Januari 2020,** Kamishna Mkuu atachukua hatua za kukusanya kodi dhidi ya walipakodi wote walioshindwa kuheshimu msamaha uliotolewa na kukusanya kodi stahiki, riba, na adhabu zote BILA taarifa nyingine zaidi ya hii.

**Kwa taarifa hii, tekeleza kama ilivyoelekezwa.**

**"Pamoja Tunajenga Taifa letu"**

**Msafiri Mbibo.**
**KAIMU KAMISHNA MKUU**

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TAARIFA KWA UMMA

### MAWASILIANO YA KIKODI BAINA YA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA NA WAWAKILISHI WA WALIPAKODI

**Dar es Salaam, Desemba 20, 2019**

Mamlaka ya Mapato Tanzania ("TRA" au "Mamlaka") inatambua na kuthamini umuhimu wa mawasiliano, kwa njia ya majadiliano, yanayohusu masuala ya kikodi baina ya Mamlaka yenyewe na walipakodi wetu. Kimsingi, majadiliano haya ni moja ya nguzo za kutusaidia TRA katika kutekeleza kwa ufanisi jukumu letu la kukadiria, kukusanya, na kuhasibu kodi ya Serikali. Pia, kupitia majadiliano haya, walipakodi hupata fursa ya kupata uelewa mkubwa ili kuwasaidia kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati.

Vile vile, tunapenda kuwataarifu walipakodi na wananchi kwa ujumla kuwa, kwa mujibu wa **Kifungu cha 27(1)(a) cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015,** mlipakodi ana haki ya kuwakilishwa na mwakilishi atakayemteua kwa ajili ya majadiliano baina ya TRA na mlipakodi husika. Hata hivyo, kwa kuwa taarifa za mlipakodi ni siri baina ya mlipakodi na TRA (kama ilivyoelekezwa katika **Kifungu cha 21 cha Sheria tajwa),** uwakilishi wowote tofauti na mlipakodi mwenyewe ni sharti uzingatie matakwa ya **Kifungu cha 27(1)(b) cha Sheria** tajwa ambapo ni lazima mlipakodi amtaarifu, kwa maandishi, Kamishna Mkuu wa TRA kuhusu uwakilishi huo. Ikumbukwe kwamba, mtu yeyote ambaye ama si Mmiliki au Mkurugenzi wa kampuni (mlipakodi), hana uhalali wa kumwakilisha mlipakodi iwapo hana Hati ya Uwakilishi (Power of Attorney), kutoka kwa mlipakodi, ambayo itawasilishwa TRA baada ya kufuata taratibu zote za kisheria, ikiwa ni pamoja na kusajiliwa na Msajili wa Hati (Registrar of Documents).

Aidha, wawakilishi Wataalam, kama vile Mawakili (Advocates), wanaweza kuwawakilisha walipakodi kama wateja wao endapo wateuliwa rasmi na wateja hao na uteuzi wao kutaarifiwa kwa Kamishna Mkuu kwa mujibu wa Kifungu cha 27(1)(b) cha Sheria tajwa kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Kwa upande wa wawakilishi ambao ni Wataalam Elekezi wa Kodi **(Tax Consultants),** kama Kifungu cha 28 cha Sheria tajwa kinavyotambua uwepo wao, ni lazima wawe wamesajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Kanuni ya 5 ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi za mwaka 2016.

Kwa upande wa masuala ya forodha yanayosimamiwa na TRA kupitia Idara yake ya Forodha na Ushuru wa Bidhaa, **Kifungu cha 6 cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015** kinampa Kamishna Mkuu mamlaka ya kutumia vifungu vya Sheria hiyo kwenye masuala ya forodha endapo matumizi ya Sheria hiyo hayakinzani na utaratibu uliowekwa na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Hivyo, Mawakala wa Forodha (waliosajiliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 145 na kwa kuzingatia matakwa ya **Kifungu Na. 146, 147 na 148 cha Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004),** Mawakili, na Wawakilishi wowote watatambuliwa rasmi kama wawakilishi wa walipakodi iwapo taarifa za uteuzi wao zitawasilishwa kwa Kamishna wa Forodha. Aidha, tunaomba ieleweke kwamba kitambulisho cha mfanyakazi (Identity Card) au sare ya kazi sio kibali cha uwakilishi halali kwa mujibu wa Sheria.

Hivyo, natoa wito kwa walipakodi na wananchi kuzingatia ufafanuzi huu kwa lengo la kuwa na majadiliano baina ya TRA na walipakodi yanayotambulika kisheria. Tunaomba ieleweke kwamba ushiriki wa watu ambao si wawakilishi halali wa walipakodi, sio tu ni uvunjifu wa matakwa ya **Kifungu cha 21 cha Sheria Na. 10 ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015,** kwa upande mmoja, lakini pia, kwa upande mwingine, husababisha majadiliano mengi yasiyo na tija na ambayo ama huwa hayafikii muafaka au hufikia muafaka usiokubalika kisheria na walipakodi husika wanapopelekewa maamuzi ya kikodi.

**Tunatanguliza shukrani kwa ushirikiano.**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Msafiri Mbibo.**
**KAIMU KAMISHNA MKUU**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada zaidi muhimu kutokomeza malaria

**UGONJWA** wa malaria bado ni tishio kwa watu wengi nchini. Ni ugonjwa ambao umekuwa ukipoteza uhai wa watu wengi mijini na vijijini.

Ni ugonjwa ambao kiwango chake cha maambukizi kimekuwa kikiripotiwa kupanda na kushuka, hivyo wakati mwingine pale inapoelezwa maambukizi kupungua kuwafanya wengi kupuuza kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Kuchukua tahadhari kimsingi ndio njia muhimu na ya pekee katika kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo, ambao unatajwa kuwa umeshaua watu wengi kuliko magonjwa mengine.

Jambo la kutia faraja ni kwamba ripoti ya karibuni imebainisha kwamba maambukizi ya malaria yamepungua nchini. Kwamba kiwango cha maambukizi nchini kimepungua zaidi ya asilimia 50 ndani ya miaka miwili kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia 7.3 kwa mwaka 2017.

Ripoti hiyo mpya ilitolewa wiki iliyopita na Mkurugenzi wa Huduma za Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Leonard Subi, wakati wa kikao kazi cha kanda kilichojumuisha, waganga wakuu wa mikoa, wilaya, wafamasia na waratibu wa malaria kutoka kanda tano za mikoa ya Dodoma, Singida, Njombe, Iringa na Morogoro.

Mkutano huo ulikuwa na lengo la kutathmini utekelezaji wa shughuli za malaria kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP).

Alisema Tanzania imedhamiria kuutokomeza ugonjwa huo, na kwamba mafanikio yameanza kuonekana kwa kipindi cha miaka kumi sasa kwani mwaka 2010 kiwango cha malaria kilikuwa asilimia 18, lakini sasa ni asilimia 7.3.

Mkurugenzi huyo alisema vifo vitokananvyo na malaria navyo vimepungua kwa zaidi ya asilimia 75 kwa zaidi ya miaka kumi, na vile vile watu wanaougua malaria na maambukizi mapya nao wamepungua kwa zaidi ya asilimia 67.

Hata hivyo, alisema Tanzania bado inatajwa kama nchi yenye kiwango kikubwa chenye malaria katika nchi za Afrika mojawapo kati ya nchi kumi, ingawa bado ipo fursa ya kuitokomeza malaria nchini.

Pamoja na taarifa hizo nzuri na zinazoleta faraja na matumaini, Watanzania tusibweteke kwamba maambukizi ya malaria yamepungua, bali jambo la msingi ni kuifanya ajenda ya kuutokomeza ugonjwa huo kuwa ya kudumu.

Kimsingi, inawezekana kabisa kuutokomeza ugonjwa wa malaria kwa sababu hatua za kuchukua ni za kawaida kama kulalia vyandarua, kuharibu mazalia ya mbu na kuweka mazingira ya makazi katika hali ya usafi.

Pia elimu endelevu kuhusiana na malaria iendelee kutolewa na serikali pamoja na wadau ili kujenga uelewa wa wananchi kuhusu ugonjwa wa malaria, maambukizi, hatua za kuepukana nayo pamoja na matibabu.


Tunaamini kuwa ushirikiano wa wadau wote na jitihada za kila mmoja zitasaidia kupunguza kiwango cha maambukizi kama si kuutokomeza kabisa ugonjwa huo hatari.

Tunaipongeza serikali na wadau wengine kwa jitihada zao zilizowezesha kupungua kwa kiwango kwa zaidi ya asilimia 50 ndani ya miaka miwili kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia 7.3 kwa mwaka 2017.

Hizi ni dalili kwamba hatua zaidi zikichukuliwa na kila mmoja kutimiza wajibu wake, bila shaka ukubwa wa tatizo unajulikana, hivyo Watanzania wengi wajikinge ili kuishi bila kuteswa na malaria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

# Tuache utendaji kazi wa mazoea kustawisha taifa

**MOJA** ya kikwazo kinachokwamisha gurudumu la maendeleo ya taifa ni cha watu kufanya kazi kwa mazoea.

Na ndiyo maana kinaendelea kupigwa vita kwa nguvu na serikali ya awamu ya tano, ili kisiwe sehemu ya utamaduni wa Mtanzania.

Kwa miongo sasa, suala la watu kufanya kazi zao kwa mazoea, likijionyesha kwa uwazi upande wa watumishi wa umma, limekuwa ni kama utamaduni wa kawaida.

Wahenga wanasema mazoea hujenga utamaduni na wataalamu mbalimbali wanabainisha wazi kuwa mazoea ni adui mkuu wa ufanisi, iwe katika sekta ya umma au binafsi, iwe kwenye biashara mpya au za zamani.

Kwa nini, kwa sababu katika zama hizi za mabadiliko makubwa ya kimaendeleo, zama za sayansi na teknolojia, zama za utandawazi, kunahitajika nidhamu ya kipekee ya utendaji kazi.

Nidhamu inayoongozwa na sheria, kanuni na taratibu za kitaasisi ili kuweza kufikia maendeleo ya watu na taifa kwa ujumla.

Na kwa kulitambua hilo, baada ya awamu ya tano kuingia madarakani, Rais John Magufuli aliwaonya watumishi wa umma kuachana na utamaduni huo.

Akachukua hatua madhubuti za kuwatumbua wale wote ambao hawakuendana na maelekezo yake ili kuonyesha anamaanisha anachokisema.

Dk. Magufuli akawataka wasaidizi wake kwenye wizara, idara, mashirika na taasisi za umma waongozwe na sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma zinazowataka wawatumikie wananchi kwa mujibu wa miongozo ya ofisi zao.

Hata hivyo, Muungwana anaona kwamba suala la kuchukulia vitu kwa mazoea ni kama imekuwa utamaduni si tu kwa watumishi wa umma, bali hata kwa wananchi wa kawaida.

Na matokeo yake, ndiyo hasara tunazoendelea kuzishuhudia kama nchi karibu kila siku.

Hasara za kupotea kwa maisha ya watu, wengine wakiambulia vilema vya maisha, uharibifu wa mali na hatimaye kuathiri uchumi wa nchi.

Hata hivyo, kinachomshangaza Muungwana ni kwamba bado baadhi yetu tunaendelea na utamaduni huo wa kufanya kazi kwa mazoea na hatusikii la Mwadhini wala Mnadi swala na hivyo kuishia kusababisha majanga makubwa.

Na hiyo ni pamoja na maelekezo, maonyo na tahadhari zinazotolewa na viongozi wa serikali, wa dini, wa kimila na taasisi mbalimbali, yanayobainisha madhara ya kufanya kazi kwa mazoea.

Kwa mfano tafiti mbalimbali zilizofanywa nchini, zinaonyesha asilimia 75 ya ajali za barabarani zinazotokana na makosa ya kibinadamu, huku asilimia 50 ya makosa hayo yanahusiana na mambo ya kibinadamu yanayofanywa na madereva.

Lakini mpaka sasa bado unakuta dereva wa Kitanzania anaendesha gari huku akiongea na simu, akichati au akizungumza na mtu wa pembeni.

Bado unakuta dereva wa Kitanzania akipita kwenye taa ambazo hazimruhusu, hasimami kwenye alama za pundamilia ama akipita gari la mbele bila ya kuchukua tahadhari na matokeo yake ni ajali.

Ukimuuliza ana majibu yasiyo na mashiko, kwamba hajaanza leo kuendesha gari akiongea na simu au akichati.

Tunaambiwa kwa mfano tuachane na mazoea ya kuchoma moto misitu au kukata miti ovyo, kwani yanagharama kwa maisha yetu, hatusikii.

Takwimu za uhifadhi wa mazingira zinaonyesha kuwa Tanzania hupoteza takribani hekta 400,000 za misitu kila mwaka kutokana na miti kukatwa kwa sababu ya mazoea.

Matokeo yake ni mabadiliko ya tabianchi ambayo ndiyo chanzo cha mafuriko na ukame tunaoushuhudia katika baadhi ya maeneo nchini.

Tunaambiwa na wataalamu wa afya tuweke mazingira yetu katika hali ya usafi ili kuepukana na magonjwa kama ya kuharisha na kipindupindu.

Hata hivyo, kutokana na mazoea ndio haohao tunaofungulia maji ya chooni na kuyaelekeza kwenye mitaro ya maji na hatimaye magonjwa ya kuambukiza.

Ni wakati sasa kwa Watanzania wa kuachana na utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea, ili kuliepusha taifa na majanga ambayo kimsingi yanaepukika.

# Kanuni zarekebishwa udhibiti taka hatarishi

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, amewataka wananchi na wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara ya taka hatarishi hususani chuma chakavu kuzingatia misingi iliyoainishwa katika kanuni mpya zilizopitishwa mwaka 2019 za udhibiti na usimamizi wa taka hizo.

Waziri Simbachawene aliyasema hayo katika mkutano na wanahabari jijini Dodoma kuhusu kanuni mpya za mwaka 2019 za udhibiti na usimamzi wa taka hatarishi na kanuni za ada na tozo za usimamizi wa mazingira.

"Ili kuzuia na kudhibiti athari zitokanazo na taka zenye madhara, mfumo mahsusi unaofanya kazi kwa ufanisi wa kudhibiti taka hizi unapaswa ufuatwe kama ulivyobainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004," alisema Simbachawene.

Alizitaja kanuni zilizofanyiwa mapitio na marekebisho ikiwa ni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi za Mwaka 2009, Kanuni za Ada na Tozo za Usimamizi wa Mazingira za Mwaka 2008 na marekebisho yake ya mwaka 2016 na 2018, pamoja na Kuandaa Kanuni mpya za Udhibiti na Usimamizi wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2019.

"Kanuni mpya za mwaka 2019 imempa mamlaka waziri mwenye dhamana ya mazingira tu akishauriwa na Mkurugenzi wa Mazingira kutoa vibali vya kuingiza, kusafirisha nje ya nchi, kusafirisha ndani ya nchi au kupitisha taka hatarishi nchini," alisema Simbachawene.

Alisema kanuni hizi zitasaidia kulinda mazingira yasiathiriwe na taka hatarishi na pia kulinda miundombinu iliyopo nchini isiharibiwe kutokana na biashara ya taka hatari hususani chuma chakavu.

"Kanuni mpya za mwaka 2019 zimeandaliwa kwa kuzingatia makundi ya aina za taka hatarishi kulingana na mkataba wa Basel unaohusu udhibiti wa usafirishaji na utupaji wa taka hatarishi baina ya nchi na nchi ambapo Tanzania ni nchi mwanachama wa mkataba huo," alisema. Alisema shehena yoyote ya taka hatarishi itakayoingizwa au kupitishwa nchini bila kufuata masharti ya kanuni hizi, itachukuliwa kuwa ni usafirishaji haramu wa taka hatarishi na zinapaswa kurejeshwa katika nchi zilikotoka kwa gharama za msafirishaji.

Aliongezea kuwa kanuni mpya za mwaka 2019 imeeleza uwapo wa masharti ya mmiliki wa kibali cha kusafirisha taka hatarishi, hivyo kutarahisisha ufuatiliaji wa uzingatiaji wa masharti yaliyoainishwa katika kibali cha usimamizi wa taka hatarishi pamoja na masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa ujumla wake. "Kanuni hii itasaidia kufanya ufuatiliaji wa karibu wa mzigo kutoka sehemu ulipopatikana mpaka anapokwenda lengo likiwa kulinda miundombinu iliyojengwa kwa gharama kubwa na serikali isiharibiwe kutokana na biashara hizi," alisema Simbachawene.

Aidha, Simbachawene alieleza kanuni mpya inayoipa mamlaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kushughulikia maombi ya vibali kupitia kanda zake saba zilizopo nchini kupokea maombi na kuyafanyia kazi mwisho kupeleka mapendekezo kwa Waziri kupitia Mkurugenzi wa Mazingira kwa ajili ya idhini na kutoa kibali.

Kanuni mpya zimeweka adhabu kali zaidi kwa makosa ya kutokuwa na kibali cha kusimamia taka hatarishi nchini. Adhabu hizo ni faini kuanzia shilingi milioni tano hadi bilioni kumi au kifungo kisichozidi miaka kumi na mbili au vyote kwa pamoja lengo likiwa kulinda mazingira.

# Makosa ya jinai yapungua Pwani

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, amesema hali ya usalama wa raia na mali zao imeimarika mkoani humo mwaka huu kutokana na kupungua kwa makosa ya jinai.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu mafanikio ya jeshi hilo kwa mwaka 2019.

Alibainisha kuwa matukio yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi kwa mwaka huu ni 2,074 kulinganishwa na matukio 2,318 yaliyoripotiwa katika vituo hivyo mwaka jana.

"Kutokana na takwimu hizo, tumepunguza makosa 244 ya jinai, sawa na asilimia 10.5, makosa ya jinai dhidi ya binadamu kama mauaji, kubaka na kulawiti kwa mwaka jana yalikuwa 382, na mwaka huu yameripotiwa makosa 366, hivyo yamepungua 16, sawa na asilimia 12.

Kamanda Wankyo aliwataka wananchi washerehekea sikukuu za mwishoni mwa mwaka kwa amani na utulivu na amani, akisisitiza ulinzi umeimarishwa.

"Wito wangu kwa wamiliki wa kumbi za starehe, zisijaze watu kupita kiasi kwa matamanio ya kuongeza kipato, ni marufuku kwa mtu yeyote au taasisi kufyatua fataki siku za sikukuu," alionya.

Pia, aliwataka madereva wa vyombo vya moto kutojaza abiria kupita kiasi, kutoendesha vyombo hivyo wakiwa wamelewa na wahakikishe wanatii sheria za barabarani.

**"Kutokana na takwimu hizo, tumepunguza makosa 244 ya jinai, sawa na asilimia 10.5, makosa ya jinai dhidi ya binadamu kama mauaji, kubaka na kulawiti kwa mwaka jana yalikuwa 382, na mwaka huu yameripotiwa makosa 366, hivyo yamepungua 16, sawa na asilimia 12.**




# Usafiri mabasi bado shida Ubungo

**Na Maulid Mmbaga**

MAMIA ya abiria bado wamekwama katika Stendi Kuu ya Mabasi Ubungo jijini Dar es Salaam kutokana na uhaba wa mabasi yanayowasafirisha abiria kwenda mikoani.

Akizungumza na Nipashe jana kwenye stendi hiyo, Meneja wa stendi hiyo, Mkama Chirosa, alikiri kuendelea kuwapo kwa tatizo hilo kipindi hiki cha mwishoni mwa mwaka.

Alisema wanashirikiana na Chama cha Wamiliki wa Mabasi (Taboa) katika kuhakikisha wanalitatua.

"Napenda kuwashauri wamiliki wa mabasi kuongeza magari kwa kipindi hiki cha sikukuu, pia wakumbuke kuyafanyia ukarabati kabla hawajaanza safari ili kuepusha usumbufu kwa abiria," alishauri.

Alisema kwa kipindi hiki, wameongeza mabasi kutoka 350 hadi 400 yanayotumia stendi hiyo, lakini bado abiria wanakosa usafiri, hivyo wanashirikiana na mamlaka zingine za nchi kuongeza magari kwa kuruhusu mabasi madogo kubeba abiria.

"Tunaipongeza serikali kwa kuongeza usafiri wa treni kwa baadhi ya mikoa ya kaskazini, kwa kiasi fulani imesaidia kupunguza msongamano wa abiria kituoni hapa," alisema.

Linda Haule, mmoja wa abiria waliokwama katika stendi hiyo jana, alisema aliwasili alifajiri lakini hadi inasifika saa saba mchana, hakufanikiwa kupata basi la kumpeleka Moshi, Kilimanjaro.

"Magari mengi hayafiki kituoni kwa wakati hali inayopelekea kuwapo kwa msongamano mkubwa wa abiria, jua, vumbi vyote vinatuishia, hapa hakuna sehemu maalum ya kujihifadhi wakati tukisubiria usafiri," alisema.



Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, akiongea na wajumbe wa Bodi ya Shirika la Reli (TRC), jijini Dar es Salaam jana. PICHA: MIRAJI MSALA


KDF Kilimanjaro Development Forum
Today, Tomorrow, Together

P.O Box 32055,
Dar es Salaam, Tanzania
+255 688 591 182
john@stageneraltz.com
www. kilimanjarodevforum.co.tz

**MABADILIKO YA UONGOZI WA KDF**

KDF ni asasi isiyokuwa ya kiserikali yenye lengo la kushirikiana na Serikali na wadau wengine ili kuchangia katika ustawi wa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na hivyo kuchangia maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mkutano Mkuu wa Kilimanjaro Development Forum (KDF) uliofanyika tarege 21 desemba, 2019, Mjini Moshi umeteua Bodi Mpya baada ya bodi iliyopita kukamilisha kipindi chake.

Hivyo KDF inachukua fursa hii kuitambulisha bodi mpya kwa wanachama, marafiki, wadau na umma kwa ujumla. Kama ifuatavyo:

1. Balozi Abubakar Ibrahim – Mwenyekiti;
2. Bw. Mahamoud Mringo – Makamu Mwenyekiti;
3. Bw. Daudi Nasib – Katibu Mkuu;
4. Adv. Zaharani Sinare – Naibu Katibu Mkuu;
5. Bw. Leonard Kisarika – Mweka Hazina;
6. Bi. Nancy W. Malekia – Naibu Mweka Hazina;
7. Adv. Saidi Mwema – Mjumbe;
8. Bw. Rashid Tenga - Mjumbe;
9. Balozi Radhia Msuya – Mjumbe;
10. Bw. Peter Marealle - Mjumbe, na
11. Bw. Danny Mruttu – Mjumbe.

Mwenyekiti wa Bodi Mpya ya KDF, Balozi Abubakar Ibrahim anatoa shukrani zake za dhati kwa Mheshimiwa Cleopa D. Msuya na wajumbe wenzake wa bodi iliyopita kwa uongozi mahiri na moyo wa kujitolea. Aidha anawashukuru wanachama wa KDF kwa kumuamini yeye na wajumbe wenzake na kuwaomba ushirikiano wao na marafiki wote wa Kilimanjaro ili kuchangia katika kuinua hadhi na maisha ya wananchi wa Kilimanjaro na Tanzania kwa ujumla


# Kamwelwe asubiri siku 8 kuzima simu

INATOKA UK 2

nye namba za vitambulisho, wanatarajiwa kusajili laini milioni 5.6 kwa sababu mtu mmoja anamiliki zaidi ya laini moja.

Aidha, laini zilikuwa zimesajiliwa hadi Desemba 10, mwaka huu, zilikuwa 47,063,603, ambazo zinamilikiwa na watu milioni 21.1. Idadi ya laini zilizosajiliwa kwa alama za vidole zilikuwa 19,681,06 sawa na asilimia 42 zinazomiliwa na watu Sh. milioni 7.6.

Mei Mosi, mwaka huu, TCRA ilianza rasmi usajili wa alama za vidole kwa kushirikiana na kampuni za simu za mikononi na kazi hiyo itafungwa Desemba 31, saa 6:00 usiku na mtumiaji wa simu ambaye hatajisajili laini yake itakuwa imefungwa rasmi.

Kuhusu utiaji saini huo, Kamwelwe alisema umoja huo ambao unashirikisha nchi 45 za Afrika umekubaliana kujenga jengo hilo jijini Arusha na kutokana na umuhimu wake, serikali imetoa msamaha wa kodi kwa vifaa vyote vitakavyotumika kwa ajili ya ujenzi.

"Mradi huu wa gharama ya Sh. bilioni 33.5 ni mradi wenye hadhi kubwa kwa taifa na kimataifa. Serikali itasimamia ili kuhakikisha ujenzi huu unakuwa na ubora na ufanisi mkubwa. Pamoja na mkandarasi kupewa miezi 30 kukamilisha ujenzi, mradi huu unapaswa ukamilike chini ya kipindi cha miaka miwili (miezi 24)," alisema Kamwelwe. Alisema mradi huo ulishindwa kutekelezeka kwa kipindi cha miaka 40 baada ya kuwapo kwa ukwamishaji kutoka kwa baadhi ya nchi wanachama.

Kwa mujibu wa Kamwelwe, uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kufanyika Januari 17, mwakani katika maadhimisho ya miaka 40 ya PAPU yatakayofanyika Arusha.

# Watetezi haki wahadharisha wajibu Polisi

INATOKA UK 2

kusimama kwa pamoja kukemea matukio hayo ili kwa pamoja kukemea yanayoendelea.

Kadhalika walisema wananchi wanapaswa kusimama na kupinga ukiukwaji unaoendelea kufanywa na vyombo vya usalama dhidi ya watuhumiwa nchini.

Walitaka pia Tanzania kuhuisha mchakato wa Katiba ili kuweka chombo huru kitakachosimamia utendaji na uwajibikaji wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama kwa lengo la kulinda haki za wananchi wakiwa mikononi mwa polisi.

"Tunaendelea pia kusihi vyombo vingine vya utoaji haki hasa mahakama, kujitahidi sana kipindi hiki kujiweka huru zaidi, kufanya kazi kwa weledi, kulinda haki za wanyonge na kufanya kazi kwa misingi ya kikatiba, kisheria na haki za binadamu."

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, kimbilio pekee kwa mujibu wa Katiba haki zinapokiukwa ni Mahakama Kuu na Tume ya Haki za Binadamu kutambua takwa hilo la kikatiba na kulitenda kivitendo.

"Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, nayo tunaikumbusha jukumu lake kikatiba la kulinda na kukemea ukiukwaji wa haki za raia. Kupitia tamko hili tunaleta malalamiko rasmi kwenu kuhusu haki za watuhumiwa hapa nchini," ilisema taarifa hiyo.

Watetezi hao walisema vyombo vya usalama viheshimu uhuru wa raia na watetezi wa haki za binadamu kutoa maoni yao kuhusu mambo mbalimbali ya kitaifa na yenye maslahi kwa taifa.

Magoti alikamatwa Desemba 20, mwaka huu, katika eneo la kituo cha mafuta cha Puma, Mwenge jijini Dar es Salaam na watu wanaodaiwa kuwa watano waliokuwa wamevalia kiraia na kumwingiza kwenye gari aina ya Harrier na kwenda naye kusikojulikana.

**"Tunaendelea pia kusihi vyombo vingine vya utoaji haki hasa mahakama, kujitahidi sana kipindi hiki kujiweka huru zaidi, kufanya kazi kwa weledi, kulinda haki za wanyonge na kufanya kazi kwa misingi ya kikatiba, kisheria na haki za binadamu."**

HABARI KITAIFA

# Bosi Magereza asisitiza nidhamu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA Jenerali wa Magereza nchini, Phaustine Kasike, amewataka maofisa na askari wote wa jeshi hilo kuendelea kutimiza majukumu yao kwa kuzingatia nidhamu ya kazi na kufuata taratibu zilizopo ndani ya jeshi.

Amesema hayo katika kikao kazi na maofisa na askari wa vituo vya Magereza Mkoa wa Dar es Salaam, ambapo walijadili masuala mbalimbali ikiwamo utendaji kazi, maadili ya kazi, nidhamu na utekelezaji wa mikakati ya jeshi hilo ikiwamo mpango mkakati wa kilimo, uwekezaji katika viwanda na ufugaji.

Kamishna Jenerali Kasike alisisitiza kuwa nidhamu ni muhimu jeshini, na hakuna mtu aliye juu ya nidhamu kwani msingi wa jeshi lolote lile ni nidhamu.

"Taswira ya Jeshi la Magereza inategemea zaidi utekelezaji mzuri wa majukumu yenu kwa kuzingatia nidhamu na maadili ya kazi. "Kila mmoja lazima atimize wajibu wake kikamilifu kwa kutumia uweledi, ubunifu na kuzingatia nidhamu ya kazi," alisisitiza Kamishna Jenerali Kasike.

Alisema wapo baadhi ya maofisa na askari ambao wana matatizo ya kinidhamu na hawataki kubadilika, hali ambayo alisema inaharibu taswira ya jeshi hilo katika jamii.

Aidha, alikemea tabia ya kutokufuata taratibu za uwasilishaji wa malalamiko kupitia utaratibu uliopo ndani ya jeshi hilo kwa baadhi ya maofisa na askari kwani tabia hiyo inachangia sana katika kushuka kwa nidhamu ndani ya jeshi.

"Jeshi ambalo halina nidhamu ni sawa na genge la wahuni ambao wamevaa sare za jeshi. Hivyo natoa wito kwa maofisa na askari wenye matatizo ya kinidhamu wajisahihishe na kujirekebisha ili kuendana na misingi ya jeshi," aliongeza Jenerali Kasike.

Pia alisema atahakikisha Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza (SHIMA) linajizatiti zaidi katika miradi yake ili kujiimarisha katika kufanya shughuli za kibiashara hapa nchini.

Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza, Julius Ntambala, alimhakikishia Kasike kuwa atahakikisha maofisa na askari katika mkoa wake wanaendelea kutekeleza majukumu yao ya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo katika uendeshaji wa jeshi hilo.

# Baba afungwa miaka 60 kunajisi mtoto

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Mkoa wa Lindi, imemuhukumu mkazi wa Mtaa wa Kariakoo katika Halmashauri ya Manispaa hiyo, M'baraka Masudi Kampunda (62) kifungo cha miaka 60 jela, baada ya kukutwa na makosa mawili likiwamo la kunajisi mtoto.

Mtoto aliyefanyiwa kitendo hicho cha kikatili mwenye umri wa miaka 11 jina lake limehifadhiwa.

Licha ya adhabu ya kifungo, pia Mahakama imemtaka Kwampunda kumlipia mlalamikaji fidia ya Sh. 600,000.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Muyonga Magala, baada ya kuridhishwa na ushahidi usio na shaka kutoka upande wa mashtaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, mshtakiwa aliulizwa kama anazo sababu zitakazoishawishi mahakama isimpatie adhabu kali kutokana na makosa yanayomkabiri mbele yake, ambapo alijitetea kwa kuiomba imemwonee huruma kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza.

Pia, mfungwa huyo alidai anayo familia inayomtegemea akiwamo mke, watoto, wajukuu na alifanya kosa hilo kutokana na kutingwa na ibilisi wa mapenzi.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Magala alimuuliza Mwanasheria wa Serikali iwapo anazo kumbukumbu za makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hana, lakini aliiomba Mahakama kumpa adhabu kali ili iwe fundisho kwa mshtakiwa na wengine wenye tabia ya aina hiyo.

Hakimu Magala akitoa huku katika kesi hiyo namba 27/2019, kupitia vifungu vya Sheria 130 (1) (2) (c) na 131 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2002, akisema amesikia maombi ya pande zote, lakini kutokana na sheria kumfunga mikono analazimika kumpa adhabu ya kifungo cha miaka 30 kwa kosa la kubaka na miaka 30 mingine kwa kosa la kumwingilia kinyume cha maumbile.

Aidha, Mahakama hiyo imempa adhabu nyingine ya kumlipa kuathirika fidia ya Sh. 600,000.

Hata hivyo alisema kwa kuwa adhabu zinaenda kwa pamoja, Kampunda atatumikia kifungo cha miaka 30 gerezani.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, ilidai kuwa siku na tarehe isiyofahamika, Januari mwaka huu, mshtakiwa akiwa anatambua kitendo anachokifanya ni kosa katika mitaa ya Kariakoo Manispaa ya Lindi, mshtakiwa alimbaka mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 11.

Aidha, alidai mshtakiwa kumwingilia mlalamikaji kinyume cha maumbile, hali iliyomsababishia maumivu makali na michubuko sehemu zake za siri.



Mwananchi akipita juu ya taka zilizorundikana kando ya barabara bila ya kuzolewa na pia kujaa maji yaliyotokana na mvua katika Mtaa wa Dunga Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wakulima wa shayiri walilia soko

**Na Renatha Msungu, KARATU**

WAKULIMA wa shayiri Kata ya Mbulumbulu wilayani Karatu mkoani Arusha, wameiomba serikali iwasaidie kupata mnunuzi wa tani 432 za zao hilo zilizokosa soko.

Kwa mujibu wa mkulima wa Kijiji cha Slahhamo, Paul Peter, wanamwomba Rais John Magufuli, kuwanusuru na janga hilo kama alivyowasaidia wenzao wa korosho ili kuepuka kuathirika kiuchumi.

Alisema tani 432 zilizopo ni nyingi, na kuiomba serikali kuwasaidia ili inunuliwe na kuwawezesha kujikimu kiuchumi pamoja na familia zao.

Mkulima Maria Sule alisema shayiri ni zao muhimu kwa wakazi wa kijiji hicho kwani ni kitega uchumi cha kuendesha maisha yao ya kila siku.

"Tunaomba serikali itusaidie kutafuta wanunuzi ni muda mrefu sasa tokea tumevuna halijapata soko," alisema Bura.

Peter alisema tangu wamevuna zao hilo limekaa ghalani muda mrefu bila kupata mnunuzi jambo linalowapa hofu kwani linaharibika.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Shayiri, Emmanuel Bura, alisema changamoto ya ukosefu wa mnunuzi wa zao hilo haijawahi kutokea, hivyo inawapa wasiwasi kutokana na kuharibika.

Alisema safari hii ukosefu wa soko umekuwa tofauti kutokana na wakulima wengi kupata mazao mengi ikilinganishwa na miaka iliyopita. Alisema serikali inapaswa kuliangalia suala hilo kwa karibu zaidi ili kuwanusuru wakulima wa kijiji hicho.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mbulumbulu, Elikana Sulumbu, alisema amekuwa akipokea changamoto mara kwa mara na kuongeza kuwa endapo hatua za haraka hazitochukuliwa, uwezekano wa kupata hasara ni mkubwa.

## Wapiga jeki elimu, afya kwa bil. 1.6/-

**Na Renatha Msungu, BABATI**

WAKAZI wa Kata ya Ayalagaya iliyopo wilayani Babati Mkoa wa Manyara, wamenufaika na mradi wa kuboresha miundombinu ya elimu na afya uliogharimu zaidi ya Sh. bilioni 1.8.

Uboreshaji huo umefanywa na wahisani wa Karimu International Foundation waliochangia Sh. bilioni 1.8 kuinua elimu na afya kwa kuweka miundombinu bora shuleni.

Meneja wa Mkoa wa Mradi wa Karimu International Foundation, Shau Erro, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Babati wakati wa ziara ya kutembelea miradi mbalimbali wilayani humo.

Erro alisema wamejikita kuisaidia serikali ya awamu ya tano kuboresha elimu na afya kwa vile serikali imetoa kipaumbele kwa sekta ya elimu na afya hivyo wanaiongezea nguvu.

Alisema miundombinu iliyojengwa ni vyoo vya kisasa vyenye sehemu ya kujisitiri kwa wasichana wakati wa siku za kila mwezi.

Erro alisema lengo la kutoa fedha hizo ni kuboresha miundombinu ya elimu pamoja na afya ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuwekeza kwenye sekta hiyo.

Diwani wa kata ya hiyo Sabini Sarme, alisema miundombinu ya ujenzi wa shule hiyo umesaidia wanafunzi wa kata hiyo kupata huduma ya elimu na kiafya kuwa bora zaidi tofauti na ilivyokuwa awali.

Akitolea mfano wa vyoo vilivyojengwa katika Sekondari ya Ayagalaya alisema ni msaada mkubwa kwa watoto wa kike ambao awali walikuwa hawana sehemu ya kujistiri.

Mwanafunzi wa kidato cha tatu Sekondari ya Ayalagaya, alishukuru Karimu Foundation kwa kuwajengea vyoo hivyo ambavyo vimesaidia kuongeza mahudhurio.

# Kazi zisizo na staha mwiba kwa kinamama

**Na Gaudensia Mnguni**

SOKO huria la kazi limetajwa kusababisha maelfu ya vijana kufanya kazi zisizo na staha zinazotishia ustawi wa taifa na kuwaumiza zaidi wanawake na watoto.

Kazi zisizo na staha ni zile zisizoheshimu haki za watumishi kama kupata mshahara wa kujikimu, hazina mikataba, zinawanyima stahili kama likizo ya mwaka, ya uzazi yenye malipo na pia hazijali kuwaunganisha watumishi na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Hoja hizo ziliibuliwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam kwenye mkutano wa vijana, viongozi wa serikali wa idara za ajira, wabunge, asasi za kirai na wadau mbalimbali waliojadili umuhimu wa taifa kuwa na mpango wa ajira zenye staha, uelewano baina ya waajiri na zenye kuheshimu utu wa mfanyakazi.

Ripoti ya vijana wanawake kutoka Zanzibar na Kilwa zikiwasilishwa kwenye mkutano huo, zilitaja changamoto kubwa ya ajira kuwa hazina mikataba ya kisheria, watumishi huajiriwa kwa mdomo.

Hali hiyo, huwatumikisha kama vibarua kwa miaka mingi kwa malipo madogo, lakini wanakosa likizo ya mwaka, ya uzazi na wanawake wanapokuwa wajawazito hujiweka kwenye hatari ya kufukuzwa.

Aidha, kinamama hawana haki ya kunyonyesha watoto kwani hunyimwa likizo ya uzazi na pia hawana haki ya kurudi nyumbani kunyonyesha kwani kama vibarua hawana haki hiyo, hali hiyo hudumza watoto.

Wizara ya Afya inaelekeza kuwa mtoto anyonyeshwe kwa miezi sita mfululizo bila kula chochote lakini wanawake wengi wanaofanyakazi zama hizi hawalitimizi hilo.

Pamoja na changamoto hizo wanawake wameendelea kunyanyaswa kingono na viongozi wasio na maadili wanaowatumia kingono kwa kutumia vibaya madaraka, ofisi wakiwapa ahadi za kuwapa ajira za kudumu, upendeleo na malipo bora.

Vijana wanaume walitoa mfano wa jinsi ajira za bodaboda zilivyokosa staha mfano ukiumwa mmiliki anavunja mkataba, anaweza hata 'kukuibia' pikipiki akiamua, wengine ukichelewesha fedha hata siku moja anavunja mkataba, pia hawawapi vifaa vya kazi kama kofia, viatu na miwani.

Katika mkutano huo, ulioandaliwa na Shirika la ActionAid, Ofisa Mradi Jovina Nawenzake, alisema kuongezeka kwa soko huria kunaziweka mashaka ajira zenye staha.

Alisema watumishi wa serikalini wako salama zaidi lakini wa sekta isiyo rasmi wana hali ngumu, aliishauri serikali kutupia jicho kwenye sekta isiyo rasmi ambako ndiko kwenye kazi zisizo na staha.

Aliwataka wadau wote kuwa na mpango na kushirikiana kuandaa mpango wa kazi salama na zenye staha kwa wote sekta ya umma na binafsi.

Maelezo ya serikali kutoka Wizara ya Kazi, Ajira na Vijana yaliyotolewa kwenye mkutano huo, yalieleza kuwa kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) inaandaa mpango wa taifa wa kazi zenye staha, utakaoondoa kero hizo.



Mwalimu mwanzilishi wa Shule ya Msingi Mwiringo Kata ya Busambara, Musoma Vijijini mkoani Mara, Mchungaji Daniel Manyonyi, akizungumza kwenye jubilee ya miaka 50 ya shule hiyo, juzi, akienda sambamba na kuweka mikakati ya kuboresha miundombinu ya shule hiyo kongwe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TEA yawapa mafunzo vijana kwa mil. 136/-

**Na Mwandishi Wetu, MOROGORO**

MAMLAKA ya Elimu Tanzania (TEA) kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) imetoa Sh. milioni 136 kuwezesha mafunzo ya ujuzi wa kuendesha na kutengeneza zana za kisasa za kilimo ikiwamo matrekta na pawatila.

Mafunzo hayo yamesimamiwa na kuratibiwa na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kwa kushirikiana na kampuni ya Agricom Africa, lengo likiwa kuwajengea vijana uwezo ili kujiajiri katika sekta ya kilimo ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa viwanda.

Akizungumza wakati wa hafla ya kuhitimisha mafunzo hayo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki mjini hapa, Mkurugenzi wa Miradi wa TEA, Waziri Salum, alieleza kufurahishwa na mafunzo hayo kwa kuwa fedha zilizotolewa zimekidhi kiwango cha huduma iliyotolewa.

"Mafunzo haya yamegharimu takribani Sh. milioni 136 ambazo zimetolewa kwa ushirika wa serikali na Benki ya Dunia, tunashukuru kuona imeleta matokea mazuri ambayo hatukuyatarajia," alisema Salum.

Salum aliwapongeza TPSF na Agricom kwa kusimamia na kuendesha mafunzo hayo ya wiki sita yaliyojumuisha vijana 135 kutoka sehemu mbalimbali ya nchi.

"Tumekuwa na ukaribu mkubwa na wenzetu wa (TPSF) ambao wamekuwa wakituunganisha na taasisi binafsi kama hii ya Agricom Africa katika kuendeleza teknolojia hususani katika sekta ya kilimo ili kuchochea ukuaji wa sekta hii muhimu kwa uchumi wa kati na ujenzi wa viwanda," alieleza.

Salum alisema wataendelea kutoa mafunzo kama haya kwa sekta sita ambazo zimepewa kipaumbele na TEA ambazo ni kilimo, utalii, usafirishaji, nishati, ujenzi na Tehama ili kutimiza kwa haraka azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

"Muungano wetu na TPSF ni wa kuisukuma nchi yetu kutimiza dira ya serikali ya ujenzi wa viwanda na uchumi wa kati ifikapo 2025, hivyo taasisi yoyote ambayo itapendekezwa kwetu na TPSF na tukajiridhisha nayo hatutasita kutoa pesa ili kutanua wigo wa vijana kupata ajira na kuongeza pato la Taifa," aliongeza Salum.

Aidha, alitumia nafasi hiyo kutoa wito kwa vijana kutumia mafunzo hayo kujiinua kiuchumi kwani kwa sasa sekta ya kilimo inakua kwa kasi na kutengeneza ajira nyingi kwa vijana.

Mratibu wa SDF, Masozi Nyirenda, alisema kazi ya mfuko huo ni kutoa ruzuku kwa vijana na kinamama ili kupata mafunzo ambayo yatachochea upatikanaji wa ajira.

Wizara ya Elimu iliingia makubaliano na TPSF ili kukuza ujuzi katika sekta mbalimbali na kwa kilichofanyika kupitia Agricom ni sehemu ya utekelezaji wa makubaliano kati ya sekta binafsi na TEA.

# Shirika lajitolea kukarabati shule 15

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la ECLAT Foundation la wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, limeanzisha mpango wa kujenga na kukarabati shule 15 wilayani humo.

Mwenyekiti wa ECLAT Foundation, Peter Toima, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumzia mpango mikakati wa maendeleo kwa kipindi cha mwaka mpya wa 2020.

Toima alisema, shirika hilo, limejipanga kujenga na kukarabati shule 15 za msingi za wilaya ya Simanjiro kwenye kata tofauti.

Alisema kwa sasa wapo kwenye ziara ya kuzungukia baadhi ya shule hizo, ikiwamo ya msingi ya Nakweni, Kata ya Shambarai na Shule ya Emishiye ya Kata ya Naisinyai.

"Mimi ni mzaliwa wa kijiji cha Emboreet wilayani Simanjiro na chochote nitakachokipata nitaleta Simanjiro kwa kuwa siwezi kusahau nyumbani na mwaka ujao tumepanga kukarabati shule 15 kwenye wilaya yetu," alisema Toima.

Alisema kupitia ufadhili wa Shirika la Upendo la Ujerumani wameaminiwa kwa kusimamia maendeleo kwa kuwa walitumia Sh. bilioni saba.

"Lengo letu ni kulipa fadhila kwa jamii yetu inayotuzunguka kwa kuwa tangu tulipofahamiana na Shirika la Upendo wameona kazi zinazofanyika hivyo wanaendelea na ufadhili wao kupitia ECLAT Foundation," alisema Toima.

Katibu wa Chama cha Walimu nchini (CWT), wilayani Simanjiro, Nazama Tarimo, aliwapongeza wadau wa shirika hilo, kwa uzalendo wao na kuwaomba wadau wengine waunge mkono.

Tarimo alisema kutokana na jiografia ya wilaya hiyo, kufanya kazi kunahitaji uzalendo kutokana na umbali wa kata moja hadi nyingine na wanatumia muda mwingi kusafiri.

"Watumishi wa idara zote za Wilaya ya Simanjiro ni wazalendo kwa kuwa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, tunaomba muwatie moyo na kuwapongeza kwa kuishi eneo hili," alisema.

Mwenyekiti wa mamlaka ya mji mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alisema wataendelea kuliunga mkono shirika hilo, kwa kuwa ni wadau wazuri wa maendeleo.

"Kwa muda mfupi tumeona matunda ya shirika hili, kwa eneo la Mirerani wametoa matofali 4,000 kwa Shule ya Sekondari Tanzanite, mabati 50 kwa Sekondari ya Mirerani B.W Mkapa na mifuko 100, ya saruji kwa Shule ya Sekondari Tanzanite," alisema.



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas, akisalimiana na wakufunzi wa askari wa Kikosi Maalum kitakachosimamia ulinzi wa amani katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji eneo la Mto Ruvuma, mkoani Mtwara. Matukio ya mauaji yamekuwa yakitokea eneo hilo dhidi ya Watanzania, yaliosababishwa na wahalifu kutoka Msumbiji. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# Wafariki dunia kwa kula mihogo ya sumu

**Na Allan Isack, MANYARA**

WATOTO wawili wa familia moja wamefariki dunia na wengine watatu wamenusurika baada ya kula mihogo mibichi yenye sumu kwenye kitongoji cha Endorbo Kijiji cha Endaghay, Kata ya Gidas wilayani Babati, mkoani Manyara.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), Paul Kasabago, alithibitisha juzi kutokea kwa vifo hivyo.

Kamanda Kasabago aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Mwanahamisi Hamad (4) na Bashiru Hamad (6), wote wakazi wa Kata ya Gidas.

Alisema chanzo cha vifo hivyo ni kula mihogo yenye sumu.

Aliwataja walionusurika kifo kwenye tukio hilo kuwa ni Paulina Bura (19), Selina Safari (41) na Christina Joseph (28).

Alisema na Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo, na watu watatu walionusurika kwenye tukio hilo, wamesha," ruhusiwa kurudi nyumbani baada ya kupata matibabu kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara.

Mama wa watoto hao, Stella Joseph, alisema watoto hao, walifariki baada ya kula mihogo mibichi na maganda yake pamoja na kisamvu.

"Baada ya kula chakula hicho watoto walizidiwa ghafla na kuanza kutapika, na tuligundua mapema kuwa walikula mihogo mibichi ikiwa na maganda yake," alisema.

Aliaomba wananchi wamsaidie kujikimu kimaisha kwa kuwa bado yupo hospitali akimuuguza mtoto wake mdogo Isaka Hamad mwenye umri wa miezi miwili anayesumbuliwa na tatizo la utapiamlo.

"Ninaomba msaada nina mahitaji mengi na sina hata chakula na pia sina mtu atakayenisaidia na atakayeguswa anaweza kuwasiliana na mimi kwa simu namba 0684 353059," alisema.

Alisema alishatengana na mume wake aliyezaa naye watoto hao, hivyo hana msaada wowote anaomba jamii, mashirika, taasisi binafsi na serikali kumsaidia.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Yesige Mutajwaa, alisema watoto hao walikula mihogo yenye sumu aina ya Cynide.

Mmoja kati ya majirani wa eneo hilo Elias Zebedayo alisema njaa ndiyo imesababisha familia hiyo kula chakula hicho bila kukiandaa vizuri.

"Walikula chakula hicho nyumbani kwao na ndugu zao, na chakula hicho walikitoa shambani muda huo walianza kula bila kuandaa vizuri," alisema Zebedayo.

# Ajipongeza ujenzi wa madarasa

**Na Allan Isack, ARUMERU**

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, amesema kwa kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake kwenye wilaya hiyo, amejenga madarasa 149, ya shule za msingi na sekondari katika halmashauri mbili za Arusha DC na Meru.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Muro, alisema Wilaya ya Arumeru, ina Halmashauri mbili za Arusha Dc na Meru Dc, zenye jumla ya tarafa sita, kata 53, na majimbo mawili ya uchaguzi ambayo ni Arumeru Mashariki na Magharibi.

Alisema kampeni aliyoianzisha mwanzoni mwa mwaka huu ya ujenzi wa madarasa, amefanikikiwa kujenga madarasa 149, ambayo yamegharimu Sh. bilioni mbili.

"Leo nimeona niwaletee mrejesho wa kampeni ya ujenzi wa madarasa niliyoianzisha mwanzoni mwa mwaka huu," alisema Muro.

Aliema katika Halmashauri ya Meru wamejenga vyumba 35 vya madarasa ya shule za msingi na sekondari vyote vipo hatua za mwisho kukamilika.

Kati ya vyumba hivyo, 42 ni vya shule ya sekondari na idadi iliyobaki ni vya shule ya msingi vipo kwenye hatua za mwisho kukamilika.

Pia alisema wamejenga majengo mawili ya utawala yapo katika hatua za mwisho kukamilika, pamoja na ujenzi maabara mbili za sayansi na ujenzi wa jengo jipya na la kisasa la wadhibiti ubora wa elimu.

Katika Halmashauri ya Meru, alisema wamejenga vyumba na majengo 82 na Halmashauri ya Arusha DC, wamejenga madarasa 34, yaliyokamilika na yameshaanza kutumiwa.

Kadhalika madarasa ya shule za sekondari na msingi yaliyopo katika hatua ya mwisho kukamilika ni madarasa 73, ambayo yapo kwenye Halmashauri ya Arusha DC.

Hadi sasa kupitia kampeni hiyo, kwenye wilaya hizo, wameshajenga vyumba vya madarasa 107, kwa shule za msingi na sekondari.

Pia alisema kampeni hiyo, imewapa fursa ya kujenga vyumba 149, na lengo la serikali ilikuwa wajenge vyumba 107, hivyo kwa mantiki hiyo alisema wamevuka lengo walilojiwekea awali.

Katika suala la uandikishaji wa wanafunzi wanaojiunga na darasa la kwanza, alidai kwamba wilayani humo, idadi imeongezeka kwa asilimia 100.

**"Leo nimeona niwaletee mrejesho wa kampeni ya ujenzi wa madarasa niliyoianzisha mwanzoni mwa mwaka huu," alisema Muro.**





# Mzee Msuya ang'atuka KDF

**Na Mary Mosha, MOSHI**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya, ameng'atuka kwenye nafasi yake ya uenyekiti wa Jukwaa la Maendeleo la Mkoa wa Kilimanjaro (KDF), baada ya kuitumikia kwa uaminifu kwa kipindi cha miaka 15.

Wakati anatangaza kukaa pembeni, aliwataka viongozi wapya waliochaguliwa kuliongoza jukwaa hilo, kuhakikisha maendeleo yanapatikana kupitia wakazi wa Kilimanjaro.

Msuya alitangaza uamuzi wake huo juzi, wakati wa mkutano mkuu wa jukwaa hilo katika Manispaa ya Moshi. Mrithi wa Msuya, ni Balozi mstaafu Abubakar Ibrahim.

Kabla ya kuachia nafasi hiyo, Msuya aliwapongeza viongozi wenzake kwa ushirikiano waliompa kwa muda wote wa uongozi wake, ambapo alisema jukwaa hilo linapaswa kufikishwa hadi chini kwa wananchi ili kuleta maendeleo ya kweli.

"Jukwaa hili lilianzishwa kwa lengo la kuunganisha nguvu za wana Kilimanjaro wote, ikiwamo uongozi wa serikali ya mkoa, wananchi, wafanyabiashara, viongozi wa taasisi za kidini, taasisi binafsi na vyama vya ushirika ili kushirikiana kukabiliana na changamoto zinazoukabili Mkoa wa Kilimanjaro na jinsi ya kuzitatua," alisema.

"Mkoa wa Kilimanjaro ulikuwa ukiongoza kwa kutoa elimu bora na wasomi wengi, lakini kwa sasa unaonekana kurudi nyuma, uongozi mpya angalieni jinsi ya kutatua changamoto zilizoko kwenye sekta ya elimu Kilimanjaro," alishauri.

Aidha, aliushauri uongozi mpya kuhamasisha wananchi kujiunga na jukwaa hilo ili kuongeza idadi ya wanachama, hivyo kuimarisha uwekezaji katika nyanja mbalimbali.

Makamu Mwenyekiti wa KDF, Mahmoud Mringo, alisema uchumi wa mkoa wa Kilimanjaro ulianza kuporomoka baada ya kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya msingi pamoja kufa kwa viwanda.

Alisema ili kuurejesha katika nafasi yake, kuna kila sababu ya kuongeza juhudi katika uwekezaji kwenye sekta mbalimbali.

"Mwelekeo wetu utalenga kuimarisha viwanda vidogo vidogo, kuanzisha vingine pamoja na viwanda vikubwa ambavyo vitatoa ajira na pia kuongeza mapato ya serikali ambayo itaboresha huduma zake kwa wananchi," alisema.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, alisema serikali imekuwa ikishirikiana kwa karibu na jukwaa hilo kwani limekuwa na mchango mkubwa katika kutatua changamoto hizo.

"Serikali iko tayari kushirikiana na wafanyabiashara ili kuimarisha mikakati ya kibiashara kwa wafanyabiashara wa mkoa wa Kilimanjaro, wakubwa, wakati, hata wadogo ili kuwainua kibiashara," alisema Mghwira.

# Kiwanda cha kuchakata takataka pasua kichwa

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MKAKATI wa muda mrefu wa Manispaa ya Moshi kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata takataka na kutengeneza mbolea, sasa ni pasua kichwa.

Licha ya Meya wa Manispaa ya Moshi, Raymond Mboya kueleza kuwa ujenzi wa kiwanda hicho uko mbioni kuanza kujengwa mwaka ujao, mchakato wake umekuwa ukipigiwa chapuo kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Mei mwaka huu, Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, ilitia saini mkataba wa ujenzi huo na Kampuni ya Ukandarasi ya Rock Trotinic Ltd ya Mjini Moshi, kwa ajili ukarabati na uboreshaji wa dampo la kutupia taka ngumu utakaogharimu kiasi Sh. bilioni mbili.

"Nia yetu ni kuongeza mapato ya ndani na kisha kuinua uchumi wa mji wetu ambao tunatarajia uwe Jiji, wakati wowote Mheshimiwa Rais John Magufuli atakaporidhia.

Kwa hiyo tunajitanua kwa ujenzi wa viwanda na tumechelewa kwa sababu mbalimbali, lakini mwaka 2020 miradi hiyo itatekelezwa," alieleza Mboya.

Baadaye Septemba mwaka huu, ujumbe maalum wa wataalamu uliioongozwa na Meya wa Manispaa hiyo ulikwenda nchini Ujerumani kutia saini makubaliano ya kupokea mitambo ya kuchakata takataka na kutengeneza mbolea.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa kiwanda hicho cha kuchakata takataka na kuzalisha mbolea, uwekezaji wake unakisiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 900.

Mradi huo unatarajiwa kujengwa katika eneo lake la dampo lililopo kati ya Kata ya Kaloleni na Njoro.

Pia inaelezwa, mradi huo utaongeza uwezo wa halmashauri hiyo kuzoa taka kutoka tani 168 kwa siku hadi kufikia tani 230.

Kuhusu ujenzi wa jengo la uwekezaji kibiashara, Meya huyo alisema halmashauri hiyo pia ipo mbioni kutekeleza miradi ya ujenzi wa machinjio ya kisasa katika eneo Kata ya Bondeni.

"Maeneo ambayo tumeainisha kwamba tutawekeza huko ni kuenga jengo la uwekezaji wa kibiashara eneo la stendi kuu ya mabasi, masoko, kujenga soko la kisasa eneo la Shanty Town, kujenga soko la ghorofa eneo la Mbuyuni," alisema Mboya.




Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha Walimu wa wilaya za Hai na Siha, Terewandumi Swai, akikabidhi vifaa vya masomo kwa mmoja wa watoto yatima 25 wanaolelewa na Kituo cha Hope Evangelist Ministry cha Wilaya ya Siha, juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Shirika launganisha wataalamu elimu, jamii

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

SHIRIKA la kiraia la Connects Autism Tanzania (CAT), limeanza kazi ya kuwaunganisha wataalamu wa elimu, ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii wa mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Lengo ni kuweka mikakati ya pamoja ya utoaji wa elimu jumuishi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa akili na ulemavu mwingine.

Akizungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa mkakati huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, GraceAnna Lyimo, alisema nia ni kuongeza fursa ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu kupata huduma stahiki za elimu kulingana na mazingira wanayoishi na changamoto za umbali zinazowafanya watoto hao kukosa fursa hiyo.

"Tumeshamaliza mchakato huo kwa mkoa wa Arusha, na sasa tunahamia tena mwaka ujao katika mkoa wa Kilimanjaro kutengeneza timu ya pamoja ya wataalamu. Tutawakutanisha maofisa elimu mkoa, ofisa taaluma wa elimu ya watu wazima mkoa na ofisa taaluma mkoa.

Aliongeza: "Wengine ni mdhibiti ubora wa elimu wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini, maofisa ustawi wa jamii na maendeleo ya jamii ngazi ya mkoa na maofisa elimu maalumu kwa wilaya sita za mkoa wa Kilimanjaro."

Shirika hilo lilianzishwa kwa ajili ya kushirikisha, kuunganisha na kuelimisha jamii kuhusu ulemavu wa akili.

Alipotafutwa Makamu Mwenyekiti Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (Shivyawata) Mkoa wa Kilimanjaro, Hellen Mmbando, kuzungumzia uamuzi wa CAT wa kutafuta dawa ya kuwasaidia wenye ulemavu kupata elimu stahiki, alisema wao wanaunga mkono juhudi hizo na wapo tayari kutoa ushirikiano.

Shirika hilo pamoja na mambo mengine, linatengeneza mjadala utakaotoa mapendekezo kuhusu utambuzi na upimaji wa mapema kwa watoto wenye ulemavu kupata afua stahiki za elimu na utekelezaji wa vitendo falsafa ya elimu jumuishi.

Agosti 13, mwaka huu, shirika hilo lilianzisha mafunzo ya stadi za jamii na ufundi sanaa kwa vijana 10 wenye umri wa miaka 18 ambao watapewa elimu hiyo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 24, 2019
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 17

## Ununuzi sahihi unabeba marufuku kwa rushwa

Ukurasa 18


## NMB na tabasamu kwa Watanzania wenye uhitaji


Ukurasa 19

## Kuinua ufikiri kwa mijadala bila mitaala wezeshi si rahisi



# Mambo ya msingi kisheria ya kufahamu ukikamatwa

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# Tuutetee usalama utuingize 2020

LEO naomba nitoe nasaha kuhusu umuhimu wa kitu kinachoitwa 'usalama' ambao ni muhimu kwa kila jambo.

Bila usalama, hakuna uhai kwa kitu chochote kinachoishi, unachokifikiria, kuanzia wanadamu, taasisi, mifumo, mipango, mali na kila utakachofikiria.

Hapa tutofautishe kati ya usalama na hali ya kuwa salama. Kuwa salama ni zao la usalama. Usalama ni mipango ya kujiweka mbali na hatari, kwa kuizuia au kuiepuka.

Mipango inayoitwa usalama ikifanywa kwa mafanikio, ndiyo inayoleta hali ya kuwa salama.

Nyumba inayolindwa kwa mipango ya ulinzi madhubuti, huitwa ina usalama, lakini nyumba isiyo na ulinzi huchukuliwa haina usalama.

Usalama ni jambo la kiasili linalowahusu viumbe wote hai na taasisi zote. Hapo kuna mashirika, kampuni, klabu za michezo, vyama, vyombo vya habari na viwanda. Ni hali inayohusika kwenye nyanja zote za maisha, kama uchumi, siasa, utamaduni na masuala ya kijamii. Jambo hilo linaanzia kwa mtu binafsi, hadi taifa.

Usalama unakuwepo penye uwezekano wa hatari inayotengeneza woga wa kupoteza maisha, kupata hasara au kushuka hadhi.

Kwa sababu usalama huanzia kwa mtu binafsi kwenda kwa familia, hadi juu kwenye nchi na mataifa, kila mtu miongoni mwetu ana wajibu wa kuujenga usalama.

Polisi ni watekelezaji tu wa hatua za usalama ambazo, sisi tunapaswa kuzianzisha. Kuna njia mbili kubwa za kutekeleza hilo. Inaanza na kujiepusha kufanya mambo ya hatari na kuwazuia tunaowamudu wasifanye hayo.

Sura ya pili ni kuwafichua wafanyao uhalifu mkubwa kwenye sehemu za makazi na ofisi za umma.

Kwa upande mwingine, wachukuaji hatua nao wanapaswa kufanya mawili makubwa; kwanza, kufanyia kazi kwa umakini na usahihi hatua hizo wanapopokea taarifa za uhalifu.

Pili, kuwalinda kwa nguvu zote watoa taarifa kwa njia ya kuwaficha na kuwapa kwa siri motisha ya kuwahamasisha wafichue maovu zaidi na wawashawishi waaminifu wenzao kufanya jambo hilo lenye tija.

Hili la kufichua uhalifu lina umuhimu mkubwa kwa maisha yetu ya mtu mmoja mmoja na familia, kwani wahalifu hatari watatudhuru wakianza na mtu mmoja hadi familia nzima. Kwa ofisi, watu wachache wanaweza kuzifilisi na tunaobaki tukarudi mitaani hohehahe.

Nina mfano wa shirika moja kubwa la umma lililosambaratishwa kwa ubadhirifu na watu wachache mpaka likafa na mwingine, chama cha ushirika katika Kanda ya Ziwa kilichoanguka kwa wizi wa watumishi wachache wasio waaminifu.

Baadhi wangefichua uhalifu huo na ukadhibitiwa, wasingeadhirika mitaani kwa wizi wa wachache. Tunapoongelea usalama wa nchi yetu, ni vizuri tutumie muda wa kutosha kushawishiana kufichua wahalifu wakubwa popote walipo.

Kinachosikitisha ni kuwapo viongozi ambao wakipata fursa za kuongea na wananchi kuhusu usalama, wanachosisitiza ni vijana waache kushawishiwa na wanasiasa kuleta chokochoko za kuvuruga amani, kwa kuandamana.

Kwa wanasiasa, hatari kubwa kuliko zote ni wao kwa wao wanavyotikisana.

Ni busara watu wakiombwa kufichua uhalifu mkubwa wa kudhuru watu na kuharibu mali, wafanye hivyo.

Tujenge taifa ambalo kila mtu atafichua wizi kwenye taasisi yake, tuwabainishe wanaochoma shule zetu na wanaomiliki bunduki kuua watu na askari wetu wanaotulinda.

Tuwape taarifa zote Polisi, ili walinde usalama wetu. Uhai ni wetu, maisha ya ajira ni yetu, usalama ni wetu na askari. Polisi ni walinzi wetu. Tuwape taarifa ili tuwe salama kutokana na kazi yao.

***Mungu Ibariki Tanzania***



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas (wa pili kushoto), akiwa katika moja ya majukumu yake. **PICHA: MTANDAO**

## JIELIMISHE

### China wafundisha watoto kusoma maneno 100,000 kwa dakika tano



Wanafuzi China wakiwa katika mafunzo ya kusoma. **PICHA: MTANDAO**

MWINGEREZA Dan Holloway ni msomaji wa haraka zaidi ulaya. Aliweza kuonyesha uwezo wake wa kusoma maneno 1,700 kwa dakika moja katika mashindano ya mwaka 2018.

Kituo cha mafunzo ya ziada nchini China, kinajaribu kuwafundisha watoto kusoma haraka kama Holloway:

Kituo hicho kinadai kuwa kinaweza kuwafundisha wanafunzi kuwa na uwezo wa kusoma maneno laki moja ndani ya dakika tano.

Lakini mafunzo haya ya kuonyesha mbinu za kusoma kwa kasi yamekuwa na utata, baada ya video inayomuonyesha mwanafunzi anavyofungua karatasi za kitabu kwa kasi kusambaa kwa watu wengi huko Beijing.

**UTAFITI**

Katika mashindano haya, wanafunzi wanasoma vitabu kama kadi kwa kuzichanganya.

Namna hiyo ya kusoma ni kufungua kurasa kwa haraka na picha ndio inaweza msaidia msomaji kuelewa maudhui ya kile anachokisoma.

Hata hivyo, mbinu hiyo imekosolewa na wengi na kudaiwa ni ulaghai tu.

Mamlaka ya elimu imetoa angalizo kwa kutoa tamko kusema kuwa ni marufuku kwa shule za awali au sekondari kufundisha masomo ya aina hiyo.

Vilevile watafanya utafiti kujua ni kina nani wanaofundisha wanafunzi masomo hayo ya kusoma kwa haraka.

**HOFU**

Wataalamu wa elimu wanahofia kuwa mafunzo ya namna hiyo yanawapotosha watu, lakini mafunzo hayo tayari yamepata umaarufu kutoka kwa watu wengi kwa sababu tofautitofauti.

Hofu inyoonekana kwa sasa ni kuwa na kiwango kidogo cha masomo ya sayansi na ukosefu wa kutumia kanuni pamoja na mapungufu mengine, ndio maana serikali imewataka wazazi na wanafunzi nchini China kulenga kupata elimu bora.

Mafunzo haya ya kusoma kwa kasi yalianzishwa nchini Japan na mwalimu Yumiko Tobitani, ambaye alichapisha kitabu chake cha mbinu za kusoma mwaka 2006.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya China, kampuni zinazotoa huduma hiyo ya mafunzo ziko kwenye miji mikubwa kama Beijing, Shenzhen, Guangzhou na Hangzhou.

Gharama ya mafunzo hayo huwa ni kati ya fedha za kimarekani dola 4,200 mpaka 8,500. Gharama kubwa zaidi ya ada ambayo mteja anaweza kulipa si zaidi ya dola 14,000.

Wachina wengi wamewadhihaki wazazi wanaowapeleka watoto wao kwenye mafunzo hayo.

Xiong Bingqi, mkurugenzi msaidizi wa taasisi ya utafiti wa elimu katika karne ya 21 ameiambia BBC kuwa mbinu hiyo inakosa mbinu za kisayansi na iko kinyume na utaratibu wa kawaida wa elimu na kutozingatia uelewa wa mwanafunzi.

**UJUZI MDOGO WA KISAYANSI**

Chu Zhaohui, mtafiti wa elimu ya sayansi ameiambia BBC kuwa mafunzo hayo yamekosa kutoa ujuzi wa kisayansi, jambo ambalo inabidi walaumiwe.

Anasema kuwa mafunzo hayo yanashindwa kuhusisha wazo la sayansi na uwezo wa kisayansi wa kuhusisha mambo

"Watoto wengi huwa wanawadanganya wazazi kuwa taarifa ambazo zimeandikwa kwenye magazeti zinapotosha na masomo hayo yanachangamsha ubongo. Jambo ambalo haliwezekani kabisa," anasema Chu.

Lakini wazazi watawezaje kuepuka uongo huu wa mbinu za kurahisisha upatikanaji wa ujuzi?

Xiong Bingqi anaamini kuwa kampuni zinazotoa mafunzo hayo zinapaswa kuwa chini ya uangalizi mkubwa, vituo vingi vya mafunzo hayo havijajisajili kwa kuzingatia taratibu za elimu nchini humo.

Aidha, Chu anadhani kuwa kubadilisha mfumo wa elimu nchini humo kunaweza kusaidia.

Kuna namna moja ya kuleta mabadiliko ya kutathmini uelewa wa masomo.

Chu anadai kuwa mbinu hiyo ya mafunzo inaua fursa za wanafunzi katika kujifunza na kuelewa.

"Wazazi na wanafunzi wanakuwa wanazingatia kupata alama za juu badala ya kuzingatia ujuzi," anasema. **BBC**

SAYANSI

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Kuishi kirafiki na mazingira ni kuepuka athari, majanga

KUNA usemi usemao "Hakuna lisilowezekana chini ya jua": Huwa najiuliza chimbuko la usemi huo ni nini?

Jibu kamili sina, ila pengine kilichomaanishwa ni kuwa na ari ya kutaka kufanikisha jambo muhimu katika maisha.

Vilevile ni kama kusema "penye nia pana njia", kwa msingi kwamba ukiwa na uthubutu wa kweli utafanya na kufanikiwa.

Yote heri isipokuwa tujitahidi tukimtanguliza Mwenyezi Mungu au kwa maneno mengine "Mungu Kwanza" kabla ya yote.

Hii ni muhimu sana maana yeye ndiye aliyetuumba na binadamu bila kuwepo nguvu ya Mungu au uwezo wa kimbingu juu yetu ni sawa na kazi bure.

Baada ya uumbaji wa vitu vyote alituumba binadamu kwa sura na mfano wake na akatupa madaraka ya kumiliki na kutawala vitu vyote vilivyopo juu na chini ya ardhi, kwenye maji pia vilivyopo angani.

Kusema kuwa hakuna lisilowezekana chini ya jua ni mtazamo chanya wa kuelekea kwenye dhana ya kumiliki na kutawala.

Namshukuru Mungu kwa kutofautisha binadamu na viumbe wengine kwanza, kwa kutuumba kwa sura na mfano wake, hii ni heshima kubwa kwetu.

Pili, kwa kutupa uwezo huo kumiliki na kutawala raslimali zote duniani isipokuwa kukatazwa kula matunda ya mti uliokuwa katikati ya "Bustani ya Edeni".

Hata hivyo, binadamu alishindwa kutii amri hiyo na kusababisha udhaifu kwenye kumiliki na kutawala hivyo kusababisha laana kumwandama mpaka leo.

Hali halisi tunayoishuhudia nyakati hizi zenye maafa mengi duniani ni matokeo ya udhaifu uliojengeka miaka mingi kutokana na kutotii pamoja na kujengeka ubinafsi zaidi kuliko kuwapo mtazamo halisi wa kutumia raslimali tulizopewa na Mwenyezi Mungu kwa misingi endelevu na kwa faida ya wanajamii wote au kwa maslahi mapana ya taifa letu.

Kwa hali hiyo shughuli nyingi za kibinadamu mijini na vijijini; zimekuwa na matokeo hasi kwa mazingira. Mathalani, ukataji ovyo wa miti na ufyekaji wa misitu ya asili bila kufuata kanuni za uhifadhi wa mazingira, kuchoma mapori moto au kutotekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini, kumesababisha misitu ya asili na uoto juu ya ardhi kutoweka.

Kabla na baada ya kupata uhuru, hali ya mazingira nchini ilikuwa ni ya kijani ukilinganisha na sasa.

Ingawa idadi ya watu ilikuwa chini ya milioni 10 wakati tunapata uhuru, na sasa inakadiriwa kuwa milioni zaidi ya 55 na mifugo zaidi ya milioni 35; hatuwezi kusema ongezeko hilo ndiyo sababu kubwa ya uharibifu wa mazingira kuwa mkubwa kiasi hicho.



Ukataji wa misitu ni moja ya sababu zinazosababisha madhara kwa binadamu kutokana na mabadiliko ya tabianchi. **PICHA: MTANDAO**

> "Sasa tunalia na athari za mabadiliko ya tabianchi, kumbe kisababishi ni kazi za mikono yetu na kinachosababisha ongezeko kubwa la joto duniani.

#### KUMILIKI NA KUTAWALA

Kwa mtazamo wangu, sababu kubwa ni kushindwa kumiliki na kutawala vyote kwa kutumia njia endelevu.

Kukosekana utayari wa kutumia raslimali asilia ikiwamo misitu; wanyamapori; ardhi, maji, samaki na kadhalika: kwa misingi endelevu (sustainable use) ndio chanzo kikubwa kinachosababisha maafa kuongezeka.

Sasa tunalia na athari za mabadiliko ya tabianchi, kumbe kisababishi ni kazi za mikono yetu na kinachosababisha ongezeko kubwa la joto duniani.

Matokeo ni maafa kila mahali ikiwamo Bara la Afrika kukumbwa na njaa, ukame, mafuriko, kupoteza uhai na mali kama nyumba kubomoka au kuezuliwa paa.

Uoto wa asili kwenye nchi za Afrika ikiwamo Tanzania umetoweka kwa kasi kubwa.

Tanzania kwa mfano, inakadiriwa kupoteza misitu ya asili kwa kiwango cha hekta kati ya 370,000 na 470,000 kwa mwaka kutegemea hali halisi ya mahalia (locality).

Hivyo, maeneo mengi nchini hayana uoto wa asili kama ilivyokuwa miaka iliyopita.

Kila kukicha uoto wa asili; nyasi, mimea, miti na misitu vinapotea kwa kiwango kikubwa.

Ndiyo maana kwa nyakati hizi, tofauti na zamani, mvua ikinyesha baada ya muda mfupi tu mafuriko yanatokea.

Vilevile, msimu wa mvua ukiisha baada ya muda mfupi upatikanaji wa maji unakuwa wa shida (chemichemi zinakauka na mito mingi kuwa na maji kidogo).

Kwa nini kumekuwapo na athari hizo nyakati hizi kuliko zamani? Binadamu, pamoja na idadi ya watu kuongezeka, hatuishi kirafiki na mazingira au hatumiliki na kutawala kwa kuzingatia misingi sahihi; na badala yake tumekuwa waharibifu wa mazingira na sasa yanatugeuka na kutuangamiza.

Kwa miaka ya nyuma mvua zilikuwa zinanyesha za kutosha. Nakumbuka nikiwa kijana miaka ya 1950 na 1960, mvua za masika zilikuwa nyingi kiasi cha kushindwa kupata kuni za kupikia chakula.

Kaya nyingi zililazimika kuweka kuni za kutosheleza mahitaji nyakati za masika kinyume cha hapo "mtapiga miayo" (yearning) kutokana na njaa kwa kukosa nishati ya kupikia kisa mvua nyingi wakati wa masika.

Wakati hali ni hivyo, mafuriko makubwa au kubomoka madaraja ilikuwa nadra sana tofauti na hali ilivyo sasa.

Hali ilikuwa salama zaidi kuliko sasa maana tulikuwa bado tunaishi kirafiki na mazingira, hivyo uoto wa asili ulikuwapo wa kutosha.

Kwa maneno mengine, kukiwepo na uoto wa asili wa kutosha (sufficient natural cover) maji ya mvua huingia ardhini taratibu na hatimaye kutiririka kwenye mito hata nyakati za kiangazi, lakini ardhi/udongo kuhifadhiwa.

Hivyo kutokuwapo uoto wa asili wa kutosha athari kwa ardhi/udongo na upatikanaji maji nyakati za kiangazi ni kubwa.

#### WATU NA MIFUGO

Ongezeko la watu au mifugo kwa mtazamo wangu havijawa tishio kwa maisha yetu na hasa tukizingatia kuwa Tanzania Bara ina eneo kubwa takribani hekta zaidi ya milioni 88.

Kwa idadi ya watu milioni 55 ni sawa na kila mtu kumiliki hekta takribani 1.6 na familia ya watu 10 kuwa na hekta 16. Kwa idadi ya mifugo takribani milioni 35 ni sawa na mtu mmoja kuwa na mfugo mmoja.

Hii inaonyesha kuwa kiuhalisia bado ardhi inatosha isipokuwa matumizi yake siyo endelevu (not sustaibable). Sehemu mbalimbali nchini tunalima kwa kufyeka misitu ya asili (kilimo cha kuhamahama), hatufugi, tunachunga mifugo; ardhi inatumika kama haitakiwi kwa vizazi vijavyo.

Matokeo yake ni kutoweka uoto wa asili na hivyo maji ya mvua kusababisha mmomonyoko mkubwa wa udongo. Hatimaye ukame na njaa kutokama na kilimo duni. Maji ya mvua yakishindwa kuingia taratibu ardhini, husomba udongo na kila aina ya takataka na kupelekwa mabondeni na kwenye mito.

Hali hiyo inasababisha vina vya mito (riverbeds) kupungua kutokana na kujaa udongo, mchanga, matope na takataka za kila aina ikiwamo maplastiki.

Mfano, Mto Msimbazi (jijini Dar es Salaam) umesheheni mchanga na uchafu wa kila aina) hivyo maji ya mvua husambaa haraka na kusababisha mafuriko wakati wa mvua. Madaraja na barabara kubomoka ni matokeo ya maji ya mvua kutoingia ardhini na badala yake kujaza mito haraka.

Isitoshe njia za asili ambazo maji ya mvua hupita zimezibwa hivyo kusababisha maji kuzagaa sehemu ambazo hayastahili kuwapo.

***Mwandishi Mwenyekiti, Taasisi ya Uhifadhi wa Maliasili na Mazingira (WCST), anapatikana kupitia P.O. Box 79011, Dar-es-Salaam, Tanzania,***

ELIMU

**NA FRANSISKO MPANGALA**

# Mambo ya msingi kisheria ya kufahamu ukikamatwa

KATIBA ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 15 (2) inasema " Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo isipokuwa (a) katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au (b) katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na Mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai."

Tafsiri ya ibara hii ni kuwa hairuhusiwi kwa mtu yeyote au chombo chochote kunyang'anya uhuru wa mtu kuwa huru (kukamata) kinyume na njia zilizoainishwa na sheria zetu za nchi au wakati wa kutekeleza amri ya Mahakama.

Busara ya ibara hii ni kutoa fursa kwa kila mtu ndani ya nchi kupata nafasi ya kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo yake binafsi na yale ya kijamii kwa uhuru wa kwenda mahali popote bila kuzuiwa au kupata kizuizi chochote.

Ni vigumu kwa mtu kushiriki katika shughuli za maendeleo kama hayuko huru au amezuiwa kwenda mahali popote anakoona kunafaa kujipatia riziki.

Kwa maana hii, ni lazima ziwepo taratibu za kisheria ambazo zinapaswa kufuatwa wakati wa kuiondoa haki hii. Tuna wajibu wa kuepuka kufanya makosa ambayo yatatufanya tukamatwe na kuondolewa haki hii ya kikatiba ya kuishi kama mtu huru.

Hata hivyo, pamoja na kwamba tunaweza kujitahidi kuepuka kufanya makosa, maisha nayo hayatabiriki. Yumkini unaweza kukamatwa kimakosa au likatokea jambo lolote lisilotarajiwa litakalokufanya ukamatwe.

Na hata usipokamatwa, yumkini mtu yoyote wa karibu kama rafiki, ndugu au jirani anaweza kukamatwa. Kimsingi, kukamatwa ni jambo linaloweza kumtokea mtu yoyote. Kwa maana hii, ni muhimu kupata taarifa za kutosha zinazohusiana na kukamatwa.

Taarifa hizi zitakupa mwongozo wa kujua haki na wajibu wako pale unapokamatwa au mtu wako wa karibu anapokamatwa.

Kwa maana hii, yafuatayo ni baadhi ya mambo ya msingi ya kufahamu pale mtu yoyote anapokamatwa.



Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam. PICHA ZOTE: MTANDAO

### MAANA YA KUKAMATWA

Kumkamata mtu kwa mujibu wa sheria ni kitendo cha kumwondolea uhuru wake wa kufanya harakati zake za kila siku kwa kumpeleka kwenye kizuizi kinachotambulika kisheria.

> Unamshtaki mumeo, halafu ukirudi utaishi kwa nani? Familia zitapasuka lakini leo waathirika wanajua jinsi ya kutumia dawati la jinsia la polisi na waathirika wanaungan-

Mtuhumiwa anawekwa kizuizini ili apelekwe mahakamani (mapema kwa kadri itakavyowezekana) kujibu mashtaka ya jinai yanayomkabili. Anaweza pia kuwekwa kizuizini kwa lengo la kufanyiwa upelelezi juu ya mashtaka ya jinai yanayomkabili.

### JINSI YA KUMKAMATA MTUHUMIWA

Sura ya 20 ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, ndiyo sheria inayotoa mwongozo wa namna na jinsi ya kumkamata mtu.

Kwa kawaida kukamatwa kunahusisha kugusa au kumshika mtuhumiwa kwa namna itakayomfanya ashindwe kumtoroka au kumkimbia mtu aliyemkamata.

Kama mtu anayekamatwa atajaribu kukimbia au kufanya jaribio la kuzuia tendo la ukamatwaji halali kufanyika, mtu au ofisa anayemkamata anaruhusiwa kutumia nguvu kiasi.

Ukamatwaji haupaswi kuendeshwa kwa maslahi binafsi, ukamatwaji unatakiwa kufanywa kwa nia njema ukizingatia utu, usiri na haki za binadamu. Mkamataji anapaswa kutanguliza maslahi ya kutenda haki wakati anamkamata mtuhumiwa.



Pingu kwa ajili ya kumfunga mtuhumiwa.

### AINA ZA UKAMATAJI

Kuna aina mbili za ukamataji. Kumkamata mtu kwa kutumia kibali na kumkamata mtu bila kutumia kibali. Ukamatwaji unaotumia kibali kwa kawaida unatolewa na hakimu, katibu kata au katibu wa halmashauri ya kijiji baada ya kupokea taarifa iliyo chini ya kiapo ikimtuhumu mtuhumiwa kuwa kuna sababu za msingi za kuamini kuwa mtu husika ametenda kosa.

### BILA KIBALI

Ukamatwaji usio na kibali ni ukamatwaji unaofanywa pale makosa kama uvunjifu wa amani mbele ya polisi au hakimu yanapotokea, kumzuia ofisa wa polisi kutekeleza majukumu yake au kitendo chochote kinachoazimia kutusi nembo ya taifa au bendera ya taifa.

### SABABU ZA MTU KUKAMATWA

Polisi au ofisa anayemkamata mtuhumiwa ana wajibu wa kutaja kosa au kutoa sababu zinazomfanya amkamate mtuhumiwa.

Ieleweke kuwa si kila kosa linaweza kukufanya ukamatwe (na hasa makosa ya madai).

Zifuatazo ni baadhi ya sababu zinazoweza kumfanya mtu akakamatwa.

### MAKOSA YA JINAI

Kwanza, makosa ya jinai kutegemeana na aina au uzito wa kosa ambalo mtuhumiwa ametuhumiwa kulifanya. Endapo mtuhumiwa atadhaniwa kufanya kosa la ugaidi, uhaini, kunyang'anya kwa kutumia silaha na makosa mengineyo ya jinai, yatamfanya akamatwe mara moja.

### AMRI HALALI

Sababu nyingine inayoweza kumfanya mtu akamatwe ni kudharau kutii amri halali ya Mahakama au kukwepa kwa makusudi kufikiwa na wito wa kufika mahakamani.

Yumkini mtuhumiwa ameitwa mara kadhaa mahakamani au amekataa kupokea wito, basi mtuhumiwa anaweza kukamatwa kwa kosa hili.

### USALAMA WA MTUHUMIWA

Ulinzi wa uhai na usalama wa mtuhumiwa unaweza kuwa sababu ya tatu itakayomfanya mtu akamatwe.

Mtuhumiwa anaweza kufanya tukio linaloweza kuibua hasira kali kwenye jamii na hivyo wananchi wakataka kuchukua hatua mkononi. Kama polisi amejiridhisha kuwa uhai wa mtuhumiwa uko hatarini, mtuhumiwa anaweza kukamatwa na kuwekwa kizuizini kwa muda ili kulinda uhai na usalama wa maisha yake.

### USALAMA WA JAMII

Sababu ya nne inayoweza kumfanya mtu kukamatwa ni pale usalama wa jamii na watu wengine unapokuwa hatarini.

Yumkini mtu husika ana matatizo ya akili au ni mtu anayependa kufanya vurugu, kuharibu mali na kujeruhi watu.

Polisi na viongozi wa maeneo husika wakijiridhisha kuwa anavyoendelea kuwa uraiani atazidi kufanya uharibifu nayo inaweza kuwa ni sababu ya kumkamata mtu husika.

Lengo la ukamatwaji huu ni kumdhibiti mtu husika asiendelee kufanya uharibifu.

### UKAMATAJI KINYUME NA SHERIA

Ukamataji ulio kinyume na sheria ni ule unaofanywa kinyume na vipengele vya kisheria vilivyopo kwenye Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai vinavyoelekeza namna na jinsi ya kumkamata mtuhumiwa.

Ukamatwaji ulio kinyume na sheria unahusisha mambo yafuatayo:- Kumkamata mtu bila kuwa na mamlaka ya kisheria, kumkamata mtu bila kumtaarifu sababu za kumkamata, kutumia nguvu kubwa (zilizopitiliza) kumkamata mtu bila sababu za msingi, kumuweka mtuhumiwa kizuizini kwa muda mrefu tofauti na mahitaji ya kisheria yanavyotaka.

Mtuhumiwa anatakiwa apelekwe mahakamani ndani ya saa 24 au kuachiwa kwa dhamana.

Vitendo vya kikatili au vitendo vilivyo kinyume na haki za binadamu wakati wa ukamatwaji navyo haviruhusiwi kwa mujibu wa sheria.

### MADHARA

Yapo madhara kwa polisi au ofisa kumkamata mtuhumiwa kwa namna iliyo kinyume na sheria.

Mtu aliyekamatwa kinyume na sheria anaweza kumshtaki ofisa husika kwa kosa la shambulizi, matumizi mabaya ya mamlaka ya kipolisi, au ofisa husika kuadhibiwa kitaaluma kwa kufanya makosa ya kinidhamu (professional misconduct).

Kama mtuhumiwa amekamatwa kimakosa au hakuna sababu ya msingi ya kuendelea kumshikilia, basi anapaswa kuachiwa mara moja. Vinginevyo anapaswa kupewa dhamana au kupelekwa mahakamani (iliyo karibu na kituo) ndani ya saa 24 baada ya kukamatwa kama inavyoelekeza Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kifungu cha 33.

Endapo mtuhumiwa ataendelea kushikiliwa kwa zaidi ya saa 24 bila kupelekwa mahakamani, basi upande wa mshtakiwa utaomba agizo la kimahakama litolewe (habeas corpus) ili mtuhumiwa aweze kupelekwa mahakamani kama sheria inavyoelekeza.

***Mwandishi anapatikana kupitia Barua pepe;fransiscompangala08@gmail.com***

---

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Ununuzi sahihi unabeba marufuku kwa rushwa




Wadau wa tasnia ya ununuzi wakiwa mkutanoni. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Niko Kasera**

TAALUMA za fedha na mfumo wa ugavi, zinakaribiana kwa kiwango kikubwa.

Wakati uhasibu unasimamia fedha zinazolipwa na kupokewa, kuandaa mahesabu, ripoti zake na kusimamia usalama wake (ukaguzi wa hesabu) na ugavi unahusu kununua bidhaa au huduma, kuisimamia ghalani, kupitia hesabu zake na kutoa inapohitajika.

Je, unapozungumzia 'hifadhi' na 'ununuzi' una maana gani? Kuhifadhi ni kumiliki vitu sahihi, kwenye ubora na mazingira sahihi.

Vivyo hivyo, ununuzi unaangukia katika namna ya kupata vinavyohitajika vikiwa vimetimiza vigezo vikuu vitano vilivyo sahihi: Chanzo au ilikopatikana, idadi na ubora, bei na wakati unaotakiwa. Kitaalamu hujulikana kama 'five rights' au '5 R.'

Kwa kawaida, msimamizi au mratibu wa ununuzi ni mtaaluma wa fani hiyo aliyemo katika kitengo cha kitaalum, aliyeundiwa mfumo, sheria na miongozo ya kitaasisi hadi juu serikalini.

Nchini kuna Sheria ya Taifa ya Ununuzi wa Umma, 2011 na kanuni zake za mwaka 2013, kisha marekebisho ya mwaka 2016.

Inaelezwa kitaaluma, uwazi kwenye ununuzi una nafasi nzuri kuzuia viashiria vya rushwa. Tayari serikali ina taasisi zinazoshughulikia uwazi, ikiwamo PPRA (Bodi ya Ununuzi wa Umma), huku taaluma ikisimamiwa na Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa (NBMM), kama ilivyo uhasibu chini ya NBAA.

Wataalamu wanaainisha ufisadi unaotendwa na kusababishwa na watu binafsi na sio wataaluma wa ununuzi.

Nchini Tanzania, wana fani hiyo sasa wako wengi na wanakuja pamoja kwa lengo la kuhakikisha eneo hilo nyeti halitumiwi na wachache kuchafua tasnia nzima kwa maslahi binafsi.

Ili kununua kwa uwazi bidhaa ikiwa nyingi, kanuni na taratibu za ununuzi unaanza kwa taasisi husika kutangaza zabuni ya uwazi, ikiainisha mengi muhimu, ikiwamo vigezo na masharti. Ni muhimu matangazo yakapitishwa kwenye mfumo wa habari kwa kuzingatia muda wa kutosha, unaowezesha wagombea kuendana na mahitaji ya ununuzi fasaha, ikiwamo ya '5R.'

Pia, katika mchakato wa kumpata muuzaji, sharti mnunuzi au mhusika wake kwa namna yoyote, asihusike, lengo ni kufuta uwezekano wa upendeleo au maslahi binafsi.

Mchakato mzima unapaswa kuonyesha vigezo vitakavyotumika kumpata mshindi wa zabuni na vigezo vilivyoainishwa kwenye zabuni.

Historia inaonyesha, hapo ndipo kwenye hatua ambazo mara nyingi ununuzi unakiukwa. Hata katika baadhi ya maeneo, vigogo wenye ushawishi katika eneo husika wawe wa kisiasa, kiutawala au wafanyabiashara hutumia nafasi zao kushinikiza zabuni ziangukie maslahi yao na hapo ndipo panashuhudiwa shinikizo kuongezwa la bei na ukiukaji miongozo na imani.

Hivi karibuni jijini Nairobi, Kenya kulifanyika kongamano lililojadili uwazi katika ununuzi na wataaluma wa Kitanzania walihudhuria.

Miongoni mwa yaliyojadiliwa ndio yanayopewa uzito mkubwa na serikali iliyoko madarakani sasa, hasa katika upatikanaji huduma muhimu za kijamii kama vile majisafi na salama, afya na elimu.

Hivyo, ni dhahiri uwazi kwenye ununuzi ni suala la lazima, huku baadhi ya nchi kama vile Japan ina uthibitisho wa kitafiti kwamba uwazi kwenye ununuzi unapunguza ufisadi kwa asilimia 20.

Hiyo ina maana kwamba tija katika mfumo wa ununuzi una sura pana ya manufaa, ikiwamo kimaadili.

Pamoja na hayo, haina maana uwazi unatumika kila mahali. Kuna baadhi ya maeneo ununuzi unaangukia katika usiri, mfano hai ni katika mahitaji ya kiusalama, jambo ambalo ni sahihi kwa asilimia zote.

Hivyo, inahitajika kuwapo mchakato unaolingana na mazingira yake na kuzingatia maslahi mapana, japo haipotezi umuhimu wa nafasi tano za usahihi; chanzo, bei, ubora, idadi na wakati.

**Kwa maoni na ushauri, baruapepe: samawatiarts@yahoo.com**

SAYANSI

**NA MWANDISHI WETU**



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Isandula wakisoma kipeperushi cha NMB wajibu account wakati wa kupokea msaada wa vifaa vya ujenzi na madawati. **PICHA: NMB**

# NMB na tabasamu kwa Watanzania wenye uhitaji

HAKUNA sheria maalum nchini, inayozilazimisha kampuni kuchangia katika miradi mbalimbali ya kijamii.

Bunge la Tanzania lilitunga sheria tatu zinazosimamia maliasili za Julai 2017 ambazo, pamoja na mambo mengine zinalazimisha kampuni za uchimbaji wa mafuta, gesi na madini kuweka bayana mipango ya kila mwaka juu ya uwajibikaji kwa jamii (CSR), iliyokubaliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Sheria hizo zinazilamisha kampuni zenye leseni za uchimbaji wa maliasili hizo, kulipa asilimia 0.07 ya mapato yao ya mwaka kupitia CSR kwenda kwa halmashauri zinazozunguka maeneo yao ya kazi.

Licha ya sheria kuwa kimya juu ya kile kinachopaswa kufanywa na kampuni, wadau wa sekta za ziada katika kuwajibika kwa jamii kupitia CSR, zipo kampuni na taasisi ambazo zimeenda mbali katika kushughulika na changamoto na mahitaji ya kijamii.

Mojawapo ya taasisi hizo ni Benki ya NMB.

Benki hiyo kwa mfano, imepiga hatua kubwa kupitia sera rasmi iliyojiwekea ya kutoa asilimia 1 ya pato lake baada ya makato ya kodi, kuielekeza pesa hiyo kusaidia utatuzi wa changamoto na kuunga mkono miradi ya kijamii.

CSR ya NMB kimsingi imelenga kusaidia sekta za elimu, afya na uwezeshaji katika majanga, ambako kupitia sera hiyo, benki hiyo imetumia takribani Sh. bilioni 4 kusaidia miradi ya kijamii katika miaka minne iliyopita.

> Hii ndio sababu katika miaka mitano iliyopita, tumejikita katika kutoa vifaa tiba na vifaa vya hospitali kwa zahanati na vituo vya afya zaidi ya 333 kote nchini.

Kwa kufanya hivyo, NMB imeiongezea nguvu serikali kukabiliana na changamoto za kijamii na kujenga misingi imara ya utoaji wa huduma bora kwa mamilioni ya Watanzania.

### SERA YA ELIMU BURE YA RAIS MAGUFULI

Novemba 2015, Rais wa Awamu ya Tano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, alitoa ahadi ya elimu bure kwa wanafunzi kuanzia shule za msingi hadi sekondari.

Utekelezaji wa ahadi hiyo, ulisababisha ongezeko kubwa la wanafunzi shuleni na kwa mantiki hiyo kukawa na mahitaji makubwa ya ujenzi wa miundombinu ili kuziwesha shule kukabiliana nalo.

Kwa kutambua umuhimu wa kuiunga mkono serikali na watoto wa Tanzania ili kufikia malengo na matarajio yao kitaaluma, NMB ikaja na misaada kupitia CSR, ambayo hadi sasa imewanufaisha zaidi ya wanafunzi 93,000 wa shule za msingi na sekondari kote nchini.

Kupitia sera hiyo, hadi sasa benki ya NMB imefanikiwa kuchangia jumla ya madawati 31,150 na kompyuta 1150 katika jumla ya takribani shule 623.

"Kwa mantiki hiyo, tunapokaa chini kuangalia namna tulivyofanikiwa, tunajisikia furaha tunapogundua kwamba zaidi ya wanafunzi 93,000 kote nchini, wanakaa kwenye madawati yaliyotolewa na benki yao pendwa," anasema Ruth Zaipuna, Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa NMB na kuongeza.

"Pia tumechangia maktaba, tumejenga vyoo na majiko kwa baadhi ya shule kupitia Mpango Maalum wa Wafanyakazi Kuwajibika kwa Jamii (CSR Staff Initiative Program)."

Wakati mamlaka zikijikita katika ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kubeba idadi ya wanafunzi na kusoma, NMB kama mshirika mtiifu, ikitoa vifaa na kufanya uezekaji katika taasisi za umma zaidi ya 369.

"Kama ilivyoainishwa katika sera yetu ya CSR, tunahitaji kuwa na wanafunzi na wafanyakazi wenye afya ili kwa pamoja wawe na mchango katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa la Tanzania," anasema Zaipuna na kuongeza:

"Hii ndio sababu katika miaka mitano iliyopita, tumejikita katika kutoa vifaa tiba na vifaa vya hospitali kwa zahanati na vituo vya afya zaidi ya 333 kote nchini."

Kama ilivyo katika elimu, michango ya benki hii katika sekta ya afya ni vifaa kama vya uchunguzi, vitanda vya kulaza wagonjwa, vitanda vya kujifungulia wajawazito na vifaa vya ujenzi - imelenga katika kuisaidia serikali kuipa nguvu kwenye kuwezesha upatikanaji wa vifaa tiba na afya kote nchini.

Michango hii imezisaidia mamlaka kukabiliana na uwingi wa wananchi wake wanaofurika katika vituo vya afya vya umma wanaohitaji huduma za kimatibabu.

### WAATHIRIKA WA MAJANGA YA ASILI

Kwingineko, NMB daima imekuwa mstari wa mbele katika kusaidia watu ambao wamekuwa wakikumbwa na majanga ya asili kote Tanzania.

Katika hili, waathirika wa gharika la mafuriko mwaka 2016 huko Hai, Kahama na Geita, waliwezeshwa kama ilivyokuwa kwa mikoa ya Iringa na Lindi mwaka 2016.

Mwaka 2017, wakati Tanzania ilipokumbwa na janga la asili, lililowaacha maelfu ya Watanzania wakihitaji misaada, NMB iliwashika mikono wahanga, ikitumia jumla ya Sh. milioni 90 kusaidia waathirika wa mafuriko ya Kilosa, Morogoro na Cholera, Zanzibar, na janga la moto huko Mugumu-Mara.

"Kupitia yote hayo, tunajaribu kuwaambia Watanzania wote tuko hapa kwa ajili yao na tutaendelea daima kushirikiana nao katika shida na changamoto wanazopitia jamii," anasisitiza Zaipuna, huku akiahidi kwamba benki yake itaendeleza hilo.

### WANUFAIKA

Baadhi ya wanufaika wa misaada ya NMB kupitia CSR, wanakiri kuwa misaada ya benki hiyo imekuwa na athari chanya katika shughuli zao za kila siku.

"Kabla ya NMB kuja hapa na kutusaidia madawati 174, nusu ya wanafunzi katika shule yetu walikuwa wakikaa sakafuni...kwa mantiki hiyo, unaweza kuona nini maana ya misaada hii kwetu," anasema Mkuu wa Shule ya Sekondari Walla, iliyoko wilayani Kwimba, mkoani Mwanza, Neema Kitiku.

Kwa mujibu wa Kitiku, madawati 174 yaliyotolewa na NMB, yamewezesha asilimia 80 ya wanafunzi wa shule yake kusoma wakiwa wamekaa madawatini.

Shule ya Msingi Mitindo, iliyopo wilayani Misungwi, mkoani Mwanza, ni miongoni mwa shule 623 nchini ambazo zimenufaika na misaada ya madawati NMB.

Ingawa uhaba wa madawati shuleni ungalipo, lakini 63 ambayo yamechangiwa na NMB yamefanikiwa kupunguza changamoto hiyo, kama anavyokiri Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Joyce Mangi:

"Madawati hayo 63, yametuwezesha kumaliza tatizo la kusoma wakiwa sakafuni kwa wanafunzi zaidi ya 200.

"Tunaishukuru NMB kwa kutusaidia kiasi chake... Tunapenda kutoa wito kwa jamii wanapaswa kujenga utamaduni chanya wa kujitoa kuchangia mahitaji ya shule zinazowazunguka kama inavyofanya NMB, badala ya kuliacha jukumu hilo kwa serikali," anasisitiza Mangi.

MJADALA

NA MICHAEL ENEZA

# Kuinua ufikiri kwa mijadala bila mitaala wezeshi si rahisi

KUNA rai zimekuwa zikitolewa hivi karibuni kuhusu umuhimu wa majukwaa ya mijadala katika shule na vyuo, ili kujenga uwezo wa kufikiri, kujenga na kusimamia hoja za kitaaluma na katika masuala tofauti ya kijamii.

Si rahisi kusema msukumo huo ulitokea wapi, kutokana na hitilafu katika maeneo gani hasa, kwani ukiangalia kinachotokea katika vyombo vya habari, kuna mijadala mingi na hoja zinatolewa kila mahali.

Tatizo lipo kwenye hoja za kitaaluma kwa maana ya kuihakiki jamii, sera au mahusiano tofauti hasa mjadala ukiendeshwa kwa Kiingereza.

Suala ambalo wanaharakati wanaweza kuuliza ni kama upungufu huo jinsi ulivyo ni tatizo la uelewa wa masuala ya jamii au ni upungufu wa uwezo wa kutumia Kiingereza katika mazungumzo ya kawaida.

Na kwa maana hiyo mijadala, bila kuwa katika urasimu fulani kwa mfano mitihani au hotuba.

Kwa vile kuna usemi 'Ukipenda chongo utaita kengeza,' haitakuwa jambo la kushangaza kusikia wanaharakati wakiafiki kuwa hapo kuna tatizo la lugha na siyo la kufikiri.

Hata hivyo, wanafunzi wanatumia Kiingereza sekondari na vyuo, iweje wasiweze kufikiri kwa lugha hiyo, kama mitaala husika ina kina cha kutosha kuchangamsha fahamu zao?

Tatizo la kutokuweza kufikiri katika taaluma ina kina kirefu, na kwa kuanzia, mitihani ya shule za msingi na sekondari imekuwa ikichukua sura ya kuangalia kipi sahihi na kuweka alama, tofauti na kueleza kwa maneno na kuonyesha ufasaha wa kuelewa suala lenyewe.

Ndiyo inaitwa 'multiple choice,' kuchagua jibu kati ya majibu tofauti kadhaa, hali inayomhitaji mwanafunzi kuwa na hisia au taswira ya kinachozungumziwa na kukitambua katika yale majibu, hata kama hawezi kufafanua nini hasa kinalengwa.

Inapofikia ngazi ya vyuo, ufundishaji unakazania 'dictation,' kutoa neno hadi neno liandikwe na wanafunzi, wasome kwa kukariri, ili wafaulu.

Bado yako maeneo ya 'coursework,' kazi anazopewa mwanafunzi kama majaribio wakati somo bado linaendelea kufundishwa na mitihani ya mwisho bado, na hapo inawezekana vyuo na hata walimu tofauti kuweka mifumo au aina za majaribio wanayopendelea.

Rahisi zaidi ni zile zile 'multiple choice,' au kujaza nafasi iliyowekwa, au insha fupi, lakini siyo rahisi kufikiria ni kwa kiwango gani bado wanafunzi wanatakiwa wajieleze kwa kina kuhusu masuala fulani yenye uhusiano wa karibu na somo husika. Ila ni wazi katika mitihani kamili hilo halikwepeki vyuoni.



Midahalo ni miongoni mwa hatua nzuri kwa wanafunzi kama hawa kujenga uwezo wao wa kuchanganua mambo, lakini iambatane na mitaala stahiki. **PICHA: MTANDAO.**

Ni wazi kuwa katika mazingira kama hayo suala la kujieleza kwa ufasaha kiasi fulani ili kufaulu linakuwa la nadra na siyo jambo la kawaida kwa mwanafunzi au mtahiniwa, na hata hivyo hitaji hilo bado liko katika somo la aina moja tu.

Inapokuja suala la kuchanganya mitaala, yaani kutoa majibu ya vitu vinavyoingia katika mitaala tofauti hapo linakuwa jambo lingine. Kutokuwepo aina fulani za mitaala ambazo ni jumuishi, zinazolenga vianzio vya mitaala kwa jumla hasa kwa upande wa masuala ya kijamii ni tatizo, ambalo limetatuliwa kwa njia mojawapo au tuseme ya kiitikadi katika jadi ya elimu hapa nchini. Siyo ajabu mtaala huo jumuishi ni sehemu ya tatizo.

Katika kipindi kilichofuatia uhuru, mitaala ya shule ilibadilishwa hapa na pale kuondoa vielelezo vya wazi vya utawala wa 'kikoloni; na utii kwa Malkia wa Uingereza, mitaala hiyo kimsingi ikiwa imeungana na mingine ya nchi za "Afrika Mashariki baada ya Uganda na Kenya kupata uhuru.

Tofauti iliingia mwaka 1967 wakati mivutano katika masuala ya sera za nje (kuvunja uhusiano na Ujerumani Magharibi halafu Uingereza kwa masuala yaliyowahusu kwa karibu na wakiwa kinyume chetu), halafu kupinduliwa Rais Kwame Nkrumah wa Ghana, halafu kukawa na maandamano ya wanafunzi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kulimweka Rais (Julius) Nyerere njia panda.

Ilibidi achukue tahadhari kiitikadi aondoe njia kuu za uchumi mikononi mwa wageni.

Suala hilo bado halijagunduliwa na wasomi nchini, wala huwezi kulisikia katika majadiliano kuhusu Azimio la Arusha, kwani mabadiliko yaliyoletwa na azimio, ikiwa ni pamoja na kutafuta mwelekeo mpya wa elimu, yalipindua itikadi ya kizalendo na kupambana na wageni (ubeberu) ikawa ndiyo ufahamu halisi wa mwanafunzi kuhusu nchi.

Hapakuwa na mijadala ya jadi ya 'for and against,' wanaounga mkono na wanaopinga, ila kwa kila swali kulikuwa na jawabu la kiitikadi ambalo lingejionyesha dhahiri. Mijadala inakuwa hasa ni kufafanua jawabu hilo, basi.

> "Tanzania ilikuwa na hitilafu kwa upande huo kwani falsafa iliondolewa kabisa labda katika seminari, na ufundishaji wa historia na fasihi baadaye ukawa unaishia na Afrika, si Ulaya, dunia.

Kwa mtu anayefahamu mazingira ya kitaaluma ya nchi tofauti, unachoweza kusema ni kuwa mijadala inayohusisha watu wengi ni lazima iwe imejichimbia katika utamaduni au upana wa ufahamu wa watu kwa jumla.

Nchi za Ulaya kwa mfano zimejengwa katika utamaduni wa elimu uliojengwa kwa karne kadhaa kuanzia mageuzi katika dini na uamsho wa kutambua ubora au umuhimu wa uelewa wa dunia, jamii au upenyo wa kumfahamu binadamu ulioanzia katika kale ya Wayunani, miaka takriban 300 kabla ya Kristo.

Maeneo hayo ya masomo ambayo kwa jumla yanafahamika kama Hellenism, yaani elimu ya Uyunani, fikra ya kipindi hicho, ndiyo msingi wa kujenga mielekeo tofauti ya fikra ambayo baadaye ilichepua fikra za kisasa, mikondo tofauti.

Baada ya uhuru, nchi nyingi za Afrika hazikuwa na uhuru wa kutosha katika medani ya siasa licha ya kubakia na mitaala ya kimageuzi ya Ulaya katika masomo kama fasihi na historia, wakati falsafa (philosophia) ilifundishwa kwa uchache zaidi.

Ni mtaala huo wa tafsiri tofauti za uwepo wa dunia, hulka za binadamu na hata maana halisi ya mantiki, yaani kufikiri kwa usahihi ambayo inajenga uwezo halisi wa kufikiri, kwa kujua 'njia' za kutumia ili kutanzua suala hili au lile.

Tanzania ilikuwa na hitilafu kwa upande huo kwani falsafa iliondolewa kabisa labda katika seminari, na ufundishaji wa historia na fasihi baadaye ukawa unaishia na Afrika, si Ulaya, dunia.

Hata hivyo njia muhimu zaidi ya kujenga uwezo wa kufikiri ni uelewa wa kilichotokea na sababu zake, hivyo licha ya kufuta mielekeo tofauti ya fikra kuhusu jamii, kukwama kwa Ujamaa na kuhangaika ni itikadi gani inafaa tayari imejijenga katika ufahamu wa watu.

Katika wakati huu, kilichokuwa kimezoeleka kama utawala wa kidemokrasia wa vyama vingi ambao pia unapambana na umaskini na hata ufisadi ulifumuliwa kwa kina, taswira mpya ikaanza kujengwa.

Katika mpangilio huo, harakati ya kuhakikisha serikali inatumikia wananchi, ikiwa kwa upande fulani inazozana na itikadi ya demokrasia, ni changamoto inayojenga uwezo wa kufikiri, kwani inamlazimisha kila mmoja tu achukue msimamo kuhusu kinachojadiliwa.

Siyo suala la kulishwa masomo shuleni na kuyarudia katika mtihani, ila kufaulu mtihani wa maisha.



WADAU
SABATO KASIKA

# Sauti za wadau

MWAKA 2019 upo ukingoni, na kuna mengi yamefanyika kwenye sekta ya elimu kipindi chote cha miezi 12. Nini kipewe kipaumbele kwa mwaka ujao? Wadau wanajadili.



**ZAINAB SALUM (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

NI kweli kuna mengi yamefanyika kwenye sekta ya elimu ikiwamo kutoa elimu bure kwa shule za msingi hadi kidato cha nne.

Watoto wengi wamepelekwa shule, ili kupata elimu, ingawa bado kuna tatizo kwenye shule za sekondari, ambalo ningeshauri litafutiwe ufumbuzi wa kudumu.

Nalo ni ukosefu wa maabara katika shule nyingi za serikali, hali ambayo inakwamisha wanafunzi kujifunza masomo ya sayansi kwa vitendo.

Unakuta wanafunzi wanaosoma katika baadhi ya shule za kata, hawajui chochote kuhusu maabara. Sasa kwa mazingira hayo wataalamu wa baadaye watatoka wapi?

Unaweza kukuta shule ina jengo kwa ajili ya maabara, lakini maabara zenyewe hazipo, au shule ina maabara lakini jengo halipo na wakati mwingine vyote vipo lakini hakuna mtaalamu wa maabara.

Haya yote ni matatizo ambayo ningeshauri mwaka ujao yatafutiwe ufumbuzi wa kudumu ili wanafunzi wasome kwa vitendo kuliko nadharia tu kana kwamba hakuna uwezekano wa shule kuwa na maabara.

Kama kuna tatizo kubwa linalokwamisha shule kuwa na maabara zinazofanya kazi, basi wananchi tujulishwe, ili kama ikiwezekana tushirikishwe kumaliza tatizo hili ambalo kimsingi halipaswi kuwapo kwenye karne hii ya sayansi na teknolojia.

Mwaka 2020 uwe wa kuhakikisha shule zote za sekondari zinakuwa na maabara zinazofanya kazi na siyo mapambo tu, kwani baadhi ya shule zina maabara lakini zimehifadhiwa tu kwa ukosefu wa jengo husika.



**RAMSON MAKONGORO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

MIMBA kwa wanafunzi limekuwa ni tatizo kubwa kwa mwaka huu unaomalizika. Tumesikia taarifa mbalimbali kwa vyombo vya habari zikielezea jinsi wanafunzi walivyokatisha masomo kwa sababu ya mimba.

Hivyo mimi ningeomba mwaka ujao uwe wa kuongeza nguvu katika vita dhidi ya mimba kwa wanafunzi, kutokana na ukweli kwamba zinakatisha ndoto zao.

Kwa mfano taarifa iliyotolewa hivi karibuni na mkuu wa mkoa wa Lindi, zinaonyesha kuwa wanafunzi 150 wamepata mimba katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Novemba mwaka huu.

Sasa kwa hali kama hii ni muhimu kuongeza kasi ya kutokomeza mimba hizo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu rika na hata kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaohusika na kukatisha wanafunzi kuendelea na masomo kwa sababu ya mimba.

Mtoto wa kike ana haki ya kusoma kama ilivyo kwa wa kiume, sasa wanapotokea watu wa kuwakatisha masomo, basi hao ni wa kushughulika nao, ili kukomesha tabia hiyo.

Mwaka unaokuja uwe ni wa kutafakari ni wapi tumekwama na kuweka mikakati mipya ya kuhakikisha tatizo la mimba kwa wanafunzi linakoma. Kimsingi hili ni tatizo sugu kwa wanafunzi ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Ndiyo maana nikasema, mwaka ujao uwe na mikakati ya kuhakikisha tatizo hilo linakoma ili wanafunzi wa kike wasome bila usumbufu na hatimaye watimize ndoto zao walizonazo kwenye elimu kuliko kuishia njiani.



**RAFIKI WILLISON (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KIMSINGI sekta ya elimu inakabiliwa na matatizo mengi sana ambayo yanahitaji kutatuliwa kwa ushirikiano na wadau wote wa elimu.

Baadhi ya shule zina walimu wachache, madawati machache, vyumba vya madarasa vichache, vifaa vya kujifunzia na kufundishia vichache na mengine mengi.

Kwa maoni yangu sekta ya elimu bado haijatulia ingawa kuna juhudi kubwa zimefanywa na serikali kwa ajili ya kukwamua elimu nchini.

Karne hii ya 21 ni ya kufanya mambo makubwa kwenye elimu, yaani kufanya mapinduzi yanayoweza kusaidia elimu yetu kuwa bora, kwa maana ya kutoa wataalam wa fani mbalimbali.

Tunapoanza mwaka 2020, serikali iwekeze zaidi kwenye elimu ili kupunguza matatizo yanayozikabili shule za msingi, sekondari na hata vyuo, vinginevyo tutaendelea kushindwa na mambo ambayo wakati mwingine yako ndani ya uwezo wetu.

Kwa mfano tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa na madawati, wazazi na walezi wanaweza kushirikishwa wakachangia kumaliza tatizo hilo, hasa kutokana na ukweli kwamba shule za umma ni mali yao, wana wajibu wa kuhakikisha wanashiriki kikamilifu kumaliza matatizo yanayozikabili shule hizo bila kusukumwa.

Mwaka 2020 tuwe mstari wa mbele kusaidia kupunguza kama siyo kumaliza kabisa matatizo yanayozikabili shule za umma.



**MICHAEL MZUNGU (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

PAMOJA na kwamba tunakwenda vizuri kwenye suala la elimu, bado kuna uhaba mkubwa wa walimu wa masomo ya sayansi katika shule mbalimbali za sekondari nchini.

Unaweza kukuta shule zina vitabu vingi vya masomo ya sayansi, lakini hakuna walimu wa masomo hayo, au unaweza kukuta hakuna walimu wala vitabu vya kutosha.

Na unaweza kukuta shule ina mwalimu mmoja wa masomo ya sayansi akifundisha masomo ya kemia na hisabati kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne. Hali kama hii inaweza kuwa inachangia wanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani. Inaumiza sana kwani kidato cha pili, wanafunzi huwa hawachagui masomo, inatakiwa wafanye yote, sasa mwisho wa siku inaonekana wanafanya vibaya, lakini ukweli ni kwamba hawakufundishwa masomo mengine.

Suala hili la shule za serikali kuwa na walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi ni la muhimu sana na linatakiwa kutiliwa mkazo. Kupeleka mwalimu mmoja katika shule ili afundishwe masomo hayo kuanzia kidato cha kwanza hadi ya cha nne ni kumuumiza mwalimu kwa kumwongezea majukumu.

Hebu serikali ifanye mapinduzi makubwa katika hili kwa mwaka unaokuja wa 2020 ili kusaidia wanafunzi kusoma masomo yote bila usumbufu, kwani mitihani inavyoandaliwa haibagui kuwa mwanafunzi hakufundishwa somo fulani hivyo asifanye mtihani wake, bali anatakiwa kufanya masomo yote hata yake ambayo hakufundishwa, na matokeo yake ni kufanya vibaya.



**PANDAGOYA NEVELE (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KWA mtazamo wangu ni kwamba, kabla ya kuendelea na uboreshaji wa miundombinu kama ujenzi wa vyumba vya madarasa, madawati na vingine, mwaka ujao serikali iwekeze zaidi kwa walimu, ambao kimsingi ndio roho ya elimu shuleni. Ihakikishe shule zote hasa zile za pembezoni zinakuwa na walimu kwa idadi sawa na wenzao wa mijini.

kumekuwapo na tatizo kubwa la uhaba wa walimu katika shule za vijijini, huku wakiwa wamerundikana katika shule za mijini, kana kwamba watoto wa vijijini hawana haki ya kupata elimu. Ikumbukwe kuwa elimu ni nguzo muhimu ya mafanikio kwa mtu binafsi na hata kwa maendeleo ya taifa lolote.

Ni njia rahisi ya kuondokana na ujinga kupitia elimu inayotolewa au katika taasisi za elimu ama katika mazingira mengine yasiyo rasmi. Lakini suala la msingi hapa ni kuwa na walimu wa kutosha kwenye shule za vijijini kama ilivyo mijini, ili watoto wote wapate elimu inayolingana, kwa maana ya kusoma masomo yote shuleni.

Kama kuna tatizo katika shule za vijijini, basi litatuliwe ili walimu wasiwe wanazikimbia, kwa sababu baadhi yao wanaopangiwa huko wamekuwa wakiomba uhamisho hasa wa kwenda mijini na maeneo mengine yenye ahueni.

Kutokuwa na uwiano wa idadi ya walimu wa mjini na vijijini ni tatizo kwenye maendeleo ya elimu. Tatizo hili litazamwe kwa mapana yake na kupatiwa ufumbuzi katika mwaka wote wa 2020.



HABARI MBEYA

## DC amwaga vifaa Jumuiya ya Wazazi

Na Nebart Msokwa, MBEYA

MJUMBE wa Baraza Kuu la Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Maryprisca Mahundi, ameanza kutekeleza ahadi yake ya kuiwezesha Jumuiya za Wazazi katika wilaya zote za Mkoa wa Mbeya kwa kugawa vifaa.

Mahundi ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Chunya, amegawa kompyuta moja na mashine ya kudurufu maandishi kwa jumuiya hizo katika Wilaya za Mbeya Mjini, Kyela, Rungwe na Mbarali.

Alikabidhi vifaa hivyo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara yake katika wilaya hizo ikiwa ni miongoni mwa mikakati yake ya kukiimarisha chama hicho, ambapo alisema ataendelea kugawa kwa wilaya mbili zilizobakia za Chunya na Mbeya Vijijini.

Alisema vifaa hivyo alivyogawa vinagharimu Sh. 4,000,000, na kwamba mpaka atakapokamilisha wilaya zote atakuwa amegawa vifaa vyenye thamani ya Sh. 6,000,000.

Alisema lengo la kugawa vifaa hivyo ni kuziwezesha jumuiya hizo kutekeleza majukumu kwa ufasaha bila kukwama kwa sababu za kukosa vifaa.

"Hizi jumuiya ni muhimu sana kwa maendeleo ya chama, hivyo naendelea na utekelezaji wa ahadi yangu kwenu ili kila jumuiya iwe imara, na watu wa kuziimarisha ni sisi wenyewe," alisema Mahundi.

Aliwataka viongozi wa jumuiya hizo kuvitunza vizuri vifaa hivyo ili vidumu kwa muda mrefu na visaidie katika shughuli hizo za chama ambazo zimekuwa zikikwama.

# Wafugaji wakaidi watangaziwa kiama

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewatangazia kiama kipya wafugaji wanaochungia mifugo kwenye mazao ya wakulima kwa makusudi kuwa ataanzisha utaratibu wa mifugo hiyo kuchinjwa na nyama kugawanywa kwenye shule kwa ajili ya wanafunzi.

Chalamila alitangaza kiama hicho mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa katika kata za Kambikatoto na Mafyeko wilayani Chunya kwa ajili ya kukagua mipaka ya Msitu wa Kambikatoto unaokusudiwa kuhifadhiwa na serikali kupitia Wakala wa Huduma za Misitu (TFS).

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Mafyeko baadhi ya wakulima walilalamika kuwa kuna mmoja wa wafugaji amekuwa akichungia mifugo kwenye mazao yao na wakimuuliza anawacharaza bakora.

Salala Shega, alisema wakulima wengi wameumizwa na mfugaji huyo na kwamba amekuwa akijivunia utajiri alionao kuwa hata wakimshtaki hatafungwa yeye bali zitafungwa fedha zake.

Alisema wakulima wa eneo hilo hawana raha kutokana na mfugaji huyo ambaye amekuwa akishirikiana na vijana wake kufanya unyama huo dhidi yao.

Baada ya maelezo ya mkulima huyo pamoja na wenzake, Chalamila aliliagiza Jeshi la Polisi kumkamata mfugaji huyo mara moja na kumsweka ndani kisha hatua za kumfikisha mahakamani zifuatwe.

Alisema mkulima huyo ni miongoni mwa watu wachache ambao wanaendeleza migogoro na wakulima isiyokuwa na ulazima, na kwamba lugha anayotumia inaashiria kuwa kuna baadhi ya viongozi wanaweza wakawa wanapokea rushwa.

Aliwataka wafugaji hao kuacha tabia hizo kwa maelezo kuwa wao na wakulima wanategemeana katika maisha kwa vile wakulima wanahitaji nyama na maziwa kutoka kwao na wao wanahitaji chakula kutoka kwa wakulima.

Alisisitiza vitendo hivyo vya kuingiza mifugo kwa makusudi kwenye mazao kikiendelea ataanza kutekeleza utaratibu wa mifugo hiyo kutaifishwa na kuchinjwa kwa ajili ya wanafunzi wa shule mbalimbali mkoani humo.

"Kwenye hili sitanii, mimi huwa natoa onyo mara ya kwanza, mara ya pili na ya tatu kisha naanza utekelezaji... sasa nikichinja ng'ombe wenu 10 ndipo mtajua kuwa sitanii," alisema Chalamila.

Baada ya maagizo hayo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema mfugaji huyo amekamatwa na yupo katika kituo kidogo cha polisi tayari kwa kusafirishwa kwenda Chunya Mjini.

Alisema lugha anazotumia mfugaji huyo kwa wenzake zinalichafua Jeshi la Polisi na serikali kwa kuhisiwa kuwa kuna viashiria vya rushwa miongoni mwa watendaji wa serikali na polisi.

Alisema mtu huyo atafikishwa mahakamani na baada ya kesi yake kuisha atafute eneo lingine nje ya Mkoa wa Mbeya la kwenda kufanyia shughuli zake za ufugaji.



Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Maryprisca Mahundi (kulia), akinunua maembe kwa wajasiriamali wa Kata ya Kandete katika Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, alipokuwa kwenye ziara ya kuimarisha Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mradi kuwanufaisha wakulima 10,000

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

ZAIDI ya wakulima 10,000 wa mpunga wa vijiji 26 vya Wilaya ya Kyela na Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe, wanatarajiwa kunufaika na Mradi wa Kilimo Trust unaoendeshwa na kiwanda cha kusindika mpunga cha Kyela Rice.

Kiwanda hicho kwa kushirikiana na wataalamu wa kilimo kinaandaa mashamba darasa kwa ajili ya kuwaelimisha wakulima namna bora za kuzalisha zao hilo ili kuongeza uzalishaji na kuimarisha soko la zao hilo ndani na nje ya nchi.

Akizungumza na wakulima juzi wakati wa uzinduzi wa mradi huo, msimamizi wa Kilimo Trust, Thobias Mwankonda, alisema mradi huo unalenga kutoa elimu ya kilimo bora cha mpunga kupitia mashamba darasa 50 ambayo yataanzishwa kwenye vijiji.

"Mradi huu wa Kilimo Trust umeanzishwa na kiwanda chetu kwa kushirikiana na taasisi ya Agra kwa lengo la kumuinua mkulima mdogo wa zao la mpunga, tunataka watu walime kilimo chenye tija," alisema Mwamkonda.

Alisema wanataka kuwaondoa wakulima kwenye kilimo cha mazoea ambacho tija yake ni ndogo hasa katika kipindi hiki ambacho serikali ya awamu ya tano inasisitiza kuingia kwenye uchumi wa kati unaoambatana na mapinduzi ya viwanda.

Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Moses Mwaipopo, alisema wamefikia hatua hiyo ya kumwinua mkulima mdogo kutokana na uhitaji mkubwa wa soko la mchele unaotoka Kyela ndani na nje ya nchi.

Alisema kila sehemu kwenye masoko ya mpunga inaonyesha mchele kutoka Kyela ndio wenye soko zuri kuliko unaozalishwa katika maeneo mengine, lakini kiwango cha uzalishaji bado hakikidhi mahitaji hayo ya soko.

"Mchele wa Kyela umekuwa na soko kubwa katika nchi za ukanda wa SADC, hivyo tumeona ni bora tuwajengee uwezo wakulima wadogo kulima kilimo cha kisasa na chenye tija maana wengi wao wamekuwa wakilima kilimo cha mazoea," alisema Mwaipopo.

Alisema endapo wakulima hao watazingatia kanuni wanazofundishwa watakuwa na uwezo wa kuvuna gunia 18 za mpunga kwenye ekari moja tofauti na sasa ambapo wanazalisha gunia tisa pekee.

Mwaipopo alisema matarajio yao ni kufikia mwaka 2021 wakulima katika halmashauri za Kyela na Busokelo watakuwa na uwezo wa kusindika mchele bora kwa zaidi ya asilimia 50.

"Uzalishaji wa mpunga Kyela kwa miaka ya hivi karibuni umeyumba kidogo kutokana na wakulima kutegemea kilimo cha msimu, ambapo msimu uliopita uzalishaji ulikuwa tani 68,000 tofauti na miaka mingine ambayo uzalishaji unakuwa kati ya tani 80,000 na 90,000," alisema Mwaipopo.

Nao baadhi ya wakulima walisema mradi huo utawasaidia kuinua kiwango cha uzalishaji kutokana na mbinu wanazofundishwa na wataalamu hao.

Mmoja wa wakulima hao, Gwamaka Andongwisye, kutoka katika Halmashauri ya Busokelo, alisema elimu hiyo itawasaidia kufahamu mifumo mbalimbali ya uzalishaji ikiwamo matumizi ya pembejeo.

Alisema wakulima wengi wamekuwa wakitamani kulima kilimo cha kisasa, lakini wanakwama kwenye matumizi sahihi ya pembejeo na viuatilifu.

Alisema mradi huo utakuwa mkombozi kwao kwa maelezo kuwa mbali na kuwapatia elimu ya namna ya kulima kilimo cha kisasa, pia wanaunganishwa na taasisi za fedha kwa ajili ya kupata mikopo na kiwanda hicho kinawadhamini.





## Jumuiya CCM yapewa mbinu za kiuchumi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoa wa Dodoma, Godwin Mkanwa, amemtaka mwenyekiti mpya wa Jumuiya ya Wazazi kusimamia uanzishwaji wa miradi ili jumuiya ijitegeme kiuchumi.

Mkanwa alitoa rai hiyo wakati akizungumza na wajumbe wa mkutano mkuu wa jumuiya hiyo kwa ajili ya kumchagua Mwenyekiti wa Wazazi Mkoa wa Dodoma.

Alisema katika suala la uchumi bado jumuiya hiyo mkoa haijafanya vizuri ukilinganisha na jumuiya nyingine kama za Wanawake (UWT) na Vijana (UVCCM) mkoa wa Dodoma.

Mwenyekiti huyo alisema pia jumuiya inatakiwa kuendelea kukipigania chama, kuhamasisha wazazi katika malezi, kusimamia maadili na kuhakikisha suala la elimu linapewa kipaumbele katika vikao vyao.

Awali Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM ambaye ni mlezi wa mkoa huo, Leila Ngozi, aliwataka wajumbe hao kufanya uchaguzi wa haki, na asiyechaguliwa asiwe na kinyongo bali ashirikiane na atakayechaguliwa nia ikiwa ni kukijenga chama.

Uchaguzi huo ulishirikisha wagombea watatu ambao ni Damas Mukasa, Baraka Mkunda na Christopha Mlemwa, na unafanyika ili kujaza nafasi iliyoachwa wazi na mwenyekiti aliyekuwapo, Emmanuel Mkumbo, aliyejiuzulu baada ya kupata kazi katika utumishi wa umma.

Akizungumza baada ya matokeo ya uchaguzi huo, Mwenyekiti mpya wa Jumuiya hiyo Mkoa wa Dodoma, Damas Mukasa, aliahidi kuanzisha miradi itayokuza uchumi.

Alisema deni walilompa ni kubwa na dawa ya deni siku zote ni kulipa na ili hilo liwezekane ni lazima wote washirikiane kwa pamoja katika kujenga jumuiya na chama kwa ujumla.

Awali akitangaza matokeo hayo, msimamizi wa uchaguzi, Raymond Mangwala, ambaye ni Katibu Mkuu wa UVCCM, alisema kura zilizopigwa ni 472 na hakukuwa na kura yoyote iliyoharibika.

# Viongozi watwishwa zigo la usafi mazingira

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewaagiza viongozi wa wilaya na mikoa kuhakikisha kuwa wanapofanya mikutano ya hadhara, wahamasishe usafi wa mazingira ikiwamo ujenzi wa vyoo na matumizi bora.

Waziri Ummy alitoa agizo hilo katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Usafi wa Mazingira ulioenda sambamba na mkutano wa maofisa afya wa mikoa, halmashauri na wadau mbalimbali.

Maadhimisho hayo yamebeba kauli mbiu isemayo 'Huduma Bora ya Afya Mazingira na Usafi ni Kichocheo Muhimu cha Uchumi Endelevu'.

Alisema kama kwenye mikutano ya hadhara maofisa afya wakihamasisha usafi wa mazingira ikiwamo ujenzi na matumizi ya vyoo bora, jamii itakuwa na afya bora pamoja na kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Alisema serikali imedhamiria kuwekeza kwenye afya, hivyo wao wanapaswa kutumia ujuzi wao kuwatibu wananchi na kuwaelekeza.

Alieleza kuwa kazi ya ofisa afya ni kuhakikisha kuwa huduma za lishe zinawafikia Watanzania wa mjini na vijijini.

"Suala la afya mazingira ni suala la kipaumbele, kila kaya, kijiji kinatakiwa kuwa na ofisa afya tena bora," alisema Waziri Ummy.

"Mimi sio Waziri wa Afya bali ni waziri wa magonjwa, lengo kubwa ni kuwafanya Watanzania wasipate maradhi, endapo wataugua ni wajibu wangu kuhakikisha wanapata huduma bora za matibabu."

Akitoa salamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, alisema ofisi hiyo imepewa jukumu kubwa la kulinda mazingira kwani usafi wa mazingira kwao ni neno pana.

"Nawaagiza maofisa afya kuwa na ushirikiano, lengo ni kuhakikisha mazingira yanakuwa katika hali ya ubora hasa katika suala zima la afya," alisema Sima.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainabu Chaula, alisema baada ya mafanikio makubwa ambayo yameletwa na maofisa afya ni pamoja na kusimamia suala la chanjo na kufanikiwa kutokomeza ugonjwa wa ndui na polio, huku akigusia kwa upande wa awamu ya pili ya utekelezaji wa usafi wa mazingira kuwa wamepanga kuhakikisha kuwa asilimia 75 ya nyumba zinakuwa na vyoo bora na kuondoa kaya ambazo hazina vyoo.

Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, alisema Dodoma ni salama na kila halmashauri inatakiwa kuhakikisha kuwa afya inaboreshwa.



Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dodoma, Felisiana Mboya, akizungumza na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi wa kituo cha Shime eneo la Makulu, jijini Dodoma. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# Waomba kujengewa madaraja makubwa

**Na Peter Mkwavila, MPWAPWA**

WAKAZI wa Kijiji cha Chipogoro Wilaya ya Mpwapwa, wameiomba serikali kuwajengea madaraja makubwa ili kuondokana na kero ya mafuriko wakati wa mvua.

Wamesema hali ambayo imekuwa ikisababisha hasara kubwa kila mwaka ya miundombinu, kutokana na yaliyopo kuwa na uwezo mdogo wa kupitisha maji.

Kilio hicho cha wananchi kilitolewa kwa waandishi wa habari kijijini hapo, na kusema kuwa hali hiyo pia imekuwa ikiwasababisha kubomoka kwa nyumba zao kila mwaka.

Akizungumza kijijini hapo Christophe Richard, alisema kwenye eneo ambalo limekuwa likikabiliwa na adha hiyo kuna jumla ya madaraja saba, lakini ni madogo na hayana uwezo wa kuhimili maji hayo ambayo yamekuwa yakipita kwa kasi kubwa inayosababisha kusambaa hadi maeneo ya makazi.

"Kwanza tunaipongeza na kuishukuru serikali yetu sikivu, kwa kututengenezea miundombinu ya barabara ambazo sasa zinapitika kwa wakati... ila kwa eneo hili la Chipogoro tunaiomba serikali yetu kufanya ukarabati wa kutuwekea madaraja makubwa badala ya haya yaliyopo ambayo yatakuwa na uwezo wa kupitisha maji haya," alisema Richard.

Mary Chigundwi, mmoja wa waathirika katika kijiji hicho, alisema kuwa mafuriko hayo yaliyotokea wiki hii yamewasababishia hasara kubwa ya kubomolewa nyumba zao na kusombwa kwa vyakula ambavyo walikuwa wamejiwekea akiba.


"Tunaiomba serikali yetu pamoja na mbunge wetu kutuondolea adha hii kwenye eneo hili ambalo kwa kweli madaraja yake ni madogo na hayawezi kuhimili kasi ya maji yanayopita hapa, ambayo yanatuathiri na kusababisha nyumba zetu kubomoka na kupoteza vyakula vyetu," alisema.

Naye Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Baraka Mahenge, akizungumza na waandishi alikiri kutokea kwa mafuriko hayo ambayo hutokea kwenye eneo hilo na kusababisha uharibifu wa barabara kutokana na madaraja yake kuwa ni midomo ya kupitishia maji yanayotoka sehemu mbalimbali.

"Ni kweli katika kata hii kumetokea mafuriko makubwa na kusababisha baadhi ya nyumba kubomoka ikiwamo na uharibifu wa mazingira, hata hivyo tunaishukuru serikali kwa jitihada zake za kudhibiti maji hayo," alisema.

Ofisa huyo alisema wameshachukuwa tahadhari za kwanza kwa kuweka tuta kubwa la mchanga ili maji hayo yasilete hasara kwa wananchi na mali zao.

"Eneo hili lote maji yanapita na kuingia kwenye makazi ya wananchi, lakini kwa upande wa serikali imefanya jitihada za kuweka uzio wa tuta... ila tatizo kubwa ni baadhi ya wananchi wamekuwa waharibifu wa mazingira kwa kukata miti milimali na ndiyo maana madhara yake ni haya," alisema.



# Benki kujenga shule za kisasa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

BENKI ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (Badea), imetoa Dola za Marekani milioni 13.5 kwa ajili ya ujenzi wa shule tatu za kisasa za ghorofa visiwani Unguja na Pemba.

Mkataba wa makubalinao ya utekelezaji wa mradi huo, yalitiwa saini na Waziri wa Fedha wa Zanzibar, Balozi Mohamed Ramia na mwakilishi wa benki, Khartoum Sudan Sidi Ouid Tah.

Katika makubaliano ya mkataba huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa Dola za Marekani milioni 1.5 kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa shule hizo.

Shule hizo zitajengwa katika mkoa ya Mjini Magharibi Unguja, Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba.

Akizungumza baada ya kutia saini makubaliano hayo, Balozi Ramia alisema Badea imeahidi kujenga shule tano za kisasa za ghorofa.

Alisema tayari shule mbili za ghorofa zimejengwa ikiwamo Kibuteni iliyoko Mkoa wa Kusini Unguja na Mohamed Juma Pinduwa huko Pemba ambayo ilizinduliwa mwaka jana.

Mwakilishi wa Badea, Tah, alisema wamekusudia kutekeleza ahadi zao za ujenzi wa shule tano katika Kisiwa cha Pemba ili kuimarisha sekta ya elimu.

Alisema shule mbili tayari zimejengwa huku moja ikiwa katika hatua za mwisho kukamilika na sasa wametia saini kuanza ujenzi wa shule tatu.

"Tumejipanga kutimiza ahadi yetu ya ujenzi wa shule tano za kisasa za ghorofa ambazo zitasaidia kukuza na kuimarisha sekta ya elimu Zanzibar," alitamba.

Utiaji saini wa makubaliano ya ujenzi wa shule tatu ulishuhudiwa na Balozi wa Tanzania Sudan, Silima Haji na maofisa wa Wizara ya Fedha wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.



Mbunge wa Chumbuni, Ussi Pondeza, akiwafariji wananchi wa jimbo hilo, ambao nyumba zao zimeathiriwa na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CCM wafurahia mpasuko upinzani visiwani Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimesema kimejipanga kushinda katika uchaguzi mkuu wa mwakani na hakina hofu na vyama vya upinzani kwa kuwa tayari vimeshasambaratika.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu wa Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya CCM Itikadi na Uenezi Zanzibar, Catherine Pater Nao, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu harakati za kisiasa kuelekea uchaguzi mkuu wa mwakani.

Alisema kipindi hiki ni muhimu kwa vyama vya siasa katika harakati zao ikiwa ni sehemu ya matayarisho ya uchaguzi mkuu wa mwakani.

Aliwataka wanachama wa CCM na wafuasi wao kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura, uandikishaji ukipangwa kuanza Januari 18, mwakani.

Alisema njia pekee ya kushiriki katika uchaguzi mkuu na kupata fursa ya kuwachagua viongozi wa kitaifa ni kujiandikisha katika daftari hilo.

Nao aliwataka vijana waliofikisha umri wa miaka 18 kujitokeza kujiandikisha katika daftari hilo na kutafuta kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi.

"Vijana waliofikisha umri wa miaka 18 ambao ni wafuasi wa CCM na wanachama wake, mjitokeze kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ili muwe na uhakika wa kuchagua viongozi katika uchaguzi mkuu mwakani," alihimiza. Alisema CCM haina hofu wala wasiwasi na vyama vingine vya upinzani katika uchaguzi huo, akidai vingi vimepoteza mwelekeo.

Alidai kauli zinazotolewa na Chama cha ACT-Wazalendo kwamba CCM inashirikiana na tume na wakala wa vitambulisho vya Mzanzibari kudhoofisha uandikishaji wa wapigakura kwa kuwanyima vitambulisho vya wananchi huko Pemba si za kweli.

"CCM haitishwi na vyama vya upinzani ambavyo vimepoteza dira na mwelekeo wa kisiasa, iweje CCM ikiogope chama cha ACT-Wazalendo chenye jimbo moja tu la uchaguzi Tanzania nzima?" Alitamba.

Awali, Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), Thabit Idarous Faina, aliwataka wananchi wenye sifa, kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la wapigakura kuanzia Januari 18.

Alisema uandikishaji wa wapigakura wapya utakwenda sambamba na uhakiki wa wapigakura walioko katika daftari hilo.

Aliwataka vyama vya siasa kufanya siasa za kistaarabu na kuwahimiza wanachama na wafuasi wao kujitokeza kujiandikisha badala ya kujenga mazingira ya chuki na uhasama.

"Hii ni fursa muhimu kwa wananchi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ambapo vyama tunaviomba kutoa ushirikiano kuhakikisha zoezi hili linafanikiwa na siyo kuwajengea wananchi mazingira ya chuki na uhasama," alishauri.

# MSD kununua dawa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeingia makubaliano na Bohari ya Dawa (MSD) ili kuimarisha huduma za afya visiwani humo.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed, alisema ni busara zaidi kutumia huduma za dawa zinazopatikana Tanzania Bara katika uimarishaji uhusiano wa kindugu uliopo.

Alisema ushirikiano wa Wizara ya Afya ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na ile ya Muungano kupitia taasisi zake, umeimarika kwa kiwango kikubwa.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea na mikakati yake kuhakikisha inatoa huduma za matibabu ikiwamo dawa bure ambayo ni ahadi ya kiongozi na mwasisi wa Mapinduzi, Hayati Abeid Amani Karume.

"Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni matibabu bure na ndiyo maana serikali imetenga bajeti kubwa ya dawa kwa wananchi wake," alisema.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk.Jamala Talib, alisema wamefurahishwa na kuridhishwa na uhusiano wao na Wizara ya Afya ya Muungano pamoja na taasisi zake ikiwamo Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Alisema wamekuwa wakipeleka wagonjwa Muhimbili na uhusiano huo umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kusafirisha wagonjwa nje ya nchi.

Alisema makubaliano ya kupata huduma za dawa MSD yatasaidia kupata huduma hizo kwa wakati na Zanzibar kuacha kuagiza dawa nje ya nchi.

"Ushirikiano huu ni muhimu sana, tunaamini utasaidia kuimarisha utoaji wa huduma za dawa kwa wananchi wetu bila ya matatizo," alisifu.

Awali mwakilishi wa Kanda ya Dar es Salaam wa MSD, Celestine Haule, alisema watahakikisha wanatimiza azma ya kuimarisha huduma hizo kwa ufanisi.

"Tunaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutumia huduma zetu na sisi tunaahidi kufanya kazi kwa ufanisi na kuyafikia malengo," aliahidi.

**"Sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni matibabu bure na ndiyo maana serikali imetenga bajeti kubwa ya dawa kwa wananchi wake," alisema.**

# TCAA yafungia viwanja vidogo vya ndege 200

Na Gaudensia Mngumi

SERIKALI imevifungia viwanja vidogo vya ndege 208 kutokana na kutotimiza masharti na kanuni za usafiri wa anga ikiwamo kusajiliwa na kupata leseni za uendeshaji, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Hamza Johari, alitangaza jana.

TCAA inadhibiti na kusimamia huduma za usafiri wa anga kuanzia usalama, wataalamu, mafunzo na viwanja vya ndege miundombinu na ujenzi, kwa mujibu wa mkurugenzi huyo.

Akizungumza na wanahabari Dar es Salaam, alisema hatua hiyo inakuja baada ya TCAA kufanya ukaguzi mapema mwaka huu na kutoa muda kuanzia Mei 6 , 2019 hadi Desemba 31 , 2019 kwa wamiliki na waendeshaji wote wa viwanja hivyo kuvisajili na kupata leseni za uendeshaji.

Aidha, alisema viwanja vyote 208 havina usajili, leseni, havitumika na baada ya TCAA kutoa tangazo wamiliki na waendeshaji hawakujitokeza, hivyo vyote vimefungwa kwa kushindwa kufuata kanuni ya 323 na nyingine na matakwa ya kisheria yanayosimamia taratibu na sheria za usafiri wa anga.

Kadhalika, Johari alisema TCAA imewaongezea muda hadi Machi 31, 2020 wamiliki wa viwanja vingine 121 walioitikia wito wa tangazo la serikali la kuwataka waendeshaji wa viwanja vya ndege kujitokeza kusajili na kupata leseni za kufanya kazi hiyo.

"Mamlaka inawapongeza waliotikia wito huo na imepokea maombi ya kuongeza muda ili kuwapa fursa ya kukamilisha usajili na kupata leseni za uendeshaji," alisema Mkurugenzi Mkuu. Alifafanua kuwa Tanzania ina viwanja vya ndege 643 ambavyo ni vya kimataifa, vikubwa, vya ukubwa wa kati na vidogo kwa hiyo baada ya kufungia hivyo 208 daftari la usajili linabakiwa na viwanja 438.

Aidha, alisema waliopewa muda wa kufanya usajili ili kutimiza masharti ni wamiliki 121.

Viwanja vilivyofungwa viko karibu Tanzania nzima vikiwamo Olduvai, Idodoma, Chimala, Bweni Mafia, Iseke na Kibaoni kilichoko Morogoro.

Mkaguzi Mkuu wa Viwanja vya Ndege Tanzania, Bernard Kavishe, akifafanua zaidi alisema viwanja vidogo ni vile vya vumbi visivyo na lami, vinavyobeba mzigo wa tani sita na kwamba vilivyofungiwa vingi vipo maporini.

Alisema wamiliki wa viwanja hivyo vilivyofungiwa ni pamoja na serikali, Mamlaka ya Wanyama Pori (TAWA) Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), hospitali, watafiti mbalimbali wakiwamo wa madini, kampuni za huduma za kitalii na watu binafsi.

Akizungumzia usajili alisema pamoja na gharama nyingine na tozo za serikali leseni ya kuendesha viwanja vidogo ni takribani Sh. milioni 1.5 na hutumiwa kwa miaka miwili. Alisema leseni ya kiwanja cha kimataifa ni Sh. milioni saba wakati vikubwa ni takribani milioni nne.

# Waomba msaada udhibiti athari za zebaki

Na Paul Mabeja, DODOMA

WAGANGA wa jadi wameiomba serikali kupitia Wakala wa Misitu (TFS) kuipima miti ambayo wamekuwa wakiichimba kwa ajili ya dawa kutokana na baadhi kuwa na zebaki.

Kemikali ya zebaki inaweza kuwaathiri watumiaji kiafya.

Hayo yalielezwa na mganga wa tiba za jadi kutoka Kijiji cha Kagongwa wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Mbeshi Kisambale, alipokuwa akizungumza na wanahabari.

Alisema kuna haja kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia TFS kuipima miti ambayo wamekuwa wakiichimba kama dawa kutokana na baadhi kuwa na kemikali ya zebaki ambayo inaathari mwili wa binadamu.

Alisema kutokana na Kanda ya Ziwa kuwa na madini mengi, wakati mwingine madini hayo huenda katika mizizi ya miti hivyo wakichimba na kuwapatia watu wenye matatizo mbalimbali, mtumiaji anapata madhara makubwa.

"Tutumie nafasi hii kuiomba serikali kupanga miti ya kuchimba pamoja na kuipima miti ambayo tunaichimba... kule kwetu kuna madini mengi, hivyo yanaingia katika mizizi na kuwa na athari kubwa kwa watumiaji," alisema.

Katika hatua nyingine, aliwasihi baadhi ya waganga kuwa wakweli katika tiba zao kwani kuna baadhi wamekuwa wakiweka matangazo ya uongo kwamba wanatibu kitu fulani wakati sio kweli.

**"Tutumie nafasi hii kuiomba serikali kupanga miti ya kuchimba pamoja na kuipima miti ambayo tunaichimba... kule kwetu kuna madini mengi, hivyo yanaingia katika mizizi na kuwa na athari kubwa kwa watumiaji," alisema.**



Wakazi wa kijiji cha Kamuguruki, Kata ya Nyakatende Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, wakiandaa shamba kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe (plau), ambalo linaendelea kutumika kwenye baadhi ya maeneo nchini. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Onyo matumizi mabaya fedha za majimbo

Na Mwandishi Wetu, PEMBA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, amezitaka kamati za mifuko ya maendeleo ya majimbo kuwa makini na waache kuzichezea fedha za mfuko wa Jimbo wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwani ni hatari kwao.

Alisema si jambo jema kuzichezea fedha hizo kwani ni tofauti na fedha za mfuko wa jimbo, hivyo ipo haja ya kuisoma na kuielewa sheria, ili iwasaidie katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Akizungumza katika majumuisho baada ya kumaliza kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na mifuko ya jimbo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba, Simbachawene aliitaka kamati hiyo kuwa makini na kuepuka kuja kupata nongwa ya kutokujua.

"Kwa upande wa Zanzibar tatizo kubwa ni kushindwa kulinganisha Baraza la Wawakilishi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, fedha hizi ni za hatari musizichezee, muwe makini munapotaka kutekeleza miradi," alisema Simbachawene.

Alisema fedha hizo zinapotoka hazina hupelekwa moja kwa moja kwenye mabaraza ya miji, ingawa kuna shida kwenye eneo la utekelezaji wa miradi kwa matumizi ya fedha yasiyo sahihi.

"Zanzibar kuna maeneo mengine yaliyotekelezwa miradi hiyo yapo vizuri, lakini baadhi ya maeneo ni mabaya sana, hivyo tujitahidi fedha kuzitumia kwa mambo yaliyokusudiwa," alieleza.

Waziri huyo aliupongeza mradi wa shule ya maandalizi Kangagani Wilaya ya Wete, mradi wa shule ya Vikunguni na mradi wa umeme Pujini Wilaya ya Chake Chake kwa kazi nzuri iliyofanyika.

Katika mradi wa majisafi na salama Wingwi Mjananza, Simbachawene alisema watatafuta wataalamu ili waangalie na kufanya utafiti ili kujua kama fedha iliyotumika inastahili au la.

Kaimu Mkurugenzi wa Muungano, Lupi Mwaikambo, alisema ni muda mwafaka wa kuangalia namna bora ya maendeleo kwa kutumia fedha zinatolewa na serikali kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi.

"Hii ni kuona kwamba wananchi wanafaidi matunda ya Serikali, hivyo kutokana na changamoto hizo, ipo haja ya kushirikiana na kukaa pamoja na wakurugenzi wa Mabaraza ya Miji ili kutatua na kuona fedha hizo zinatumika ipasavyo," alisema.

Mbunge wa Chambani, Yusuf Salim Husein, alisema walikaa kikao cha kamati na kuidhinisha ujenzi wa barabara Ukutini-Tumbini, ingawa hadi zinaingia fedha za mwaka mwingine bado barabara hiyo haijatengenezwa.

Naye Mhasibu wa Baraza la Mji Mkoani, Omar Ali Said, alisema gharama za utengenezaji wa barabara ni kubwa, hivyo kutokana na fedha zilizopo hazitoshi.

HABARI KIMATAIFA

# Kundi la IS lajiimarisha tena Iraq

**BAGDAD,** Iraq

TAHADHARI imetolewa kwamba kuna ongezeko la ishara kundi la Islamic State (IS) linajipanga tena nchini Iraq na wanaweza kuwa tishio mwaka 2020.

Kujiunda tena kwa kundi hilo ni baada ya miaka miwili kupoteza eneo la mwisho lililokuwa linalidhibiti nchini humo.

Wakurdi na maofisa wa ujasusi wa magharibi wameiambia BBC kwamba uwapo wa IS nchini Iraq ni uasi wa kisasa na mashambulio yao yanaongezeka.

**Tunashuhudia shughuli zikiongezeka sasa, na tunafikiri awamu ya kukijenga upya imekwisha.**

Wanamgambo hao kwa sasa wana ujuzi zaidi na ni hatari zaidi kuliko al-Qaeda kwa mujibu wa ofisa wa ngazi ya juu wa Kikurdi wa masuala ya kupambana na ugaidi Lahur Talabany.

"Wana mbinu bora zaidi, mikakati bora, na pesa zaidi," alisema.

"Wako tayari kununua magari, silaha, chakula na vifaa. Kiteknolojia wako mbele zaidi. Ni vigumu zaidi kuwamaliza," alisisitiza Talabany.

Katika ngome yake iliyopo eneo la Sulaimaniya, lililozingirwa na milima ya Jimbo la Kurdistan Kaskazini mwa Iraq, alitoa picha ya kundi hilo lililomaliza miezi 12 likijijenga baada ya kusambaratishwa.

"Tunashuhudia shughuli zikiongezeka sasa, na tunafikiri awamu ya kukijenga upya imekwisha," alisema Talabany, ambaye ni mkuu wa kikundi cha Zanyari moja ya makundi ya ujasusi ya Iraqi katika Kurdistan.

Ameongeza kwamba kuna IS mpya imejitokeza, ambayo haitaki kudhibiti eneo lolote ili kuepuka kulengwa na mashambulio. Badala yake kama ilivyokua kwa watangulizi wao al-Qaeda - wapiganaji hao wenye itikadi kali wamejificha katika milima ya Iraq ya Hamrin.

"Hiki ndio kitovu cha ISIS kwa sasa, ni eneo lenye milima mingi, na ni gumu sana kudhibitiwa na Jeshi la Iraq ingawa kuna maeneo mengi sana ya kujificha na mapango," alisema. **BBC**

## Kulala na maiti kwaongeza kasi maambukizi ya ebola DRC

**KINSHASA,** DRC

MILA na desturi wakati wa mazishi zinatajwa kuwa miongoni mwa changamoto za kupambana na ugonjwa wa ebola katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Jinsi shughuli za mazishi zinavyofanyika DRC, kulala, kumuogesha maiti na kumvika nguo marehemu, ni baadhi ya mila zinazosababisha kuenea kwa ugonjwa huo katika maeneo ya mashariki mwa nchi hiyo ambapo zaidi ya watu 2,300 wamefariki dunia.

Ebola umekuwa ugonjwa sugu na hatari katika eneo lote la mashariki mwa DRC, licha ya chanjo pamoja na tiba zinazotolewa kutoka kwa madaktari, lakini jitihada za kuutokomeza hazijafanikiwa.

Daktari Christoph Shako, mmoja wa viongozi katika kamati ya kupambana na ebola mkoani Ituri, anaamini kuwa ni mila potofu ndiyo kizingiti.

Jamii nyingi ya watu wa maeneo ya Beni wamekuwa na mitizamo hasi kuhusu ebola, wengi huamini ugonjwa wa kawaida huo uliletwa kwa manufaa ya watu kujilimbikizia fedha.

Madaktari wanaopambana na ebola nchini humo wameeleza wanakijiji waliopoteza jamaa zao kuwa hawawezi kuwazika kwa utaratibu wa kitamaduni.

Tamaduni zimekuwa zikikinzana au kugongana na maelekezo ya madaktari katika mchakato wa kupambana na ugonjwa huo.

"Baadhi wamekuwa na imani kwamba mgonjwa wa ebola anaweza kupona kwa kuombewa au kwa usaidizi wa waganga wa jadi, jambo ambalo limekuwa likichangia ongezeko la maambukizi katika baadhi ya maeneo," alisema Omar Kavota, ambaye ni mratibu wa Shirika la Cepadho mjini Goma. **BBC**



Polisi wa nchini India wakitumia fimbo kukabiliana na waandamanaji wanaopinga sheria mpya. **PICHA: REUTERS**

## Saudia yawahukumu kifo wauaji wa Jamal Khashoggi

**RIADHI,** Saudi Arabia

MAHAKAMA nchini Saudi Arabia imewahukumu adhabu ya kifo watu watano kutokana na mauaji ya mwanahabari mkosoaji wa serikali ya nchi hiyo, Jamal Khashoggi.



Khashogg (pichani) aliuawa mwaka 2018 katika jengo la ubalozi wa nchi hiyo mjini Istanbul, nchini Uturuki.

Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Saudi Arabia, amesema kwamba watu wengine watatu wamepewa vifungo vya jumla ya miaka 24.

Alisema Saud al-Qahtani, mshauri wa zamani wa ngazi ya juu wa Mwana wa Mfalme wa Saudi Arabia, alichunguzwa, lakini hakushtakiwa na akaachiwa huru. **DW**

## Nato, Urusi kukutana kuzungumzia mvutano

**BERLIN,** Ujerumani

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Kujihami ya Nato, Jens Stoltenberg, amesema yuko tayari kukutana na Rais wa Urusi, Vladmir Putin, kama mazingira yatakuwa sawa.

Stoltenberg ameliambia Shirika la Habari la Ujerumani (DPA) kuwa mazungumzo ni muhimu katika wakati huu ambapo kuna mahusiano mabaya.

Alisema Urusi ni jirani mkubwa wa Nato na ndio maana ni muhimu kuimarisha uhusiano kati yao.

Uhusiano kati ya pande hizo mbili uliharibiwa wakati Urusi ilipoinyakua rasi ya Crimea kutoka Ukraine mwaka 2014 na ikawaunga wapinagaji waliotaka kujitenga katika eneo la mashariki mwa nchi hiyo. **DW**

# Mkuu wa shule kortini tuhuma rushwa ngono

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Dodoma, imemfikisha mahakamani Mwalimu Baraka Sabi kwa tuhuma za kuomba rushwa ya ngono kwa mwanafunzi wake.

Sabi (41), Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Serengeti mkoani Mara, anadaiwa kutenda kosa hilo la kuomba rushwa hiyo ili kumpatia cheti cha kuhitimu masomo yake ya kidato cha sita.

Mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Dodoma, Paschal Mayumba, Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Clarence Kimaro, alidai mahakamani huko kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Desemba 12, mwaka huu katika Hoteli ya Pahi iliyoko jijini Dodoma.

Kimaro alidai mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Mshtakiwa alikana mashtaka yanayomkabili na yuko nje baada ya kukamilisha masharti ya dhamana yaliyomtaka kuwa na wadhamini wawili watakaotia saini bondi ya Sh. 500,000 kila mmoja na pia wawe ni wakazi wa Mkoa wa Dodoma.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Januari 10, mwakani baada ya upande wa mashtaka kudai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.



Meneja wa Tigo wa Mkoa wa Shinyanga na Simiyu, Sadock Phares, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mradi wa Tigo wa malipo ya mazao ya pamba alipowatembelea wakulima wa pamba katika kijiji cha Zanzui wilayani Maswa mkoani Simiyu. Zaidi ya wakulima 120 wamelipwa pesa zao kupitia Tigopesa kwenye msimu uliopita kiasi cha Sh. milioni 189. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Kalambo yapitisha bil. 36/- bajeti

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa imepitisha bajeti ya Sh. bilioni 36.4 katika mwaka wa bajeti 2020/2021.

Akisoma bajeti hiyo jana, katika Baraza la Madiwani lililofanyika mjini Matai, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Eric Kayombo, alisema katika bajeti hiyo halmashauri imepanga kukusanya mapato ya ndani Sh. bilioni 1.8.

Alisema Sh. bilioni 27.0 zitatumika kwa ajili ya mishahara, Sh. bilioni 5.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya matumizi mengine.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Daudi Sichone, aliwaomba madiwani wa halmashauri hiyo kwa kushirikiana na wananchi wajitahidi kujenga vyumba vya madarasa pamoja na maboma kwa ajili ya zahanati na vituo vya afya kwa kuwa serikali inatoa hela za kumalizia.

Alisema vijiji ambavyo havijishughulishi vitakosa maendeleo kwa kuwa serikali inatoa fedha kukamilisha maboma, hivyo ni lazima wananchi waanze ndipo serikali imalizie.




## 'Mafunzo usalama mitandao'

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), inabadilika kila siku hivyo kunahitaji mafunzo katika usalama wa mitandao.

Hayo yalisemwa jana Mwakilishi wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Richard Mgema, wakati akifunga shindano la wanafunzi wa vyuo vikuu nchini linalohusu usalama wa mitandao lililoandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na kampuni ya nchini Kenya.

Mgema alisema kuwa dunia iko katika mabadiliko ya Tehama, hivyo Tanzania haiwezi kuwa kisiwa cha kutoendana na teknolojia hiyo.

Alisema wanafunzi walioshiriki shindano hilo wamepitia katika mchujo na washindi watakwenda kushindana na nchi nyingine suala la ulinzi katika mitandao.

"Kama nchi kumekuwa na mabadiliko ya huduma za fedha kwenda katika mitandao, hivyo vijana wengi wanahitajika kujua mifumo ya ulinzi wa mitandao ili fedha za wananchi ziwe salama," alisema.

Pia alisema Tehama ukuaji wake ni kasi kutokana na mifumo ya kiteknolojia na kubuniwa hivyo lazima kuwapo kwa rasilmali watu ya kuendana kwa kasi katika teknolojia hizo.

Mkuu wa Kanda ya Kati wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Antonio Manyanda, alisema wakati wa usajili wa shindano hilo jumla ya wanafunzi 1,056 walishiriki na baada ya mchujo wa kwanza walipatikana na 600 na baadaye walifikia 50 wanaotoka vyuo vinane.

## Nondo aibwaga tena serikali

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Iringa imetupilia mbali rufani dhidi ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Mtandao wa Wanafunzi Vyuo Vikuu, Abdul Nondo, iliyopinga hukumu iliyompa ushindi katika kesi iliyokuwa ikimkabili.

Nondo alikuwa anakabiliwa na mashtaka ya kusambaza taarifa zenye lengo la kuleta taharuki kwa wananchi na pia kutoa taarifa za uongo katika Kituo cha Polisi Mafinga.

Nondo aliyeshtakiwa mahakamani hapo mwaka jana kwa makosa mawili ya kusambaza taarifa kupitia mtandao wa WhatsApp na kutoa taarifa ya uongo kwa mtumishi wa umma, Kopro Salimu, akidai kutekwe jijini Dar es Salaam na watu wasiojulikana waliomsafirisha na kumtelekeza mjini Mafinga, aliachiwa huru jana, baada ya rufani hiyo kushindwa kumtia hatiani.

Akisoma hukumu ya kesi hiyo ya rufani namba 10 ya mwaka 2018, Jaji wa Mahakama Kuu, Panterin Kente, alisema Upande wa Jamhuri ulikuwa na jukumu la kuthibitisha pasipo shaka kuwa mjibu rufani, Nondo alitenda makosa hayo.

Aliongeza kuwa maelezo ya shitaka linalodai kusambaza taarifa za uongo yako kinyume cha kifungu cha 14 cha Sheria ya Makosa ya Kimtandao ya Mwaka 2015 kwa kuwa sheria hiyo inazungumzia kusambaza taarifa kwa umma wakati nondo alituma taarifa kwa rafiki yake na hivyo kutoangukia kwenye kosa hilo.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA,** SHAMBA EKA 40 MOROGORO. Linafaa kufuga na kilimo, limeshavunwa misimu 3, lina nyumba vyumba 2 na Gari inafika. Bei ml.25 zenye mjadala. Wasiliana 0718965491 / 0784653304 / 0629478005.


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI MADOGO NA: 236/2019**

**JOHN BILISINGI ............MDAI**

**DHIDI YA**
**JUSTINIAN ELIZEUS......WADAIWA**

KWA: JUSTINIAN ELIZEUS
(POPOTE PALE MLIPO)
Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Na: 236/2019 yamepangwa kutajwa tarehe 25.02.2020 mbele ya mwenyekiti wa baraza , R.Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa baraza hili leo tarehe 05.12.2019

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

## KUPOTEA KWA CHETI



AMINA J. JUMA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1382-0001 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia LAKE VIEW Sekondari mwaka 2009.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: KW/RB/8197/2019.

115562802

## PUBLIC NOTICE

**SKYSTARS INSURANCE BROKERS LIMITED** REGRETS TO INFORM YOU THE GENERAL PUBLIC THAT MOTOR INSURANCE CERTIFICATES AND COVER NOTES ISSUED TO US BY ALLIANCE INSURANCE T LIMITED WITH BELOW SERIAL NUMBERS

**8356051 - 8356075**
**9533676 - 9583700**

PLEASE NOTE THE COMPANY WILL NOT BE LIABLE OR RESPONSIBLE FOR ANY MIS USE ARISING OUT OF THE USAGE OF THE ABOVE MOTOR STICKERS

**IF FOUND PLEASE CONTACT:** SKYSTARS INSURANCE BROKERS OR ALLAINCE INSURANCE T LTD OR ANY POLICE STATION **RB CD/RB/2152/2019**

**SHERIA YA UMILIKI WA ARDHI**
**YA MWAKA 1999**
**(SURA YA 113)**

KUHAMISHA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI

MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: HAMIS IBRAHIM MCHECHE

ARDHI: KIWANJA NA. 222 KITALU 'G' ENEO LA MBAGALA

MANISPAA YA TEMEKE JIJINI – DAR ES SALAAM
Taarifa inatolewa kwamba BARUA YA TOLEO YA HAKI YA KUMILIKI ARDHI iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA HAKI YA KUMILIKI ARDHI. Iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa siku 30 tangu tarehe ya taarifa hii ilipotangazwa katika gazeti. BARUA HALISI YA TOLEO ikipatikana, irudishwe kwa MKURUGENZI WA MANISPAA YA TEMEKE S.L.P 46343, DAR ES SALAAM.

F.A. Masoy
AFISA ARDHI MTEULE
MANISPAA YA TEMEKE

115566102

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI
IDARA YA UHAMIAJI

**OMBI LA URAIA**



DAVID MWAMGHUNDA MWADIME mwenye picha hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MKENYA. Nchi atokayo ni KENYA. Shughuli zake ni HOTELIA. Anwani ya Mwajiri ni OCENIC – BAGAMOYO. Yupo nchini tangu 1991. Pamoja na kuishi BAGAMOYO pia amewahi kuishi DSM. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini muombaji asipewe uraia wa Tanzania atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb No. DN AC: 27/340/1094.

AFISA UHAMIAJI WILAYA
BAGAMOYO

115565702

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KINGLION INVESTMENT CO. LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili T 474 CUC KINGLION. Chassis namba LTBPK82B2DIC22108. Engine namba KL157FMI13J22138.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KBM/RB/14036/2019.**

115565902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NYARUBAMBE MGENDI GIRAHUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 242 DLL AUDI. Chassis namba **WAUZZZ8E46A284315.** Engine namba ALTEAA901430.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**NZ/RB/357/2019.**

115566302


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa***

***Kutangaza Nasi***

***Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# RUDIGER ATAKA WABAGUZI KUADHIBIWA

**LONDON,** England

BEKI wa Chelsea, Antonio Rudiger ameshauri Tottenham Hotspur kuwatafuta na kuwaadhibu wale waliohusika na vitendo vya ubaguzi wa rangi kwenye mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa Jumapili.

Mjerumani huyo alihusika kwenye tukio ambalo lilisababisha mchezaji wa Tottenham, Son Heung-min aliyeonyeshwa kadi nyekundu dakika ya 62 na dakika moja baadaye alionyeshwa ishara za kufananisha na nyani.

Chama cha Wanasoka wa Kulipwa (PFA) wameitaka serikali kukomesha ubaguzi wa rangi kwenye soka la Uingereza baada ya mchezo huo ambapo Chelsea walishinda mabao 2-0.

"Kwa uhakika wale waliohusika watafutwe na kuadhibiwa haraka, katika soka la kisasa timu kama Tottenham Hotspur yenye mashabiki wengi uwanjani pamoja na televisheni na kamera za ulinzi, itawezekana kuwatafuta na kuwaadhibu," aliandika Rudiger kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Kama sio, lazima kutakuwa na mashahidi uwanjani ambao waliona na kusikia tukio lile. Ni aibu kwamba matukio ya ubaguzi wa rangi bado yapo hadi mwaka 2019. Upuuzi huu hautakoma?"

Tottenham imebainisha kwamba itachukua hatua "kali inavyowezekana" kama shabiki yoyote atatambulika na kwa kuonyesha ishara za kibaguzi.

Rudiger ni mchezaji wa hivi karibuni kwenye Ligi Kuu England kukumbana na ubaguzi wa rangi kwenye mchezo, huku nyota wa Manchester United, Fred alizomewa na Manchester City mapema mwezi huu.



# *Sarri akataa kuwalaumu washambuliaji wake*

**TURIN,** Italia

MAURIZIO Sarri amebainisha Juventus ilikosa nguvu wakati wakifungwa 3-1 kwenye mechi ya Kombe la Italia (Super Coppa Italia), dhidi ya Lazio, lakini kocha huyo alisisitiza uchaguzi wa Cristiano Ronaldo, Paulo Dybala na Gonzalo Higuain sio wa kulaumiwa.

Bianconeri hao walifungwa na Lazio kwa mara ya pili mwezi huu, wakishindwa kutetea taji la Super Coppa.

Kipigo hicho kilikuja licha ya Ronaldo, Dybala na Higuain kuanza pamoja, kama walivyoshinda dhidi ya Udinese na Sampdoria.

"Tuliingia kwenye mchezo huu kwa kukosa nguvu, na akili," alisema Sarri akiwaambia waandishi wa habari.

"Hii huwa inatokea. Tumesikitishwa na matokeo, tumepoteza, lakini bado tupo kwenye mashindano mengi ya kucheza kwa miezi mitano ijayo. "Kuna hasira, lakini kulia hakuwezi kuwa suluhisho na kumaliza matatizo yaliyopo kwa sasa. "Hatukupoteza kwa sababu ya washambuliaji watatu wa mbele, tuliruhusu bao la tatu licha ya kuongeza mchezaji kwenye safu ya kiungo."

# Solskjaer awabwatukia United kwa kichapo

**MANCHESTER,** England

KOCHA ole Gunnar Solskjaer amekibwatukia kikosi cha Manchester United kwa kucheza vibaya katika kipindi cha kwanza wakati wakifungwa na Watford 2-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, juzi Jumapili.

United iliingia kwenye mchezo huo kwa ajili ya kuendeleza presha ya kubakia kwenye nne bora katika Ligi Kuu England, ikitoka kupata sare na Everton.

Lakini kwenye mchezo huo uliopigwa pale Vicarage Road walionyesha kiwango kisichovutia, huku wakifungwa mabao ya haraka ya kipindi cha kwanza, huku David de Gea akiusindikiza wavuni mpira uliopigwa na Ismaila Sarr, kabla ya Troy Deeney kufunga kwa mkwaju wa penalti.

Paul Pogba angalau alionyesha uhai kwa mashetani wekundu hao baada ya kuingia kwenye dakika ya 64, lakini hakuweza kubadilisha matokeo ya Watford iliyopo chini ya kocha, Nigel Pearson, ambapo ulikuwa ni ushindi wake wa kwanza.

Solskjaer alionyesha kutoridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na akasema: "Kipindi cha kwanza, ilikuwa rahisi kwao kupata matokeo.

"Tulicheza vibaya, taratibu, bila ari na hata mashabiki walishangilia pale tulipowatoa wachezaji wengine nje na ilionyesha kama tumewazawadia mabao yale mawili.

"Ninafurahishwa kabisa na matokeo ya mchezo huu, tumezungumza na kwamba tunahitaji kuwa na mtazamo chanya zaidi."



## HABARI MICHEZO

# Madrid kutosajili mshambuliaji Januari

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesema Real Madrid "haitaingia sokoni" kumsajili mshambuliaji Januari, baada ya juzi kutoka sare ya bila kufungana dhidi ya Athletic Bilbao.

Madrid ilishindwa kufunga bao na kulazimika kutoka sare tasa kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, La Liga, dhidi ya Athletic pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu Jumapili.

Toni Kroos na Nacho mashuti yao yaligonga mwamba, kabla ya Luka Jovic aliyetokea benchi pia alikosa bao la wazi zikiwa zimesalia dakika chache mpira kumalizika.

Karim Benzema hadi sasa ndiye anayeongoza kwa kikosi cha Madrid kwa kufunga mabao, akiwa ametikisa nyavu mara 12 katika mechi 16 alizocheza hadi sasa, huku Jovic amefunga bao mara moja tu tangu alipotua hapo akitokea Eintracht Frankfurt.

Hata hivyo, Zidane ameondoa uwezekano wa kufanya usajili kwa kikosi hicho cha Los Blancos kipindi cha Januari.

Alipoulizwa kama ataomba kusajili mshambuliaji mpya, Zidane alijibu: "Hapana. Kwa uhakika kabisa hapana, sioni kama kuna uhitaji wa kusajili mshambuliaji."

Sare dhidi ya Athletic umekuwa ni mchezo wa tano kwa Madrid kutofunga bao kwenye LaLiga msimu huu, huku vijana hao wa Zidane sasa wapo nyuma kwa pointi mbili dhidi ya vinara Barca wakati wakielekea kwenye mwaka mpya 2020.

"Nimekasirishwa na hili," amesema Zidane. "Wachezaji wangu wameacha kila kitu uwanjani.

"Naangalia kwa mtazamo chanya na kitu kizuri zaidi cha kufanya. Pointi tatu katika mechi tisa hazitoshi."





# VIEIRA ALIKATAA KAZI YA KUINOA ARSENAL

**LONDON,** England

KOCHA wa Nice, Patrick Vieira, alikataa kufanya mazungumzo na Arsenal ili kuchukua mikoba ya kuinoa timu hiyo kabla ya kuteuliwa kwa Mikel Arteta kama kocha mkuu.

Arteta alitangazwa rasmi kuwa kocha pale kwenye dimba la Emirates Ijumaa na alikuwapo jukwaani Jumapili wakati wakicheza na Everton baada ya kusaini mkataba wa miaka mitatu ya kuchukua mikoba ya Unai Emery.

Mkuu wa soka wa Arsenal, Raul Sanllehi, alisema Mkurugenzi wa Ufundi, Edu alizungumza na "makocha kadhaa wa daraja la juu," mmoja wao akitajwa kuwa ni Vieira.

Nahodha wa zamani wa washika bunduki hao, Vieira alikuwa akihusishwa na mpango wa kuchcukua nafasi hiyo, lakini katika mahojiano na Canal Football Club, alidai hakukuwa na makubaliano yoyote.

Alipoulizwa kama aliwasiliana nao, Vieira, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda kuinoa timu ya David Beckham inayoshiriki Ligi Kuu Marekani, MLS, Inter Miami, alisema: "Hapana. Inavutia kuona jina lako likitajwa sehemu nyingine, lakini mimi nina mkataba na Nice.

"Nimejua tangu nilipokuja hapa kwamba, ni mtu mwenye bahati nataka kuendelea kuhusika na maendeleo ya klabu hii.

"Sina mpango wala mawazo yoyote ya kwenda sehemu nyingine."

Nice ilimaliza nafasi ya saba katika msimu wake wa kwanza chini ya Vieira na sasa ipo nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

# Klopp: Wachezaji Wafaransa ghali

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL haiwezi kuwasajili washambuliaji nyota wa Ufaransa kama vile Kylian Mbappe na Antoine Griezmann kwa sababu ni ghali sana, amesema kocha, Jurgen Klopp.

Vinara hao wa Ligi Kuu England, Liverpool hawana mchezaji Mfaransa kwenye kikosi chao cha kwanza licha ya Les Bleus kushinda taji la Kombe la Dunia mwaka jana.

Mamadou Sakho alikwenda Crystal Palace kwa mkataba wa kudumu Agosti 2017 na hakuna Mfaransa mwenzake aliyehamia Anfield.

"Hakuna sababu kwa hilo," alisema Klopp akiiambia Canal Football Club.

"Kylian anaichezea PSG, Griezmann amejiunga na Barcelona. Kwa uhakika mnajua namna gani timu yao ya taifa ilivyo nzuri.

"Tungependa kuwa na mchezaji wa Ufaransa, lakini wengi wao ni ghali mno kwa upande wetu."

Liverpool watakuwa na mchezaji mpya aliyeongezwa kwenye kikosi chao wakati dirisha la usajili ya Januari litakapofunguliwa baada ya kufikia makubaliano na winga kutoka Japan, Takumi Minamino, anayeichezea Salzburg.

Kikosi cha Klopp kilishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na wikendi iliyopita kimetwaa taji la Klabu Bingwa ya Dunia baada ya kuibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Flamengo mjini Doha nchini Qatar.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MERTENS, VOLLAND WATAKIWA ARSENAL

●●● Ni nyota ambao Arteta anatarajiwa kuwasajili mapema katika...

**LONDON,** England

KATIKA kuhakikisha kuwa anaimarisha kikosi chake, kocha mpya wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema kuwa anataka kumsajili winga wa Napoli na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Dries Mertens, ambaye mkataba wake na klabu hiyo uko katika mwaka wa mwisho.

**Arteta alianza kazi rasmi ya kuifundisha Arsenal Jumapili iliyopita na tayari anaonekana kutaka kuingia sokoni kwa nguvu katika kipindi cha dirisha dogo la usajili cha Januari.**

Klabu hiyo maarufu kwa jina la The Gunners, imeripotiwa tayari kutaka kuwasajili wachezaji nyota wawili, mmoja wao akiwa ni nyota wa Serie A.

Arsenal inataka kurejea kwenye soka la ushindani baada ya sasa kuwa kwenye nafasi ya 11 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England kutokana na sare ya bila kufungana waliyopata dhidi ya Everton.

Nyota wanaotajwa kutakiwa na Arsenal ni pamoja na winga wa Napoli, Dries Mertens, limeandika gazeti la CalcioMercato.

Mertens, ambaye ameonekana kutakiwa na mabingwa mara tano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, anatarajiwa kuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu.

Borussia Dortmund pia inatajwa kuweka nguvu zaidi katika mawindo ya kumsajili nyota huyo mwenye umri wa miaka 32, na kuwafanya Arsenal wawekeze macho yao kwa kusaka mchezaji mwingine ili kujiimarisha.

Mbali na nyota huyo, Arsenal pia imeweka wazi nia yake ya kuwania saini ya Kevin Volland, Sky Sports News imesema kuwa mabosi wa timu hiyo wametuma mawakala wake kwenda kumwangalia mshambuliaji huyo wa Bayer Leverkusen na watali-wasilisha jina lake kwa Arteta.

Arsenal ina nafasi nzuri ya kumpata Mjerumani huyo ambaye amebakiza miezi 18 katika mkataba wake kwa kulipa kiasi kidogo cha ada ya uhamisho.

Volland ambaye amezoea kucheza kama mshambuliaji wa kati, pia ana uwezo wa kupangwa katika nafasi ya winga na kuonyesha kiwango kizuri, endapo kutakuwa na mahitaji hayo.

Katika mazoezi ya kwanza ya Arteta, wachezaji nyota kama Alexandre Lacazette, Nicolas Pepe, Matteo Guendouzi na Mesut Ozil walihudhuria na kuonyesha ushindani wa kuwania namba kwenye kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM AGOMBEWA

MANCHESTER United imeungana na klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu ya Ujerumani maarufu Bundesliga, kuwania saini ya kiungo chipukizi wa England na Birmingham City, Jude Bellingham (16). ***(Telegraph)***

### MATIC SAFARI IMEIVA

UONGOZI wa Manchester United umesema kuwa hautampa mkataba mpya kiungo wa Timu ya Taifa ya Serbia, Nemanja Matic (31), baada ya mkataba wake uliopo kumalizika ifikapo Juni mwakani.***(Express)***

### BARBOSA AIKATAA FLAMENGO

NYOTA anayewindwa na West Ham, Gabriel Barbosa, amekacha kufanya mazungumzo kuhusu hatima yake na klabu yake ya Flamengo ambayo ilipoteza mchezo wa fainali ya Klabu Bingwa ya Dunia dhidi ya Liverpool. Mshambuliaji huyo Mbrazil mwenye umri wa miaka 23 anaichezea klabu hiyo kwa mkopo akitokea Inter Milan. ***(Goal)***

### EVERTON KUSAJILI WAPYA

EVERTON imemwahidi kocha wake mpya, Carlo Ancelotti, itampatia fedha kwa ajili ya kusajili wachezaji wapya katika dirisha dogo la Januari baada ya Mtaliano huyo kuanza maandalizi ya kukiimarisha kikosi hicho cha Goodison Park. ***(Star)***

### ZLATAN KUIBEBA MILAN

MSHAMBULIAJI raia wa Sweden, Zlatan Ibrahimovic, anatarajia "kuongeza hamasa na nguvu" katika kikosi cha AC Milan, amesema Kocha Mkuu wa timu hiyo, Stefano Pioli, lakini mchakato wa nyota huyo kutua klabuni hapo bado haujakamilika. ***(DAZN, via Goal)***

### SHEFFIELD KUJIIMARISHA EPL

KOCHA wa Sheffield United, Chris Wilder, amesema kuwa klabu hiyo inahitaji kuongeza nguvu kwa kufanya usajili katika kipindi cha dirisha dogo la Januari ili kuhakikisha wanaendelea kuwa na matokeo mazuri kwenye Ligi Kuu England. ***(Sheffield Star)***

### PAQUETA ANUKIA PSG

PARIS St-Germain imeweka wazi kuwa inataka kumsajili kiungo wa AC Milan Mbrazili Lucas Paqueta, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(RMC Sport - French)***

### NUBEL KUONDOKA SCHALKE

GOLIKIPA na nahodha wa Schalke, Alexander Nubel, anatarajia kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu. Imeelezwa kuwa mlinda mlango huyo mwenye umri wa miaka 23, anawindwa na klabu kubwa za Ulaya. ***(Mail)***

### BILIC AMWACHA HEGAZI

BEKI wa West Brom na Timu ya Taifa ya Misri, Ahmed Hegazi (28), ameachwa katika kikosi cha Slaven Bilic, kufuatia kupata majeruhi akiwa kwenye mazoezi ya timu hiyo. ***(Express & Star)***

### MANDZUKIC ATUA QATAR

STRAIKA wa zamani wa Juventus na Croatia, Mario Mandzukic (33), tayari ameshatua Qatar kabla ya usajili wake wa kujiunga na Al-Duhail ukiwa haujakamilika, nyota huyo pia anawindwa na Manchester United. ***(Sky Italia)***

HABARI MICHEZO

## Zimamoto yaweka mipango hadharani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Klabu ya Zimamoto inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar umesema kuwa hawana mpango wa kusajili wachezaji wapya katika kipindi cha dirisha dogo kwa sababu kikosi chao kimekamilika.

Katibu Mkuu wa Zimamoto, Ali Jongo, alisema kuwa kikosi chao kina wachezaji wenye uwezo na wanaamini wataendelea kupambana kuhakikisha wanatwaa ubingwa wa ligi hiyo.

Jongo alisema wachezaji waliopo katika kikosi hicho wanaweza kukabiliana na kasi ya Ligi Kuu Zanzibar na wanachojiimarisha ni kuwekeza nguvu zaidi kwenye kukamilisha vema programu za mazoezi.

Alisema kuwa wamebaini upungufu mdogo mdogo katika mzunguko wa kwanza na wanajiandaa kuufanyia kazi kwenye kipindi cha mapumziko na hivyo wanaamini watarejea wakiwa imara zaidi.

"Timu ipo vizuri, ndio maana hatuweki nguvu katika suala la kufanya usajili wakati huu wa dirisha dogo, nipo nafasi ya pili lakini aliyeko kileleni tumepishana kwa alama moja tu, hivyo bado tuna nafasi ya kufanya vizuri zaidi," Jongo alisema.

Zimamoto ipo nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 25 baada ya kucheza michezo 10, baada ya kushinda mechi nane, kutoka sare mara moja na imepoteza mechi moja pia.

# YANGA YAFUNGUKA KILICHOMZUIA YIKPE

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya mshambuliaji raia wa Ivory Coast, Gislein Yikpe, kuipa Yanga saa 24 ili kukamilisha usajili wake, uongozi wa klabu hiyo umesema kuwa kiwango cha mchezaji huyo ndio kimesababisha mchakato wa kumpa mkataba usifanyike haraka.

**Yikpe alikaririwa katika vyombo mbalimbali vya habari akitaka kupewa mkataba na hayuko tayari kufanyiwa majaribio kama ambavyo mabosi wa Yanga walivyohitaji.**

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, alisema kuwa uamuzi wa kutaka mshambuliaji huyo afanyiwe kwanza majaribio, ni kujiridhisha na kiwango chake.

Nugaz alisema kuwa kwa sasa Yanga iko makini katika usajili wake ili kutorudia makosa yaliyojitokeza kwa kusajili wa wachezaji ambao hawakuwa na viwango bora.

"Tulimwita ili aje tumtizame kwanza, tuone kama ataweza kuendana na hali ya Yanga, mazingira ya Yanga, na yale yote ambayo yanazungumzika, ikiwamo mazungumzo ya kifedha na baada ya kujiridhisha ndio tumpe mkataba, hatutaki kurudia makosa yaliyojitokeza huko nyuma," alisema Nugaz.

Aliongeza kuwa mshambuliaji huyo kutoka Gor Mahia, bado makali yake katika kufumania nyavu si ya kiwango cha juu.

"Kiwango chake si cha kudumu, amefunga goli moja katika mechi sita, wewe unajiuliza huyu tukimchukua, atatusaidia, hatutaki tukosee kama tulivyokosea, hata Ambani (Boniface), ameonyesha kutokuwa na imani na kiwango chake," Nugaz aliongeza.

Wachezaji wapya ambao wamesajiliwa na Yanga katika kipindi hiki cha dirisha dogo ni pamoja na Ditram Nchimbi kutoka Polisi Tanzania, Adeyum Saleh (JKT Tanzania), na Haruna Niyonzima, ambaye alirejea kwao Rwanda kuitumikia AS Kigali.

Yanga inayofundishwa na Kaimu Kocha Mkuu, Boniface Mkwaza, leo inatarajia kushuka ugenini kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya kuwakabili wenyeji Mbeya City katika mchezo wa Ligi Kuu Bara na Ijumaa itateremka kwenye uwanja huo huo kuwavaa Tanzania Prisons.



Mashabiki wa Yanga wakimsalimia mshambuliaji raia wa Ivory Coast, Gislein Yikpe, wakati wa mchezo wa Kombe la FA Tanzania dhidi ya Iringa United uliochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Usajili Kilimanjaro Marathon mambo yameiva*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI msimu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya ukiwa umewadia, washiriki wa mbio za Kilimanjaro Marathon wanakumbushwa kujisajili kabla ya ada ya ushiriki wa mbio hizo haujapnda.

Taarifa iliyotolewa na waandaaji wa mbio hizo, wanasema kuwa punguzo la bei kwa wanariadha watakaoshiriki mbio za kilomita 42 na 21 linatarajiwa kukamilika Januari 14, mwakani.

Taarifa hiyo iliongeza kuwa usajili umekuwa ukiendelea kwa njia ya mtandao na Tigopesa na kuwataka washiriki waendelee kujisajili hata wakati wa sikukuu ili wajihakikishie punguzo la ada ya ushiriki katika muda uliotangazwa na pia kupata namba za ushiriki.

"Washiriki wote wanatakiwa kujisajili kwa kupitia www.kilimanjaromarathon.com na kwa Tigopesa kwa kubonyeza *149*20#," ilisema taarifa hiyo iliyotolewa na Mratibu, John Bayo.

Mkurugenzi huyo alisema kwa kupitia taarifa hiyo kuwa kuna idadi maalumu ya washiriki inayotakiwa kwa mbio zote tatu (Kili marathoni, half marathon (mbio za Tigo kilomita 21) na mbio za kilomita tano zinazodhaminiwa na kinywaji cha Grand Malt ili kuhakikisha wanatimiza viwango vilivyowekwa na Shirikisho la Kimataifa la Riadha (IAAF).

Bayo alisema pia watahakikisha washiriki wanafurahia mbio hizo bila ya msongamano na kuwapa nafasi kwa waandaaji kutoa huduma zinazotakiwa katika njia zote za mashindano hayo kuanzia mwanzo hadi sehemu ya mwisho ya kumalizia.

"Kuhusu punguzo la bei, tunatoa wito kwa washiriki wachangamkie utaratibu huo ambao ulianza Oktoba Mosi mwaka huu na utamalizika Januari 14, 2020," alisema Bayo.

Aliongeza kuwa mchakato wa usajili utafungwa rasmi ifikapo Februari 16, mwakani au pale idadi ya washiriki wanaohitajika itakapotimia.

Alivitaja vituo vilivyopo vya kujiandikisha ni pamoja na Mlimani City ambapo usajili utafanyika kati ya Februari 22 na 23, mwaniani wakati jijini Arusha wenyewe watajisajili kwenye hoteli ya Kibo Palace kati ya Februari 25 na 26 na Mjini Moshi zoezi hilo litaendeshwa kati ya Februari 27 na 28, mwaka huu.

"Washiriki watatakiwa kujitambulisha na kuthibitisha kuwa wameshalipia kabla ya kukabidhiwa namba zao," Bayo aliongeza.

Naye Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Pamela Kikuli, amewataka washiriki wa mbio za kilomita 42 wajitokeze kwa wingi, wajisajili na kufanya mazoezi ili kuhakikishia wanamaliza katika nafasi nzuri na kuzibakisha zawadi hapa nyumbani.

Mbio za Kilimanjaro Marathon zinazoandaliwa na Kampuni ya Wild Frontiers na kuratibiwa na Executive Solutions, zinatarajiwa kufanyika Machi Mosi mwakani, kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

# Michezo


Jumanne Desemba 24, 2019

Nipashe



Madrid kutosajili mshambuliaji Januari

HABARI UK.29




Winga wa Chelsea, Willian (kulia), akifunga bao la pili kwa penalti katika mechi ya Ligi Kuu England huku golikipa wa Tottenham, Paulo Gazzaniga, akishindwa kuzuia shuti hilo. Chelsea ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA, MBEYA CITY HAPATOSHI

## ●●● Mkwasa atamba nyota wake wameimarika, huku Amri akijipanga...

**Na Somoe Ng'itu**

HUKU joto la mechi ya watani wa jadi nchini likiwa limeanza kushika kasi, Kocha Mkuu wa Yanga, Boniface Mkwasa, amesema kuwa anataka kuona kikosi chake kinapata ushindi mnono katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City, utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

**Yanga itashuka uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Iringa United katika mashindano ya Kombe la FA wakati Mbeya City wao imewaondoa Migombani kwa penalti 3-2 baada ya kutoka sare ya bao 1-1 katika dakika 90 za kawaida.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mkwasa maarufu "Master", alisema kuwa ana matumaini malengo ya kupata ushindi yatatimia, kutokana na wachezaji wake kufuata vema maelekezo yanayotolewa na benchi la ufundi.

Mkwasa alisema kuwa anahitaji kuona wanaibuka na ushindi, licha ya kujiandaa kukutana na ushindani kwa sababu wenyeji wao hawajapata matokeo mazuri katika mechi zao zilizopita za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema kuwa wachezaji wote wa timu hiyo walioko jijini Mbeya, wako tayari kwa mchezo huo wa kiporo na anafurahishwa na hamasa iliyoko kwenye kikosi hicho.

"Kwa kiasi kikubwa wanafanya kile ambacho tunakielekeza mazoezini, tuna mwelekeo mzuri, sasa hivi wanafunga mabao mengi tofauti na ilivyokuwa huko nyuma, malengo yetu ni kuhakikisha tunashinda vema mchezo huu na mingine ya viporo," alisema Mkwasa.

Alisema kasi ya kupata ushindi mnono iliyopo, inaonyesha kuwa ni dalili njema katika kikosi hicho kuwa mambo yako vizuri na anawaomba mashabiki na wanachama wa timu hiyo waendelee kuwapa ushirikiano.

Kocha wa Mbeya City, Amri Said, amesema wamejipanga kucheza kwa tahadhari na hiyo inatokana na kikosi cha wapinzani wao kuwa na wachezaji wenye uzoefu na ligi pamoja na mashindano mbalimbali.

Said amesema mechi hiyo inatarajiwa kuwa ngumu na ushindani katika pande zote mbili, kutokana na kila timu kuhitaji kutimiza malengo yake.

"Tumejiandaa na tumejipanga vizuri, tunaijua Yanga na wao wanaijua Mbeya City, tutaingia uwanjani tukifahamu ubora na upungufu wa wapinzani wetu, ni timu kubwa, tunawaheshimu pia, lakini kikubwa tusubiri dakika 90 ndio mwamuzi wa kila kitu," alisema beki huyo wa zamani wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu, Simba.

Baada ya mechi ya leo, Yanga itaendelea kubakia Mbeya kwa ajili ya kusubiri mchezo mwingine wa ligi hiyo dhidi ya "Maafande" wa Tanzania Prisons, ambao utachezwa Ijumaa.

# Ajibu afichua siri ya ushindi

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Ibrahim Ajibu, amesema kuwa umakini mkubwa ulioonyeshwa na wachezaji wa timu hiyo, ndiyo siri ya kupata ushindi mnono wa mabao 6-0, katika mechi ya Kombe la FA dhidi ya Arusha FC, uliochezwa juzi jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo Ajibu, alikataa kuzungumzia mchezo wao dhidi ya Yanga, unaotarajiwa kuchezwa ifikapo Januari 4, mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ajibu, alisema kuwa marekebisho yaliyofanywa katika benchi la ufundi yamewasaidia wachezaji wa kikosi hicho kuimarika na hatimaye kufanya vema kwenye mchezo huo wa mtoano.

Ajibu alisema kuwa yeye, pamoja na wachezaji wenzake wanaitazama mechi inayofuata dhidi ya Lipuli na kamwe hawaifikirii Yanga ambayo watakutana nayo baadaye mwakani. Alisema kuwa umakini huo ndio umesababisha wao kupata matokeo mazuri na hivyo kusonga mbele katika michuano hiyo.

Hata hivyo, Ajibu, alikataa kuzungumzia mipango ya timu hiyo kuelekea mechi ya watani wa jadi ambayo joto lake limeshaanza kusambaa kwa mashabiki na wanachama wa timu hizo mbili kongwe hapa nchini.

"Leo (juzi), tulikuwa makini zaidi na mechi, ...siwezi kufikiria mechi ya Januari 4, kwa sababu hapa kuna michezo mingine mitatu iliyoko mbele yetu, huwezi kuufikiria mchezo huo, lazima kwanza tucheze michezo hii, halafu tuanze kuifikiria Yanga, sina lolote, tunajipanga hadi hiyo siku itakavyofika, tutajua nini kitatokea," alisema Ajibu.

Vinara wa Ligi Kuu Bara, leo wanatarajia kuendelea kujifua kwa ajili ya kuwakaribisha Lipuli FC kutoka Iringa, katika mchezo wa ligi hiyo unaotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >